

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Februari, 2011

(Kikao Kilanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Leo ni siku ya Alhamis tunaanza na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna watu wengi sana wanataka kuuliza, hapa tutakwenda kwa mujibu wa vyama, jinsia na pande tunazokwenda. Lakini kwanza kabisa tutaanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Mbewe, ngoja waingie, mnaoingia mnaingia kwa utaratibu na kimya. Mheshimiwa Mbewe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa yamejitokeza matukio mengi sana ya askari kupiga risasi raia na kwa sababu katika matukio haya raia kadhaa wamepoteza maisha yao katika maeneo mbalimbali hususani ukizungumzia suala la Arusha Mjini tarehe 5 Januari, 2011 na kule Mbarali, Mbeya; na katika matukio mengi Serikali haijawahi kutoa taarifa yoyote ya kina kuhusiana na vifo hivi na kwa sababu Taifa bado linaomboleza vifo hivi na vingi ambavyo vinatokea kwa sababu ya watu kupigwa risasi, je, katika hatua ya sasa Serikali inaweza kutoa tamko rasmi kuhusiana na vifo vya Arusha sambamba na kuhitaji kujiuzulu kwa wale wote waliohusika akiwemo Waziri wa Mambo ya Ndani na Inspeksi Jenerali wa Polisi? (*Makofifi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwamba Mheshimiwa Mbewe ameamua ye ye mwenyewe kuliulizia hili. Lakini nataka niseme tangu mwanzo kwamba Serikali hii ni makini sana. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, ukiona jambo limetokea kama ilivyotokea pale Arusha usikimilie tu kusema Serikali, Serikali. Ni vizuri ukauliza nani aliyesababisha mauaji hayo?

Mheshimiwa Mbwe, katika hili mimi nasikitika sana kwamba tumepoteza maisha ya Watanzania watatu bila sababu. (*Makofi*)

Mliomba wenyewe mfanye maandamo, hatukukataa, mkakaa na askari pale mkaelewana vizuri. Mkakubaliana kwamba sisi tunafikiri ili tuweze kuwadhibiti vizuri na kuwalinda vizuri, tutumie *route* moja tu. Wenzangu nyie mkakataa, tukasema *okay*, sasa kama ni hivyo sisi hatuwezi kufanya hiyo kazi katika mazingira ambayo mnataka tufanye, kwa hiyo, hata hayo maandamano ambayo mlikuwa mmeifikiria tuyafanye, tukaamua kwamba namna tunavyopima upemo, hapa kunaweza kutokea vurugu kubwa sana.

Arusha yenyewe unaijua, vibarabara vyenyewe unavielewa, tukasema tunaruhusu Mkutano uendelee kufanya na watu waende kwenye Mkutano kama tunavyokwenda kwenye Mikutano mingine yoyote. Mkasema hapana, sisi tunaandama. Sasa mkaamua kufanya maandamano yale bila kujali kabisa kwamba utaratibu uliokuwa wamekubaliana mmeukiuka wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sasa kilichotokea pale ni namna ya kuzuia hayo maandamano, hatua ya kwanza. Baadhi yenu mlikamatwa kwa sababu mliongoza kwenye maandamano. Mkatawanyika, tukashukuru kwamba mlikwenda kufanya mkutano, mkaaliza. Lakini matamshi yaliyotoka kwenye mkutano ule si matamshi kweli ya chama ambacho kweli mnadhamiria kujenga nchi yenze amani. (*Makofi*)

Mmetoa matamko pale, mnawataka wanachama wenu watoke pale kwenye mkutano Mheshimiwa Freeman Mbwe waende kuwakomboa wale viongozi waliokuwa wamekamatwa, mkutano wenyewe watu zaidi ya elfu mbili, elfu tatu, na kweli mkaamua kwenda, kituo cha polisi.

Mheshimiwa mlipokuwa mnakwenda ni kituo cha polisi kikubwa, kina silaha, kina mabomu, kina nini na mambo mengine mengi tu. Lakini bado polisi walijitahidi sana kujaribu kuwa na staha, kuwaonya jamani, chonde chonde na wakaanza na vitu vidogo vidogo tu kupiga mabomu kidogo ya moshi, jaribu hiki, lakini bado mkaenda. Mpaka mmekaribia mita 50 muweze kuingia kwenye kituo cha polisi. *Police was left with no option* kwa kujua tu kwamba kama mkiingia hatujui litakalotokea ni kitu gani. Katika purukushani ile, maskini wale Marehemu wale watatu wakapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika sana kwa sababu ni kitu ambacho hakikuwa na sababu ya kutokea. Kwa hiyo, kwa sehemu kubwa kama Mheshimiwa Mbwe na chama chako, mngeamua kushirikiana na Serikali hii mkafanya ule mkutano kama tulivyokubaliana haya yote yasingetokea. (*Makofi*)

Tatizo la Mbeya lina maelezo tofauti kidogo, kwa sababu mara nyingi haya mambo yanatokana na watu kujichukulia sheria mkononi, wakati mwengine kufanya fujo za nguvu, polisi wanajitahidi kufanya hili na lile, wakati mwengine inashindikana. Kwa hiyo, muda wote ujue kwamba kuna kitu kimesukuma askari mpaka kikawafikisha pale. Rai yangu kwako, Chama cha CHADEMA tushirikiane na muda wote tujue kabisa

kwamba tunalo jukumu kama Watanzania wote ninyi na sisi kwamba ni lazima tujitahidi kujenga Taifa tulivu, Taifa lenye amani ili tuweze kweli kuendesha nchi hii vizuri. (*Makofi*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sababu ni haki ya kiraia ya kila mtu kuishi, na kwa sababu watu wamepigwa risasi na wamekufa na kwa sababu huwezi kumuhukumu mtu bila kumsikiliza, swali; kama Serikali imepewa maelezo ya polisi na Serikali haijaona umuhimu wa kupata maneno ya upande wa pili, lakini imependa kuhukumu na kuna taarifa za kina ambazo zingesaidia Taifa hili kuweka misingi ambayo polisi hawatakwenda kuua raia bila sababu za msingi.

Je, ni lini Serikali itakubaliana na sisi kwamba ili kuondoa utata wa kudumu wa suala hili na masuala mengine yote katika Taifa letu, ni lini itaunda *Judicial Commission of Inquiry* kutafuta ukweli kutoka pande zote mbili na vile vile kuchukua hatua kwa wale wanaohusika? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, labda nirejee nilichosema. Mimi nina hakika kabisa Mheshimiwa Mbewe kama dhamira yako ni nzuri kiasi hicho, wala lisengengoja liletwe mpaka Bungeni kumuuliza Waziri Mkuu kana kwamba hakuna namna nydingine nzuri ambazo ungeweza kufikisha wazo hili Serikalini, pale unapoona kwamba liko jambo ambalo linastahili. Sasa umekuja umelitumbukiza hapa, unataka uchunguzi ufanyike, sawa. Uchunguzi unaweza ukafanyika kwa utaratibu wa kawaida, lakini kuamua tufike pale ni lazima vilevile na sisi tujiridhishe kwamba ziko sababu za kutosha za kutufanya tuanzishe uchunguzi huo. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma huanzia katika uandaaji wa Bajeti, na kwa kuwa hivi sasa matumizi yasiyo na tija kama posho za safari ya ndani na nje ya nchi, posho za kujikimu, mafuta na gharama zingine mbalimbali ambazo ziko Serikalini zinafikia asilimia 35 ya makusanyo ya fedha yote ya Serikali. Je, Serikali imejipanga vipi katika Bajeti hii inayokuja kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili fedha hizo zielekezwe katika shughuli za maendeleo yanayoleta tija kwa wananchi kama kilimo, ujenzi wa viwanda, shule, zahanati na kadhalika ili Watanzania wengi wanufaikie wakiwemo Watanzania wa Kisesa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mpina ni jambo ambalo nimekuwa nalisema na yeche naona analisema vilevile, lakini nadhani ushauri wake ni mzuri kwamba maadamu jambo hili litaletwa hapa kwenye Bunge lako Tukufu, kama Serikali tutafanya makosa ya kurundika matumizi ambayo si ya lazima, jukumu la Bunge liwe ni kuibana Serikali kuhakikisha vipengele hivyo vinaondolewa kwa manufaa ya Watanzania. Sisi tutajitahidi sana, lakini Bunge nalo lazima nalo liwe macho, msije mkapitisha vitu ambavyo baadae tena tunaulizwa maswali. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Serikali inapoletwa katika Kamati au katika Bunge huwa haina *details* zake kwa mfano inasema

posho ya safari za nje ya nchi shilingi bilioni 10 lakini hakuna *details* zake, je, Serikali itakubali sasa kuanzia sasa Bajeti ya Serikali zinapoletwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na zinapoletwa kwenye Kamati za Kisekta zitakuwa na *details* ya maelezo halisi ya fedha hizo zimetengwa kwenda kufanya nini?

SPIKA: Sijui kama Waziri Mkuu anakwenda moja kwa moja na *details* hizo, mimi nadhani kipindi cha Bajeti kipo na tutaweza kupata hayo unayozungumza Mheshimiwa Mpina. (*Makofi*)

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa nchi yetu inatawaliwa kwa msingi wa mfumo wa vyama vingi vya siasa; na kwa kuwa Halmashauri katika mfumo wa Serikali za Mitaa zinazoongozwa na Vyama vya Upinzani; na kwa kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa wana wajibu kisheria kuziwezesha na kuzisaidia Halmashauri hizi kutimiza wajibu wake; je, kwa vipi Wakuu hawa wa Mikoa na Wilaya watazitendea haki Halamashauri zinazoongozwa na Upinzani na huku wao ni Makada wa CCM na Wajumbe wa Kamati za Utendaji za CCM, Mikoa na Wilaya? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Kiwia zima simu yako.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mfumo wa Serikali ulivyo ndivyo ulivyo kwa sasa. Mkuu wa Mikoa, Mkuu wa Wilaya anatakiwa kuhakikisha kwamba anatekeleza Ilani ya Chama inavyotakiwa...

SPIKA: Leo naona hawataki ujibu maswali, niombe sijui uhamie wapi, eh! Labda pale. Wanakuambia kwa nini huendi CHADEMA huko? (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeanza kueleza kwamba mfumo ulivyo kwa sasa ndiyo unaoweka utaratibu wa Wakuu hawa kuonekana kama vile ni Mawakala wa Chama cha Mapinduzi. Lakini msingi wake mkubwa ni kwamba Serikali ndiyo inayotekeleza kutoka kwenye Chama kilichoshinda na wala huwezi ukahamishia lawama hizo kwa Mkuu wa Mikoa na Mkuu wa Wilaya peke yake kama hoja ndiyo hiyo. Hata Rais ndiyo Rais wa Chama vile vile, ndiyo Mwenyekiti wa Chama, Waziri Mkuu ni Mjumbe wa Kamati Kuu na kadhalika na kadhalika. Lakini lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba yale yaliyoahidiwa na Chama na kukabidhi Serikali inayohusika kuwepo na muingiliano wa kutosha wa namna ya kusukuma maendeleo. Mengine yote ni matokeo tu ya utendaji kazi, unaweza kukuta Mkuu wa Mikoa au DC mmoja ana mapungufu hapa na pale, lakini kimsingi anatakiwa kufanya kazi ya kusukuma maendeleo kwa mujibu wa ahadi zilizotolewa.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Swali langu kwa sehemu kubwa, nilitaka kujua vurugu na matukio ya kutisha yaliyotawala katika uchaguzi wa Meya wa Jiji la Arusha na kwa kuwa Watanzania walio wengi tukiwemo na sisi Wabunge hatukuja ni nini hasa kilichojiri na kupelekea vurugu

na matukio haya ya kutisha ili Watanzania ikiwezekana wasiendelee na mtindo huo ambao kwa nchi ni jambo geni. Sasa kwa kuwa kwa sehemu kubwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amejibu wakati akijibu swali la Mheshimiwa Freeman Mbowe, lakini bado tunataka sisi kuielewa kwa kina na hasa sisi jirani zao wa Mkoa wa Manyara kuelewa ni tatizo gani lilitokea na kuleta vurugu kama hizo na pili sasa, je, nini msimamo wa Serikali kwa yule Meya na Naibu Meya ambae alichaguliwa katika uchaguzi huo wa Meya wa Jiji la Arusha?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali tunasikitika kwa ajili ya hivi visemea. Inaelekea kuna mtu amewasha mashine mahali, muangalie kila mtu kisemea chake kama kinawaka.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Martha Umbulla kwa swalii lake, hili ni eneo lingine linalosikitisha sana, Baraza la Madiwani la Manispaa ya Arusha kama zilivyo Halmashauri nyingine zilipanga kwamba mkutano wao kwanza ufanyike tarehe 17 Desemba, 2010. Wajumbe walipata taarifa wote wakahudhuria kikao cha tarehe 17, jumla yao wajumbe ni 31. Katika 31 hawa *TLP* Mjumbe mmoja, CHADEMA Wajumbe 14, CCM ilikuwa na Wajumbe 16. (*Makofi*)

Mkutano umeanza wajumbe wote 31 wakiwepo, zikaanza hoja kwamba sawa, anayetaka kwenda kuapishwa lakini kwanza tunataka ufanuzi, huyu Mheshimiwa Mary Chatanda ambaye ni Katibu wa Chama Mkoa wa Arusha na Mbunge Viti Maalum anaingiaje kwenye mkutano huu? Na sisi CCM tukasema; “Na ninyi mnaye Mheshimiwa Rebecca Mngodo, ye ye hajaapishwa Bungeni, Viti Maalum anaingiaje hapa? ” (*Makofi*)

Ubishi ule tukalazimika sasa pale Manispaa kuielekeza, ombeni ushauri mmoja kutoka Katibu wa Bunge lakini ulizeni na Tume na ikiwezekana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ufanuzi ukatoka kwamba Mheshimiwa Rebecca Mngodo ni Mbunge halali na Mheshimiwa Mary Chatanda ni Mbunge halali na kwa hiyo ni Wajumbe halali kwenye mkutano huo. Ubishi huu ulichukua siku nzima mpaka jioni hawajaelewana. Lakini kwa sababu ilibidi tufanye mawasiliano hatimaye jioni kabisa ufanuzi ukawa umepatikana, wakapewa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wakakubaliana kwa nia nzuri tu, kwa sababu imeshafika saa 12 jioni na zaidi kidogo kwamba kwa sababu taratibu zinasema saa 12 jioni na bahati mbaya siku ile umeme ukakatika jioni ile wakakubaliana mkutano ule uendelee kesho yake tarehe 18 Desemba, 2010 saa 4.30 asubuhi na kila mjumbe akapewa barua. (*Makofi*)

Kwa mujibu wa Sheria ili mkutano ule uwepo ni lazima akidi itimie. Bahati nzuri wote 31 walikuwepo. Kesho yake sasa saa 4.30 asubuhi imefika wakawepo wajumbe 17, 16 wa CCM, mmoja *TLP*. Wajumbe wa CHADEMA wakawa wanakuja lakini wanatoka. Wanakuja kila anaeingia anatoka, aah, mkutano ukasema bwana tusipoteze muda tuendelee. Wakaendelea na mkutano ule siku ile kwa sababu ulikuwa umeahirishwa jana yake. Wakapiga kura Meya kutoka Chama cha Mapinduzi akashinda. Walikuwa wanashindana mmoja wa CHADEMA, mmoja wa CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakaingia awamu ya pili ya kumtafuta Naibu Meya, wakapiga kura, Mjumbe kutoka *TLP* akashinda, CCM alishindwa hakupata kura hata moja, CHADEMA hawakupata hata kura moja, wakati huo ilikuwa kama saa 7.00 mchana. Ndipo akaingia Mheshimiwa Mbunge Godbless Lema na wajumbe wengine wawili pale kwenye ukumbi wa kikao. Kwa maelezo niliyopewa mimi ameingia pale kwa ukali kwamba sasa ni zamu ya CHADEMA kufanya uchaguzi, tuweke Meya wetu. Wakamwambia hapana, hatuwezi kufanya hivyo. Kulikuwa na fujo fujo hivi, ikabidi polisi waagizwe kuja kumwondoa. Baada ya pale wajumbe wa mkutano ule wakaona katika mazingira hayo wacha tuahirishe tukapumzike. Mkutano ukaahirishwa mpaka utakapopangwa tena. (*Makofi*)

Sasa baada ya pale ndipo tukapata hizo taarifa sasa za maandamano ndiyo yalikuja kufanyika na katika taarifa tulizopewa, moja ilikuwa ni kwamba wanapinga matokeo ya uchaguzi wa Meya na Naibu Meya na mambo mengine. *Okay*, lakini tukasema kuna haja gani kama ni maandamano kama jambo hili liliyvo si kwenda tu Mahakamani mkalalamika likaamuliwa likaisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini halikufanyika hivyo, sasa niseme hivi, yaani hata kwa hesabu tu za kawaida za mtoto wa darasa la kwanza hakuna namna ambavyo kwa hali ilivyokuwa kwamba mna CHADEMA Wajumbe 14, una CCM 16 utashindaje? (*Makofi*)

Sasa kwa sababu hoja hii ilikuwa ni kubwa na hakuna namna nyingine ya kuweza kuitatua ikaonekana suluhu labda hiyo ya maandamano na njia nyingine, mimi nasema hazikuwa lazima sana. Sasa kulikuwa na jitihada kwamba wakutane wazungumze. Mimi nikawaambia hapana mtakutana kuzungumza mnazungumza nini? Hili jambo la kisheria tu. Kwa hiyo, kama kuna mtu ana tatizo aende Mahakamani, alalamike pale Mahakama itaamua tu na wakiamua sisi tutaheshimu kabisa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nataka tu nimalizie kwa kusema ukiniuliza mimi na kwa kuwa nilikuwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, utaratibu uliofuatwa ulikuwa sahihi kabisa, haukukosewa kitu chochote. Meya ni halali kabisa na alipatikana kihalali kabisa. (*Makofi*)

Baadaye ndipo Naibu Meya alikuja akasema kwenye vyombo vya habari kwamba amejitoa. Lakini sisi hatujapata taarifa yoyote ya maandishi kwamba kajitoa. Matumaini yangu ni kwamba atafika mahali ata-*register* kwa maandishi ili tuweze sasa kuchukua hatua nyingine ya kutangaza nafasi hiyo iweze kufanyika. Kwa kifupi naweza nikasema ndiyo maelezo niliyonayo. (*Makofi*)

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, swali dogo tu. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa sasa suala hili limeeleweka kwa upana zaidi. Lakini kwa kuwa tunaelewa kwamba suala hili kwa sehemu kubwa liko Mahakamani, lakini tumelielewa kwamba kuna sababu iliyopelekea vurugu hizo na hata kupoteza maisha kwa baadhi ya vijana wetu. Je, Serikali sasa inachukua hatua gani kwa

chama kilichohusika cha CHADEMA kuwaadhibu ili tukio kama hilo lisirudie katika chaguzi za nchi yetu?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi nadhani hili wala si suala pengine la kusema ichukue hatua dhidi ya CHADEMA, hapana. CHADEMA ina wajumbe watu wazima, wasomi wazuri. Mimi nadhani kubwa ni wao tu kufika mahali waone kwamba wanalo jukumu la kujenga chama cha kuaminika, chama ambacho hata kikikabidhiwa madaraka mwaka kesho watasema tumewapa watu ambao wanaweza wakaongoza nchi vizuri. (*Makofi*)

kwa hiyo, mimi nataka niwasih sana, hata haya matokeo mengine yote kususia kwenda kwenye matokeo ya uchaguzi pale, kususia kuja kwenye hotuba, juzi hapa wameshindwa kwenye ajenda ni kushindwa tu, wametoka nje. *Behaviour* hii haiwezi kuwa ndiyo ya kujenga chama kizuri. Nataka niwaombe sana, hili hatuwezi kama Serikali tukasema tutachukulia hatua CHADEMA, kikubwa ni kwamba wananchi wenyewe wataendelea kuona chama kinavyokwenda na hatua wanazochukua, halafu wataamua tu. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi tulipata *briefing* juu ya hali chakula nchini, lakini vile vile tumeona katika taarifa mbalimbali kwamba hali ya chakula duniani siyo nzuri. Lakini leo tumeputa taarifa nyingine ya kutisha zaidi kwamba hata hali ya mafuta wazalishaji wakubwa kama Saudi Arabia hali yao siyo nzuri na wakubwa wanaanza kufikiria kwamba kutakuwa na tatizo kubwa la nishati. Serikali inachukua hatua gani za dharura kuona tunaikabili hali hiyo ili kupunguza ukali wa maisha ya wananchi? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mhesihmiwa Spika, ni kweli kabisa anachokisema Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed juu ya kupanda kwa gharama kwa ujumla tu za maisha kutoptana na mambo fulani fulani na *of course* ni hili la mafuta na bei ya mafuta sasa hivi kwa *metric tone* ni karibu dola 730, kidogo iko juu. Sasa na hiyo ita-trigger bei za vyakula vile duniani kupanda, ukichanganya na matatizo sasa ya mabadiliko ya tabia nchi tatizo linakuwa kubwa zaidi. Hapa Tanzania tunayo bahati kidogo tu kwa sababu msimu uliopita hali ya hewa ilikuwa nzuri zaidi, angalau tuliweza kuzalisha chakula cha kutosha, tunayo akiba angalau ya kuweza kutusukuma kwa miezi kadhaa bila matatizo yoyote. Lakinii bado haitupi matumaini makubwa sana na nalisema hili kwa sababu kwa maoteo ya kitaalam kutoka Idara ya Hewa inaonekana kama Taifa mvua zetu zitakuwa chini ya wastani kwa maeneo mengi, kitu hicho kidogo si kizuri sana. Tutakuwa na maeneo machache ambayo yanaweza kufanya vizuri. Kwa hiyo, nilichofanya baada ya kupata ile taarifa pamoja, ilikuwa ni kuwapelekea Wakuu wa Mikoa taarifa yote ili kila Mkuu wa Mikoa aone mkoaa wake uko katika kifungu kipi na kusukuma juhudzi za kilimo kwa nguvu zaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mikoa kama Nyanda za Juu Kusini, upande wa Magharibi kule Kigoma wamefanya vizuri sana. Ni bahati mbaya tu kwamba sasa ukame kidogo

umejitokeza tokeza, lakini hali ya chakula tunaamini bado itakuwa nzuri. Kwa hiyo, hiyo ni moja ya matumaini ambayo tunayapata. Lakini kwa upande mwingine ni kuwaomba Watanzania katika mazingira haya kutumia chakula kwa uangalifu mkubwa. Tutajitahidi sana kujaribu kupeleka mbegu katika mvua zitakazofuata zitakazodumu kwa muda mfupi ili tuweze kujihakikishia kwamba tuna akiba ya kutosha ya chakula. Kwa hiyo, nadhani tumejipanga vizuri nafikiri tutakwenda vizuri. (*Makofi*)

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri unakumbuka kwamba katika suala langu hili niliulizia suala zima la nishati na unakumbuka kwamba katika Bunge hili tuliamua tutapitisha Sheria ya kwamba sasa tuweze kufanya ile *bulk purchases* ya mafuta. Sasa sina hakika kama Serikali imetekeleza hilo ili kuweza kupunguza tatizo hili la bei ya mafuta pale ambapo watu wataona kuna *shortage* ili waweze kuuza mafuta. Je, ununuaji wa mafuta wa jumla umefikia wapi mpaka sasa?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa swali lake hilo la nyongeza. Ni kweli tulifanya ule uamuza na Serikali ukauchukua, ukawasilishwa kwenye *Cabinet*, tukalizungumza, tukalikubali kwamba ni vizuri tuanze mfumo sasa wa ununuizi wa mafuta kwa kutumia mfumo huo. Lakini kulikuwa na taratibu ambazo ilibidi zikamilishwe ili uweze ku-*function* vizuri. Kwa hiyo, taratibu hizo mpaka tunakwenda kwenye uchaguzi ndiyo zilikuwa zinashughulikiwa ili zikamilike.

Mheshimiwa Spika, matumaini yangu ni kwamba kwa sasa inawezekana zimeshakamilika, lakini nita-*check*, lakini pili upande mwingine tulikuwa vilevile bado kama kawaida kigugumizi hasa kutoka kwa wafanyabiashara kujaribu kukutana nao, tumewaeleza faida zake. Lakini bado baadhi yao wanaona kama haitawanufaisha sana. Sasa naweza nikaelewa sababu, maana sielewi kwenye vyanzo wanavyopata, wanapata kwa namna gani. Lakini bado sisi kama Serikali msimamo wetu ni pale pale. Ni lazima tufike mahali tuyaaagize kwa pamoja ili tuweze kupata tija inayotakiwa. Kwa hiyo, nina hakika tutaifanyia kazi tukamilishe ili tuanze.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mwongozo wa Spika

SPIKA: Ninaongea mimi, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge tuna nafasi kubwa ya kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa umakini wa kuweza kujibu maswali mazito ambayo kwa kipindi kilichopita yalituletea wasiwasi na mashaka makubwa kabisa ndani ya nchi. Sasa tunashukuru sana kwa wale waliouliza maswali, tunashukuru sana na mwenyewe uliyejibu maswali kwa sababu angalau Watanzania sasa waelewe kiini na mambo yaliyofanyika. Lakini kikubwa Watanzania tutunze amani yetu. (*Makofi*)

Haya kuhusu utaratibu.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 68(7), naomba kupata ufanuzi kwamba Mbunge anaweza akachukua hatua gani kama anaona mtu mwenye nafasi kubwa katika nchi kama Waziri Mkuu analidanganya Taifa na kulidanganya Bunge. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, Bunge hili lazima liwe na adabu inayostahili. Kwa hiyo, kama tutafanya Bunge letu hili ikawa ni mahali, sasa unataka kusema Waziri Mkuu kwa ahadi aliyoweka ndani ya Bunge hili anadanganya? Kama anadanganya naomba ukaiandike vizuri kabisa kuhusu kudanganya kwake, halafu nitakuambia tufanye nini. (*Makofii*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 27

Ruzuku Ndogo kwa Halmashauri za Wilaya Nchini

MHE. JOHN P. LWANJI aliuliza:-

Halmashauri za Wilaya nyingi zinalalamikia ruzuku kidogo wanayopewa na Serikali ambayo inakwamisha kutatua kero za wananchi katika maeneo mbalimbali ya nchi:-

(a) Serikali inachukua hatua gani za dhati za kuziongezea Halmashauri za Wilaya ruzuku?

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kupima Halmashauri zote nchini kabla ya kutoa ruzuku?

(c) Je, Serikali haioni kwamba vigezo hivyo ndivyo chimbuko la kupunjwa kwa baadhi ya Halmashauri hizo na kwamba sasa virekebishwe?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ruzuku iliyotolewa kwenda kwenye Halmashauri kote nchini imeongezeka kutoka shilingi 200,174,297,222 mwaka 2008/2009 hadi shilingi 324,384,655,755 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia 62 kwa miaka mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ongezeko la asilimia hizi linaonesha kuwa Serikali imefanya jitahada za dhati katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Hata hivyo Halmashauri zinavyo vyanzo nya ndani ikiwa ni pamoja na kodi za majengo, kwa maana ya Miji, Manispaa na Majiji na kodi za ardhi ambavyo kwa takwimu za mapato kuanzia mwaka 2005/2006 hadi mwaka 2009/2010 zinaonyesha makusanyo ya mapato ya ndani hayazidi asilimia saba ya jumla ya mapato yote ya Halmashauri. Halmashahri zinatakiwa kuongeza uwezo wa kujitegemea kutohana na mapato ya ndani kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vilivyopo na kubuni vyanzo vipyta ya mapato ambavyo havileti kero kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala hili ni letu sote kwa upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) tumeanza kulifanyia kazi kwa kuziwezesha Halmashauri kushirikiana na Mamlaka ya Mapato yaani *TRA* kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam ili kuona namna ya kujijengea uwezo wa kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tukiwa ni sehemu ya Madiwani katika Halmashauri zetu kuimarisha mifumo ya ukusanyaji pamoja na kuweka makadirio halisi ya mapato badala ya kuweka makadirio hafifu ya mapato ambayo yanadhoofisha kasi ya kubuni mbinu za kuongeza mapato.

(b) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kupima Halmashauri zote nchini kabla ya ruzuku kutolewa hivi vifuatavyo:-

- (i) Usimamizi wa fedha na kuandaa taarifa kwa wakati.
- (ii) Kuandaa Mpango na Bajeti na kutoa taarifa ya utekelezaji.
- (iii) Kufanya maamuzi kwa kufuata Sheria.
- (iv) Utendaji wa Halmashauri kuzingatia vikao na kuandaa taarifa za vikao.
- (v) Halmashauri kutopata hati isiyoridhisha yaani chafu;
- (vi) Kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika ngazi zote;
- (vii) Mahusiano baina ya Halmashauri, Kata na Vijiji na Mitaa; na
- (viii) Maendeleo ya Watumishi kwa kuwepo kwa viongozi walioteuliwa rasmi katika Halmashauri.

(C) Mheshimiwa Spika, vigezo nilivyovitaja hapo juu vinatokana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ikiwemo Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba, vigezo hivyo vinachangia katika kupunja baadhi ya Halmashauri kwani kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa, inapaswa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Nchi. Vigezo hivi vimesaidia katika kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa Watendaji wa Halmashauri kwa nyanja mbalimbali hususan katika uandaaji wa taarifa za hesabu za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ina nafasi ya kukata rufaa pindi inapoona haikutendewa haki. Vilevile Halmashauri zinazokosa ruzuku ya maendeleo bado zina nafasi ya kupata ruzuku ya kujenga uwezo kwa asilimia 100 ili zirekebishe upungufu uliobainishwa na baadaye ziweze kupata asilimia 100 ya stahili yake ya ruzuku ya maendeleo.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa vigezo vilivyoainishwa vinahusu zaidi Watendaji wa Halmashauri husika; inapotokea kwamba wanashindwa kutimiza wajibu wao; je, Serikali haioni kwamba wananchi wa maeneo husika wanaadhibiwa bila sababu?

SPIKA: Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Waziri anasema hasikii, labda tuhame hiyo mashine tuje inayofuata. Leo kuna vurugu za mashine.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa vigezo vilivyoainishwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri vinaonesha kwamba vinahusu zaidi Watendaji wa Halmashauri husika; sasa wanaposhindwa kutimiza wajibu wao kama ilivyoainishwa; je, hauoni kwamba adhabu hii inayotolewa ya kunyimwa ruzuku au kutolipwa ruzuku kwa wakati inawaumiza zaidi wananchi kuliko kawaida?

(ii) Idadi ya watu na eneo husika la Halmashauri pamoja na kiwango cha umaskini huwa ni vigezo ambavyo ni muhimu katika kuainisha kiwango cha ruzuku kinachotolewa, lakini ninashangaa kuona kwamba vigezo hivi havikutajwa katika majibu; ni kwa sababu gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, mimi ninaelewa anachozungumza Mheshimiwa Lwanji; anachosema ni kwamba, pale unaye *DED* wa Halmashauri, kuna Afisa Mipango, kuna Afisa Biashara na kuna watumishi ambao wamewekwa pale na Halmashauri, sasa hawa watumishi kama imetokea kwamba hela zimetumika vibaya, wao ndiyo inatakiwa uwaadhibu. Kwa hiyo, huna haja tena ya kutoa adhabu hii ya kusema kwamba unaacha kuweka *Local Government Capital Development Grant* kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe takwimu hapa kuonesha jinsi ambavyo utaratibu huu umesaidia. Mwaka 2000 Halmashauri ambazo zilipata Hati Chafu ziliwa 75, leo tunapozungumza hapa Halmashauri ambayo ina Hati Chafu kutokana na huu mkakati imebaki moja tu. Halmashauri ambayo Mheshimiwa Lwanji anaizungumza hapa, mwaka 2004 ilikuwa na Hati Chafu. Kutoka pale mpaka sasa hivi tunapozungumza hapa, wamefanya kazi nzuri na wana Hati Safi. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba, utaratibu huu ambao umetumika hapa umesaidia sana katika kuhakikisha kwamba, hela za Halmashauri zinasimamiwa vizuri na ndiyo haya niliyoyaeleza hapa.

Mheshimiwa Spika, swal la pili anasema kwamba ni kwa nini Mheshimiwa hukutaja vile vigezo vingine? Mimi ninadhani labda nifafanue hapa; ninachozungumzia hapa kuna vigezo viwili; mimi nilichoeleza hapa kuna kitu kinachoitwa *assessment criteria*, yaani unaangalia unasema huyu anastahili kupata hela. Baada ya hapo, unakwenda kwenye kigezo cha pili ambacho kinaitwa *resource allocation criteria*; huyu ame-*qualify* sasa tunataka useme unafanyaje.

Hapo ndipo unapoanza kusema asilimia 70 itakwenda kwa ajili ya *population*, asilimia 20 itakwenda kwa ajili ya *poverty* na hivi vigezo vinatofautiana katika Idara mbalimbali. Kwa mfano, ukienda pale Afya, wana vigezo vyao wanaangalia *child mortality rate*, ukienda pale Maji kwa Mheshimiwa Profesa Mwandosya, ataangalia maeneo ambayo hayana maji na huko ndiko atakakopeleka pesa.

Mheshimiwa Spika, mimi sikuitaja hii ya pili kwa sababu hakuuliza hiyo, aliuliza kuhusu hii nyingine. Ninataka niseme kwamba, mimi nitaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Lwanji, kwa vigezo hivi vilivyozungumzwa hapa ili tuone kwamba Halmashauri yake inaendelea kufanya vizuri.

Na. 28

Suala la Mafuta Kuondolewa Kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO aliuliza:-

Suala la kuondoa mafuta kwenye orodha ya Mambo ya Muungano limeshafikishwa Serikalini ili litolewe maamuzi lakini hadi sasa haifahamiki ni maamuzi gani yamefikiwa:-

- (a) Je, ni sababu gani zilizochelewesha maamuzi juu ya jambo hili?
- (b) Kwa nini suala hilo lisipatiwe ufumbuzi wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kuwa suala hilo linazungumzika na lifanyiwe kazi?
- (c) Je, hadi sasa ni hatua gani imeshafikiwa juu ya suala hilo na kufanya libakie kuwa siri?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu swali namba 28, lililoulizwa na Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Mgogoni, kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, suala la Mafuta na Gesi Asilia ni mojawapo ya hoja zinazoshughulikiwa na Kamati ya Pamoja ya Kero ya Muungano kati ya SMZ na SMT. Kwa sasa hivi suala hili limeshawasilishwa katika ngazi ya juu ya uongozi. Tunamwomba Mheshimiwa Kombo pamoja na wananchi, wawe na subira hadi Viongozi wetu Wakuu watakapotoa maelekezo.
- (b) Mheshimiwa Spika, suala hili linazungumzika na kama alivyosema Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Maadhimisho ya Sherehe za Muungano mwaka 2009; tuna imani kwamba suala hili litapata ufumbuzi muafaka pale muda utakapowadia.
- (c) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, suala hili siyo siri; Serikali zetu zina nia thabiti ya kushughulikia masuala ya Muungano na ndiyo maana ziliajiri Mshauri Mwelekezi kushauri juu ya suala hili na taarifa ipo katika ngazi za juu kama nilivyosema kwa tafakari na kutoa maelekezo yanayofaa. Katika kulishughulikia suala hili ni lazima Serikali iangalie manufaa ya pande zote mbili za Muungano. Ahsante.

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge linaongozwa na Kanuni; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishatoa kauli juu ya suala hili; je, Serikali haioni kwamba inakwenda kinyume na Kanuni ya 64(1)(d) baada ya kutolitumia jina la Rais kwa dhihaka lakini ikawa inaendelea kuifanyia dhihaka kauli ya Mheshimiwa Rais na kwamba inakwenda kinyume na Ibara ya 64(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoipa mamlaka Zanzibar kujiamulia mambo yanayohusiana na Zanzibar? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la Pili: Ikiwa hili limeshindikana kutolewa maamuzi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano; je, Wazanzibari watajihisi wamedharauliwa kwa kiasi gani na Serikali yao ya Jamhuri ya Muungano; na je, ni lini sasa hicho kilichopelekwa ngazi ya juu kutolewa maamuzi kitatolewa maamuzi ili maamuzi hayo yaweze kuwaridhisha Wazanzibari?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Kuhusu utaratibu?

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, baadhi ya waulizaji wa maswali nimeona kama wawili hivi na huyu aliyemaliza sasa hivi wanauliza maswali ya nyongeza kwa kusoma kitu ambacho ni kinyume na Kanuni yetu ya 45.

SPIKA: Ahsante. Nakubaliana na yeye. Waheshimiwa Wabunge, hampaswi kusoma hotuba wala maswali yenu.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, jibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimhakikishie kwamba, majibu yangu hapa na kutaja jina la Rais, siyo suala la dhihaka lakini Serikali imefanya kazi na imekamilisha kazi hiyo na imeikabidhi kwa uongozi wa juu wa nchi. Vilevile ni kweli kwamba, Mheshimiwa Rais, alisema kwamba suala hili linazungumzika; kwa hiyo siyo dhihaka.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Wazanzibari au maamuzi ya Zanzibar, yamo katika kazi iliyofanywa na Kamati na maamuzi yao pia yamo katika *package* ambayo imepekwaa uongozi wa juu kwa maamuzi. Kuhusu ni lini suala hili litatolewa maamuzi; sitaweza kujibu hapa kwa sababu tunasubiri mwongozo wa Kiongozi Mkuu wa Nchi.

Kwa hiyo, atakapopata nafasi atatupa maelekezo na Bunge lako litajulishwa rasmi.
(*Makofii*)

Na. 29

Kero za Muungano

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED aliuliza:-

Moja kati ya majukumu ya kuimarisha Muungano ni pamoja na kuhakikisha kuwa kero zote zinatatuliwa:-

Licha ya vikao vingi vilivyokaa kujadili kero hizo; je ni kero ngapi na zipi ambazo hadi sasa zimekwishapatiwa ufumbuzi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba kujibu swali namba 29 lililoulizwa na Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya hoja 13 zilizoibuliwa kama kero za Muungano, hoja sita zilijadiliwa na kupata ufumbuzi na kuondoshwa katika idadi ya kero za Muungano. Kati ya hizo, hoja mbili ziliandaliwa Hati za Makubaliano ambazo zilisainiwa na Mawaziri wa Serikali ya SMZ na SMT tarehe 2 Juni, 2010 huko Zanzibar. Hoja hizo ni Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu, ambapo Tume hii ilitakiwa ifanye kazi Zanzibar na tayari imesharuhusiwa. Hoja nyiningine ni ile ya utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na uwezo wa Zanzibar kujiunga na *International Maritime Organization (IMO)*, ambayo tayari Zanzibar wameshajunga.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine zilizotolewa maamuzi ni kuhusu malalamiko ya Wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili na ilikubalika kwamba, bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha kupitia kituo chochote rasmi cha forodha zitahesabika kuwa zimeingizwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, utekelezaji wa suala hili bado una utata. Katika kulishughulikia, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania, imeahidi kuchukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaotumia vibaya fursa za ukadiriaji wa thamani ya kodi za bidhaa zinazoingizwa kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hoja nyiningine ambayo imepatiwa ufumbuzi ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nje, ambapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapata 4.5% ya misaada ya kibajeti. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanza kunufaika na 4.5% ya mikopo ya kibajeti katika *General Budget Support (GBS-C)*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lililopatiwa ufumbuzi ni misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF* na *MDRI*. Suala hili limepatiwa ufumbuzi kwani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilishapata fedha za misamaha hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi; ilikubalika kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa ndani ya nchi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaweza kukopa nje ya nchi chini ya udhamini wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja saba zilizobakia bado zinafanyiwa kazi.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimwia Waziri kwa kujibu swali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa vimefanyika vikao sita na kuendelea na vikao vya Mawaziri, vya pamoja ili kero hizi za Muungano zitatuliwe lakini bado inaonesha kwamba Wizara au Wafanyakishara wa Zanzibar, pamoja na Mamlaka ya Mapato bado kero hii haijatatuliwa: Je, kuna tatizo gani baina ya Wizara yako na Mamlaka ya Mapato kuwa mpaka leo hawajataka kutatua tatizo hili; na ukiangalia jibu lako la msingi utaona kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania itachukua hatua za kinidhamu kwa watendaji wanaotumia vibaya fursa ya ukadiriaji wa thamani ya bidhaa?

SPIKA: Maswali yawe mafupi, utamchanganya na anayetaka kujibu. Haya endelea.

MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante.

(ii) Ikiwa kero hii bado inaendelea; utawasaidiaje wafanyakishara hawa hasa ukizingatia kwamba wafanyakishara hawa wataweza kutafuta njia mbadala ili Serikali ikose mapato yake?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongenza la Mheshimiwa Thuwayba Idrisa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo gani kwa *TRA* kumaliza suala hili? Kuna utata wa kifungu kimoja cha sheria ambacho kinasema kwamba, mkadiriaji anaweza akatumia thamani ya juu ya bidhaa ile au thamani ya chini ya bidhaa ile. Kinachotokea ni kwamba, wakadiriaji wanatumia thamani ya chini ya bidhaa zinazopitishwa na ule ni uwezo wao ambao wamepewa kisheria. Bidhaa zinapovuka kuja Bandari ya Dar es Salaam, Maafisa wa *TRA* wanatumia kifungu kile kile cha sheria kwa kutumia thamani ya juu ya bidhaa zile. Kwa hiyo, Maafisa wote wawili wanakuwa wako sawa kisheria. Tunachozungumza ni mazungumzo yanayoendelea kuhakikisha kwamba *TRA* inatoa *decision* moja, kwa sababu ni *TRA* ile ile kwa Zanzibar na ni *TRA* ile ile kwa Tanzania Bara. Kwa hiyo, wakubaliane watoe *decision* moja na waache kuwayumbisha wafanyakishara.

Mheshimiwa Spika, je, nitawasaidiaje wafanyabiashara kumaliza utata huu?

Mheshimiwa Spika, mazungumzo yanaendelea na mimi kama Waziri wa Muungano, nitalisimamia hilo kuhakikisha linatimia. (*Makofit*)

Na. 30

Kuimarisha Idara ya Hali ya Hewa

MHE. MKIWA A. KIMWANGA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa na tatizo la kushindwa kutabiri majanga mbalimbali kama vile ukame, mafuriko na kadhalika hali inayosababisha nchi kukumbwa na uharibifu mkubwa wa miundombinu, uhaba wa chakula na kuathirika kwa uchumi wa nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiimarisha Idara ya Hali ya Hewa kwa kuipatia wataalam waliobobea na vifaa vyta kisasa ili kuweza kutoa utabiri wa hali ya hewa kwa uhakika zaidi?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 1999, iliyokuwa Idara ya Hali ya Hewa nchini chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ilibadilishwa na kuwa Wakala wa Hali ya Hewa kwa Sheria ya Wakala za Serikali ya Mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba, Mamlaka inakuwa na vifaa vyta kisasa vyta kutosha, serikali imeanzisha Programu ya Kutandaza Mtandao wa Vituo vyta Rada zinazofikia saba hapa nchini, ambazo zitaiwezesha kutoa utabiri kwa uhakika zaidi. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, Serikali ilinunua rada moja na kuisimika eneo la Pugu, Dar es Salaam. Mchakato wa ununuzi wa rada ya pili ambayo itasimikwa Mkoani Mwanza, ungali unaendelea. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa, imeendelea kuongeza vituo vyta kuchunguza hali ya hewa, ambapo katika mwaka 2010/2011, kituo kikubwa cha hali ya hewa kitajengwa Mpanda Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Spika, ili Mamlaka kupata wataalamu waliobobea, Serikali imeendelea kujenga uwezo katika kutoa utabiri wa hali ya hewa na tahadhari kwa uhakika zaidi. Mpango wa Serikali ni pamoja na:-

- (a) Kusomesha wafanyakazi wa fani ya hali ya hewa katika ngazi mbalimbali kama vile shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu, ndani na nje ya nchi.
- (b) Kuimarisha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, kinachotoa elimu ya kati katika fani ya hali ya hewa kwa kukiongezea fedha na kuboresha miundombinu.
- (c) Kuweka mazingira ya maridhiano na Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*), ambao wameendelea kuisaidia Mamlaka kwa kuipatia vifaa mbalimbali vikiwemo vituo vinavyoijendesha vyenyewe (*Automatic Weather Stations*), pamoja na *computer* kubwa ya uchambuzi wa mifumo ya utabiri pia kuongeza uelewa wa tabia ya nchi.
- (d) Mazungumzo yanafanyika kati ya Mamlaka na Vyuo Vikuu vya Sokoine (SUA) na Dar es Salaam UCLASS, kuanzisha kozi ya stashahda ya juu, *postgraduate diploma* ya sayansi ya utabiri wa hali ya hewa kwa wale wanafunzi wenye shahada za kwanza, yaani ni *bachelor of science* katika fizikia na hisabati.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa nchi inahitaji rada saba ili kuweza kukidhi mahitaji yake na Serikali imenunua rada moja tena kwa kusuasua kwa muda mrefu sana kulingana na hali ya hewa ya uhakika; je, Serikali haionti kwamba ni muhimu suala hili kulifanya la dharura kuliko kulipeleka kwenye mchakato ambao huwa tunachakata bila kujua ukomo wake na kutokupata jibu la uhakika kwa wakati muafaka?

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, wanataka kukiimarisha Chuo cha Hali ya hewa Kigoma; kwa kuwa Chuo hiki kiko katika hali mbaya sana; na kwa kuwa kwa mara zote Serikali husema wataongeza pesa katika Chuo hiki lakini hakuna pesa inayoongezwa na kuna majengo ambayo yamejengwa kwa muda mrefu sana hayajaisha wanafunzi wanaishi kwa shida na kusoma kwa matatizo kwa kupokezana madarasa; je, Serikali inasema nini sasa kukiongezea Chuo hicho pesa ya uhakika ili kiweze kwisha na wanafunzi wasome kwa utaratibu unaostahiki?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kimwanga. Suala la rada kuwa moja na zinahitajika saba ni suala kibajeti, tutaendelea kuiomba Serikali rada ziongezeke lakini tunachofanya pia tunaongeza mazungumzo na wafadhili ili rada ziongezeke na sasa hivi mazungumzo haya yako katika hatua nzuri.

Kuhusu Chuo chetu cha Hali ya Hewa kuwa na majengo chakavu na kwamba pesa ziongozeke, hilo suala tunalifahamu na tunalifanyia kazi ili mazingira mazuri ya wanafunzi kusoma yaweze kupatikana. Tuelewe suala la bajeti na mahitaji mengi katika Wizara mbalimbali yanafahamika, kwa hiyo, tunaomba uvumilivu tuendelee katika hali hiyo tutarekebisha kufuatana na uwezo wa Serikali.

Na. 31

Mgogoro Kati ya Wanakijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA aliuliza:-

Kumekuwepo na mgogoro kati ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na Wananchi wa Vijiji vya Nansimo, Nambaza, Bunene, Busambara, Nakutaba, Bulendabufwe, Igundi na Kigaga ambavyo vinauzunguka Mlima Kurwirwi unaodaiwa kuwa ni hifadhi ya msitu; baadhi ya Wananchi wa Kijiji cha Nansimo, Kitongoji cha Kamcheche wamewahi kushtakiwa mahakamani kwa madai ya kuishi kwenye mlima huo unaodaiwa kuwa hifadhi ya msitu:-

- (e) Je, ni kweli mlima huo ni hifadhi ya msitu kisheria na kama ni kweli je, ni sheria gani?
- (f) Je, hifadhi ina eneo lenye ukubwa kiasi gani linalotambulisha mipaka yake?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli msitu huo wa Mlima Kurwirwi umehifadhiwa kisheria na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kama ilivyotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 39 la tarehe 1 Februari, 1957 na unalindwa kwa Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002, vifungu namba 23 na 25. Hifadhi hii ilipotangazwa ilikuwa chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe na Mkoa wa Ziwa Magharibi kwa wakati huo na sasa uko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, msitu huu wenyе ukubwa wa hekta 1,580, kwa ramani JB Na. 311 ni chanzo kikuu cha maji ya mbubujiko kwa vijiji vinavyozunguka eneo hili ambavyo ni Nansimo, Mwitende, Nambaza, Idungu, Bulendabufwe na Malama na Katuba na Malebe na Bumele. Kwa hiyo ni vizuri ukaendelea kutunzwa kwa ajili ya usalama na maendeleo ya wananchi wa eneo hilo.

MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa mipaka ya hifadhi hii inafahamika; na kwa kuwa Serikal iliwashtaki akina John Maige na wenzake sita, Kesi Na. 4 ya Mwaka 2009 katika Mahakama ya Mwanzo ya Nansimo kwamba wako ndani ya hifadhi; na kwa kuwa Mahakama ya Mwanzo iliwatia hatiani na kuwatoza faini ya shilingi 50,000 lakini wakakata rufaa Mahakama ya Wilaya wakashinda; je, ni lini Serikali itarudisha fedha hizo pamoja na riba?

(ii) Kwa kuwa wananchi walizuiwa kulima mashamba yao ambayo kumbe ni halali yao; wakaishi kwa mateso na kukosa riziki; je, Serikali haioni inao wajibu wa kuwalipa kifuta jasho wananchi hawa ambao waliishi kwa mateso takriban miaka miwili?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Lugola, Mbunge wa Bunda, kwa maelezo yake ambayo ni kweli kwamba, kulikuwepo mgogoro kwenye eneo hilo na Kesi hiyo Na. 4 ya Mwaka 2006 ilifunguliwa na watuhumiwa wakawa wamehukumiwa. Baada ya kuwa wamekata rufaa na rufaa hiyo ikawa imeotolewa uamuzi, sisi kama Wizara tulikwishawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, kuwaeleza kwamba sasa wanahitaji warejeshe hizo fedha kwa mujibu wa hukumu.

Taratibu za kurejesha fedha hizo zinaendelea na zinasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya. Kama nilivyosema, msitu huu ni wa Halmashauri, kwa hiyo, sisi tuna mamlaka ya kisheria ya kuwaelekeza ni nini cha kufanya.

La pili, kuhusu usumbufu na mambo mengine, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hili kwa kweli linazungumzika lakini kubwa ni kwamba ile mipaka haiko bayana sana, kuna maeneo ambayo mipaka ile imeshafifia, iliwekwa miaka mingi iliyopita, mwaka 1958 baada ya kuwa imetangazwa mwaka 1957. Kwa hiyo, maeneo mengi mipaka imefifia sana, sasa hivi wanafanya jitihada Halmashauri ya Wilaya kuweza kuirejesha ionekane waziwazi.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tuzungumze na mimi pamoja na Halmashauri ya Wilaya Bunda, tuone namna gani tunaweza tukaondoa kero hiyo ya wananchi hao saba ambao walikuwa pembezoni mwa hifadhi.

Na. 32

**Mgogoro wa Mpaka Kati ya Hifadhi ya TANAPA
na Wananchi Mbarali**

MHE. MODESTUS D. KILUFI aliuliza:-

Ushirikiano baina ya Hifadhi za Taifa na wananchi wa maeneo yaliyo jirani na hifadhi hizo ni jambo jema pale inapokuwa hakuna migogoro yoyote kati ya hifadhi hizo na wananchi walio jirani:-

Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Wananchi wa Jimbo la Mbarali kupitia Mbunge wao katika kutafuta suluhisho la mgogoro uliopo kati ya TANAPA na wananchi jirani na hifadhi hiyo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kujibu swalii la rafiki yangu, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii naomba kutoa maelezo mafupi kidogo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 14 Machi, 2008, Serikali ilitoa Tangazo la Serikali Na. 28 la kupanua Hifadhi ya Ruaha kwa kujumuisha Bonde la Usangu ili kulinda mazingira na vyanzo vya maji. Sababu ya kutoa Tangazo hilo, inatokana na uharibufu wa mazingira uliosababishwa na uvamizi wa wafugaji na shughuli za kilimo, jambo ambalo liliathiri kwa kiasi kikubwa, mazingira na vyanzo vya maji katika maeneo hayo. Hivyo, Serikali ililazimika kuwaandoa wafugaji na wakulima waliokuwa wamevamia maeneo hayo kwa lengo la kunusuru mazingira na mabonde hayo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wananchi wa maeneo hayo wameendelea kulalamika hasa baada ya kupitisha mpaka wa upanuzi wa hifadhi na kuonekana kuathiriwa na mipaka iliyoweka, hali iliyopelekea kuibuka kwa migogoro ya mara kwa mara baina ya wananchi na Uongozi wa Shirika la Hifadhi za Taifa, ambapo wananchi wameendelea kупinga fidia waliyolipwa wakati wa kuhamishwa. Hali hii imesababishwa kuwepo kwa mgogoro, hali ambayo ilipelekea Wizara yangu kuunda kikosi kazi kwa lengo la kukagua sehemu ya Shamba la Madibira, ambalo liko ndani ya hifadhi na kuona hali halisi ya vijiji/vitongoji vilivyo ndani ya hifadhi. Kikosi kazi kimekasilisha kazi yake na mapendekezo yamefikishwa ofisini kwangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa nijibu swalii la Mheshimiwa Kilufi, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Migogoro iliyobuka inavihu Vijiji vya Ikanutwa, Kitongoji cha Tagawano na Vikae, Kitongoji cha Kapunga, ambapo wananchi hawa wanapinga viwango vya fidia walivolipwa. Vijiji hivi viliteua wawakilishi amba wamefungua kesi mbili tofauti kwenye Mahakama ya Ardhi Mbeya - Kesi Na. 9/2008 ya Kijiji cha Ikanutwa na Kesi Na. 1/2009 ya Kijiji cha Vikae.

Sambamba na hali hiyo, mgogoro mwengine ni ule unaowahuwanu wananchi wa Vijiji vya Ikanutwa, Iwalanje, Vikae, Igunga na Igava, amba wanalamikia mpaka mpya kuwaingiza katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kufuatia malalamiko hayo,

wamefungua kesi Mahakama Kuu - Dar es Salaam, Namba CC 43/2008, kupinga kuingizwa kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa migogoro hii imefikishwa Mahakamani na kufunguliwa mashauri, Wizara yangu haina budi kusubiri uamuzi wa Mahakama. Hata hivyo, tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge kutatua migogoro huo nje ya Mahakama kama itaamuliwa kufanya hivyo.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa vile Mahakama imeshatoa nafasi ya kushughulikia mgogoro huu nje ya mahakama kati ya mwezi Februari hadi mwezi Aprili tarehe 12; je, Waziri yuko tayari au Serikali iko tayari kuona kwamba mgogoro huu sasa unashughulikiwa ndani ya kipindi maalum ambacho tumepewa na Mahakama?

Suala lingine linalofuata ni juu ya wananchi wale wanaodai fidia kwamba hawakuridhika; Mheshimiwa Waziri ametaja maeneo ya Ikanutwa, Tagawano, Vikae, lakini amesahau Kata ya Msangaji, wananchi hawa waliomba kuongezwa malipo ya fidia kwa sababu viwango vilivyotumika kuwalipa wakati ule vilikuwa ni vidogo haviendi na wakati: Je, sasa Serikali iko tayari kama hao wananchi wataitoa kesi Mahakamani kuwalipa fidia ambayo itaendana na wakati?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali ni ya wananchi na hakika sidhani kama kuna mtu ye yeyote ambaye anapenda Serikali iwe inapelekwa mahakamani na watu wake. Nimefurahi sana kusikia kwamba, tayari Mahakama imeshatoa nafasi hiyo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, habari hizo sisi kama Wizara tunazipokea kwa furaha na tuko tayari kabisa kuzungumza na Wananchi wa Mbarali pamoja na Mheshimiwa Mbunge, kuona namna gani tuweze kutatua tatizo hili. Kwa hiyo, hilo la kwanza nimhakikishie kwamba kwa hakika tuko tayari.

Suala la pili linahusiana na la kwanza yote yale yanazungumzia mipaka; kuna kesi inayohusu mipaka na kuna kesi inayohusu fidia. Kwa hiyo, katika mazungumzo yale tutayazungumzia masuala yote mawili na ninaamini kwamba, tunaweza kufikia mahali pazuri.

MWONGOZO WA SPIKA

SPIKA: Kuhusu mwongozo.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), ninataka tu mwongozo wako, lakini Kanuni inayokwenda sambamba na hiyo ni ile ya 64(g) kwamba, Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Wakati Mheshimiwa Godbless Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, akiomba mwongozo wako juu ya jibu la Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa swali alilouliza, ametumia lugha kwamba, kama mtu amesema uwongo au ni mwongo; lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Kiongozi Mkubwa sana katika nchi hii; na kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni; ofisi yako ni kubwa na kwa hiyo kwa mila na desturi za Kitanzania, kumwambia mtu anayekuzidi umri, mbali ya nafasi aliyonayo kwamba ni mwongo; ni kinyume cha mila na desturi zetu. (*Makofi*)

Katika jibu la Mheshimiwa Waziri alivyokuwa akijibu lile swali alisema, jambo hili liko Mahakamani. Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako juu ya jambo hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge huyu alisema zamani, sasa niko kwenye maswali, ukianza tena kuomba mwongozo wakati hiyo ungeileta kwa utaratibu mwingine kabisa kwamba, tulipokuwa tunajadili suala fulani kuna Mbunge alifanya hivi. Sasa hapa tupo mbali kabisa, mwongozo ultakiwa uwe katika swali hili tunalojibu. Kwa hiyo, inawezekana ulikuwa sahihi lakini ulichelewa wakati ule. (*Makofi*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, mwongozo.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, naomba tumalize kwanza kazi hii kwa sababu tuko kwenye maswali mengine. (*Makofi*)

Na. 33

Ujenzi wa Kituo cha Polisi Chenye Hadhi ya Wilaya

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI aliuliza:-

Wilaya ya Manyoni haina Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya; kutokana na hali hiyo Wananchi wa Manyoni kwa kushirikiana na Mbunge wao wamenunua mashine tatu za kufyatua tofali za kushikamana na kazi imeanza kufyatua matofali ya ujenzi wa Kituo cha Polisi chenye hadhi ya kiwilaya:-

Je, Serikali itakuwa tayari kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kutenga fedha katika bajeti yake ijayo kwa ajili ya Mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali hili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi anazozifanya, kusimamia maendeleo kwa kushirikana na Wananchi wa Jimbo lake. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu iko tayari kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kutenga fedha na kuhakikisha kwamba,

tunajenga kituo cha polisi chenye hadhi ya wilaya. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Serikali imetenga jumla ya shilingi 472 milioni kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho. Hata hivyo, fedha hizo bado hazijatolewa na Hazina. Tunaendelea kuhimiza fedha hizo zitolewe kwa ajili ya kutekeleza azma hiyo.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ya kutia moyo; hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa hela zilizotengwa kwa ajili ya Mradi huu shilingi milioni 472 hazijafika Manyoni na karibu mwaka wa fedha unakwisha; je, Wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha watatoa lini fedha hizi ili Mradi huu uanze kutekelezwa?

(ii) Kwa kuwa askari polisi pale Manyoni wanapata tabu kubwa ya nyumba; je Mradi huu unaweza ukaunganishwa na Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Askari pamoja na vifaa vidogo vidogo vya kufanya kazi kama *radio call* kwa vituo vya mbali kama Makanda, Kitinku, Chikuyu na Henka? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu katika swalı langu la msingi, hizo fedha zimekwishatengwa na ziko Hazina. Tunazungumza na Hazina tupate fedha hizo katika kipindi cha mwaka huu uliosalia; ni matumaini yangu kwamba, tutazipata hizo fedha kwa sababu na sisi kama Wizara, tuna shauku kubwa kuona kwamba, kituo hiki kinakamilika kwa kuzingatia kwamba, Mheshimiwa Mbunge amekuwa anafuatilia suala hili kwa muda mrefu sana.

Kuhusu suala lake la pili, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ambaye ye ye mwenyewe aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na siyo siku nyingi sana kwamba, anajua vema kabisa kwamba, tunapojenga Kituo cha Polisi cha Wilaya kuna masharti yake na mionganoni mwa masharti hayo ni kuhakikisha kwamba, zinakuwepo nyumba na vinakuwepo vifaa ambavyo vinaendana na hadhi ya kituo kuwa Kituo cha Wilaya. Kwa hiyo, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hilo tunalizingatia.

Na. 34

Posho za Askari Polisi Wanaohamishwa Vituo

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Kwa kawaida Askari Polisi wanapohamishwa sehemu moja kwenda nyingine hupewa posho za uhamisho:-

- (a) Je, ni askari wangapi waliohamishwa katika kipindi cha mwaka 2008 - 2010?
- (b) Je, ni wangapi hadi sasa wameshalipwa posho za uhamisho?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swal la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jumla ya askari 3,879 wamehamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine katika kipindi cha 2008 - 2010 kama ifuatavyo: 2008 walihamishwa askari 636; 2009 walihamishwa askari 1,974; na 2010 walihamishwa askari 1,269.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 31 Desemba, 2010 jumla ya askari 1,552 walishalipwa posho zao za uhamisho. Hii ni sawa asilimia 40 ya askari wote waliohamishwa kwa kipindi hicho. Ninapenda kulitaarifu Bunge lako kwa kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Siku ya Jumanne wiki iliyopita, Wizara ilipokea shilingi bilioni 3.5 kutoka Hazina kwa lengo hilohilo la kulipa posho za askari polisi.

Waziri wa Fedha ameahidi madeni yote yatalipwa kabla ya mwezi Juni, yaani katika mwaka huu wa fedha wa 2010/2011.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumwuliza swal moja la nyongeza:-

Kwa kuwa ulipaji huu unakwenda taratibu; Serikali haioni iko haja ya kubadilisha Sheria ili kuwawezesha Askari hawa kupata posho zao kwa wakati?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Haji Kai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nakiri siku zote kwamba, ulipaji wa posho umekuwa unakwenda taratibu. Ninaomba nimhakikishie kwamba, hakuna haja ya kubadili Sheria kwa sababu si suala la kisheria, ni suala la ugumu wa upatikanaji wa fedha kwa kulingana na bajeti ambayo tunakuwa nayo na mgawanyo huo katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunayo machungu kabisa kuhusu posho za Askari na madeni waliyonayo katika Wizara au katika Serikali na hili linafanyiwa kazi na ndiyo maana nimejibu kwa kusema kwamba, ifikapo mwezi Juni kwa uhakika ambao tumeupata kutoka kwa Waziri wa Fedha, madeni yote yatakuwa yamekwisha na hapo tutakapoanza tukijaliwa mwaka wa fedha unaokuja, nafikiri tutakwenda kwa utaratibu mzuri wa kulipa kwa wakati.

Na. 35

**Baadhi ya Waathirika wa Ukimwi Huambukiza
Wengine kwa Makusudi**

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Baadhi ya watu wanaojulikana kuwa tayari wameathirika na Ugonjwa wa UKIMWI wamekuwa wakisambaza Ugonjwa huo kwa makusudi kwa wengine:-

Je, Sheria zetu zinasema nini kuhusu hali hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, Bunge la Jamhuri ya Muungano, lilitunga Sheria mahususi kwa ajili ya kudhibiti UKIMWI na katika kifungu cha 47 cha sheria hiyo inayojulikana kama Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI (The HIV and AIDS Prevention Act, 2008), Sura ya 431, inatamka bayana kwamba, kitendo cha mtu yeyote kusambaza Virusi vya UKIMWI kwa makusudi ni kosa la jinai. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, mtu wa aina hiyo, adhabu yake huwa ni kutumikia kifungo kisichopungua miaka mitano au kisichozidi miaka kumi jela.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Kifungu cha 179 cha Kanuni ya Adhabu (*Penal Code*), Sura ya 16, kinaeleza kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote ambaye bila uhalali au kwa uzembe, anafanya kitendo chochote ambacho anajua au anaamini kitasababisha kuenea kwa ugonjwa wowote wa hatari kwa binadamu. Adhabu iliyoainishwa katika sheria hiyo ni kifungo kisichopungua miaka miwili au faini au vyote kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi wenye taarifa za watu wanaoeneza Virusi vya UKIMWI kwa makusudi, watoe taarifa Polisi ili watu hao washughulikiwe kwa mujibu wa sheria. Aidha, ninaomba kutumia nafasi hii kuwaasa watu wa aina hiyo kuacha tabia hiyo ambayo ni kosa la jinai.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri. Kwa kuwa vitendo hivi vya uambukizi wa makusudi vinafanyika katika maeneo yenye unyanyasaji mkubwa wa wanawake na watoto; na kwa kuwa vituo vingi vya polisi havina maeneo ya siri ya kuwashawishi wanawake kutoa ripoti hizo:-

(i) Je, Wizara yako haiko tayari kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuweka maeneo maalum ili Wanawake kuripoti kesi hizo?

(ii) Je, mpaka sasa ni watu wangapi wameshabanwa na sheria hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Kwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kwa sasa Vituo vya Polisi hasa vya Dar es Salaam, vina Dawati Maalum la Kusikiliza Unyanyasaji wa Wanawake. Kwa hiyo, Wanawake wanaweza kwenda kwenye Vituo vya Polisi ambavyo viko Dar es Salaam kwa ujumla, hatujakwenda katika Wilaya na nia yetu ni kwenda katika kila Wilaya. Kwa hiyo, Wizara ya Mambo ya Ndani imeshalifanya hilo na wengi wanakwenda kusikilizwa matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tangu Sheria hii ianzishwe mwaka 2008 mpaka hivi sasa hakuna kesi yoyote ambayo imeshafikishwa mahakamani. Kesi moja tu ambayo imeripotiwa katika Mkoa wa Kilimanjaro katika Mahakama ya Moshi ya suala la kuambukizwa UKIMWI kwa makusudi, lakini baadae yule mlalamikaji aliitua kesi hiyo Mahakamani na wakaenda kuelewana nje ya Mahakama.

Na. 36

Huduma za Afya Bure kwa Makundi Maalumu

MHE. REGIA ESTELATUS MTEMA aliuliza:-

Inafahamika wazi huduma za afya zinatolewa bure kwa akina mama wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wazee na wenye ulemavu, lakini zipo wilaya ambazo mpaka sasa wanawauzia wajawazito kadi zao kati ya shilingi 500 na shilingi 1000, kadi ambazo hazipaswi kuuzwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia jambo hili na kuhakikisha kuwa wajawazito hawatozwi gharama za kadi?

(b) Je, ni lini Serikali itatekeleza maamuzi yake ya kutoa huduma za afya bure kwa makundi yaliyoainishwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijbu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa Mwongozo Maalum utakaotumwa kwa waratibu wa afya ya uzazi na mtoto wa mikoa na wilaya ili kuwataka kuhakikisha kuwa viongozi wa vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo yao wanazingatia utaratibu wa kuagiza kadi za wajawazito kiwango cha kutosha kutoka MSD; na kwamba kila kituo cha kutolea huduma za afya kinakuwa na kadi hizo muda wote. Aidha, katika mazingira ambapo imeshindikana kabisa kupata kadi za wajawazito kutoka MSD, wajawazito waruhusiwe kutumia madaftari ya kawaida na baada ya kupatikana kwa kadi, taarifa zao zihamishiwe kwenye kadi husika.

Pamoja na hatua hiyo, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, niwaombe Viongozi wa Halmashauri wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na Watendaji, waendelee kuwafahamisha wananchi juu ya haki zao za matibabu hususan kwa makundi maalum yaliyopewa msamaha wa kuchangia huduma za afya wakiwemo wajawazito na kwamba hawatakiwi kulipa kwa huduma yoyote wanayoipata katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa au kupewa ruzuku na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaanza na inaendelea kutekeleza maamuzi yake ya kutoa huduma za afya bure kwa makundi maalumu kama yalivyoainishwa kwenye Sera ya Afya ya Mwaka ya 2007 kwamba, makundi maalum wapate huduma za afya bure. Aidha, kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri zao, waendelee kuwakumbusha watoa huduma kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Afya na Miongozo iliyopo ili kutoa huduma za afya zinazostahili kwa makundi maalum.

Wizara kwa upande mwingine itaendelea kutoa elimu zaidi juu ya huduma za afya na msamaha wa malipo na kuwahamasisha zaidi juu ya kutoa taarifa kuhusiana na vitendo vyovyote vinavyoikiuka taratibu za utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi maalum bila kulipa.

MHE. REGIA ESTELATUS MTEMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa, lakini pamoja na majibu hayo mazuri ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Inafahamika kwamba Wilaya ya Kilombero tuna matatizo makubwa ya huduma za afya kwenye Zahanati za Kata. Wananchi wanakwenda kupata huduma kwenye Zahanati hizi lakini hakuna dawa za kutosha, Wataalam pia hawapo wa kutosha: Je, Serikali imejiandaa vipi kuhakikisha inaboresha huduma ya Zahanati kwenye Wilaya ya Kilombero?

(ii) Vilevile Wilaya ya Kilombero wananchi wanapata matatizo makubwa ya kuchangia *ambulance* ili kufika vituo vya afya kati ya shilingi 40,000 hadi shilingi

120,000 lakini tunatambua wananchi wengi wa kule ni maskini wanashindwa kufikia kiwango hiki kikubwa. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na suala hili hasa kwa hawa wananchi maskini ambao wanashindwa kutoa shilingi 120,000 ili kuweza kulipia *ambulance* wafkishwe kwenye hospitali?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Regia Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, swal la kwanza anazungumzia juu ya ukosekanaji wa dawa au kutokuwepo kwa dawa za kutosha katika Zahanati na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa dawa katika Zahanati na Vituo vya Afya unategemea jinsi ambavyo wahuksika wanavyotoa takwimu za maradhi hasa yale ambayo yapo kwa kawaida siku zote. Kwa hiyo, uagizaji wa dawa muhimu umekuwa na matatizo. Ili kutatua hilo, Wizara imeelekeza MSD, MSD sasa watakuwa na vituo katika Wilaya na watakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba, wanasambaza dawa katika Vituo vya Afya na Zahanati kutoka katika maeneo husika. Watakuwa na vituo katika Mkoa na katika Wilaya, watakuwa wanasambaza dawa kuzipeleka kwenye Zahanati na kwenye Vituo vya Afya kufuatana na jinsi ambavyo wanaagiza zile dawa, lakini kwa sasa hivi kutakuwa na ufuutiliaji wa karibu hivyo dawa zitakuwepo.

(ii) Mheshimiwa Spika, kuhusu swal la pili, Mheshimiwa Mbunge anazungumzia juu ya uchangiaji wa mafuta kwa ajili ya *ambulance*.

Mimi ninaamini kwamba, huo mchango unatolewa kwa ajili ya mafuta. Sasa kutokana na tatizo hili, ndiyo sababu Wizara ya Afya iliona kwamba, tuchukue mfano wa wenzetu wa Afrika Kusini, Malawi, Ghana pamoja na Uganda wa kuagiza pikipiki ambazo zimetengenezwa *special* kwa ajili ya kuwa *ambulance*. Pikipiki hizi siyo Bajaji. Naomba nirudie tena, hizi pikipiki zimetengenezwa kuwa *ambulance*, zitatumia mafuta kidogo na tutakuwa na uwezekano wa kuhakikisha kwamba, kwenye vituo vya afya kunakuwa na pikipiki ambazo ni *ambulance* za kubeba wagonjwa kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, zinakuja pikipiki 400 na kwa njia hii tunatatua tatizo hili.

SPIKA: Ahsante. Maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Waheshimiwa Wabunge, mtaona nimewa-*rush rush* sana kwa sababu toka tumeanza kila siku tuna kiporo cha maswali na maswali mliyouliza kule ni mengi na ratiba ya kujibu tumekwishatoa, sasa nikiacha kumaliza maana yake ni kwamba, wale waliouliza maswali ya msingi wanakosa haki, tunatoa maswali ya nyongeza ambayo siyo ya msingi kwa waliouliza. Kwa hiyo, ninaona afadhali waliouliza angalau wajibiwe kwa sababu muda unaweza ukakosekana wa kuwapangia tena kwa sababu tuna maswali mengi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Godbless Lema, alisimama kuhusu utaratibu na akawa ameomba kwamba,

kama mtu anasema mambo yasiyo ya uongo kama Waziri Mkuu hatua gani zichukuliwe. Nilijibu kwamba, sasa Bunge hili linaanza kukosa adabu. Ninapenda nitumie kifungu kinachohusika kwa maelezo, naomba wote mnisikilize vizuri. Nitasoma kifungu karibu chote cha 63.

Kifungu cha 63(1) kinasema: Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kabisa kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge ye yeyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha tu.

(2) Mbunge ye yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kuwa anasema uongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au iloandikwa na vyombo vy ya habari.

(3) Mbunge mwengine ye yeyote anaweza kusimama mahali pake na kutamka “kuhusu utaratibu” (ndivyo alivyofanya Mheshimiwa Godbless Lema), na baada ya kuruhusiwa na Spika, kudai kwamba, Mbunge aliye kuwa anasema kabla yake ametoa maelezo ya uongo kuhusu jambo au suala alilokuwa analisemea Bungeni; ndivyo alivyosema Mheshimiwa Godbless Lema.

(4) Mbunge anayetoa madai kwa mujibu wa fasili ya (3) ya Kanuni hii atakuwa na wajibu wa kutoa na kuthibitisha ukweli kuhusu jambo au suala hilo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Spika au Mbunge mwengine ye yeyote, baada ya kutoa maelezo mafupi ya ushahidi unaotilia mashaka ya dhahiri kuhusu ukweli wa kauli au usemi au maelezo juu ya jambo au suala ambalo Mbunge amelisema Bungeni, anaweza kumdati Mbunge huyo atoe uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake na kama atashindwa kufanya hivyo, afute kauli au usemi au maelezo yake hayo.

(6) Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake aliyyatoa Bungeni, atawajibika kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, papo hapo au katika muda atakaopewa na Spika kwa ajili ya kufanya hivyo.

Kifungu cha 63(7) kinasema: “Endapo Mbunge aliyetakiwa kuthibitisha kauli au usemi au maelezo yake aliyyatoa Bungeni atashindwa kufanya hivyo, anaweza kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake hayo papo hapo au katika muda atakaokuwa amepewa na Spika kwa ajili ya kuthibitisha kauli au usemi au maelezo yake.”

Kifungu cha 63(8) kinasema: “Endapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa Mbunge aliyetakiwa kutoa uthibitisho wa ukweli wa kauli au usemi au maelezo yake

aliyoyatoa Bungeni atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge na kama atakataa kujirekebisha kwa kufuta kauli au usemi au maelezo yake basi Spika atamuadhibu kwa kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi vitano.”

Ya (8) kama mimi nikiamua hapa Wabunge wengine wasiporidhika, wanatoa hoja kwamba hiyo adhabu ni ndogo. Sasa mimi naishia hapa. Mheshimiwa Lema, upo tayari kuthibitisha hayo maneno?

MBUNGE FULANI: Hayupo.

SPIKA: Na kwa sababu ...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ningependa nipaye mwongozo wako, kwa sababu katika maelezo yaliyoelezwa siyo ya kifungu ambacho Mheshimiwa Lema alikirejea. Wakati Mheshimiwa Lema anazungumza, aliomba Mwongozo wa Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) na hakusema Kuhusu Utaratibu. Aliomba Mwongozo wako kwamba, kwa kuwa Waziri Mkuu ni mtu mkubwa katika nchi yetu, siyo Mbunge wa kawaida kwa maana ya mchango wa Mbunge wa kawaida, ikiwa taarifa ambayo imetolewa wakati wa kujibu maswali na Waziri Mkuu haina ukweli; Mbunge atumie utaratibu gani katika jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, wewe ukatoa Mwongozo ukasema pamoja na maelezo uliyoyaeleza awali, anapaswa kuwasilisha taarifa. Sasa nimeshangaa kidogo ndiyo maana nataka Mwongozo wako kwamba, katika maelezo uliyoyaeleza umesema kwamba, aliomba kuomba kuhusu utaratibu wakati kimsingi aliomba Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Sawa sawa, ndiyo maana uamuzi wangu nasema akaandike na hii ndivyo inavyosema. Sasa nampa mpaka tarehe 14 asubuhi alete maandiko ya kuthibitisha maneno aliyoyasema; hivyo ndivyo nilivyotaka kusema.

Kwa hiyo, tarehe 14, kipindi cha asubuhi, atoe maelezo ya kwamba, Waziri Mkuu amesema uongo. Maana alisema kwamba, Waziri Mkuu amesema uongo; sasa anataka tumpe Mwongozo wa namna ya kufanya na akasema aandike! Kifungu cha 64 kinamda alete maelezo hayo mpaka tarehe 14. (*Makofifi*)

Waheshimiwa Wabunge ...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Kifungu cha 68(7).

SPIKA: Ndiyo, soma.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yataolewa papo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hayo ambayo yanazungumzwa sasa hivi ...

SPIKA: Yapi hayo?

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Eehh!!! Haya ya Mheshimiwa Mbunge, ambayo ulikuwa unatoa maelezo.

SPIKA: Eleza vizuri ni *Hansard* hapa. Mheshimiwa Mbunge yupi; jana wengi walikuwa wanaeleza hapa?

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Basi nisikilize kwanza.

SPIKA: Ndiyo nakusikiliza; Mbunge yupi unayemsema?

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mwongozo ambao ninaumba ni kuhusu maswali ya kawaida ambayo yanaulizwa, ambapo jana na juzi kuna maswali hayakujibiwa na Waheshimiwa Wabunge ambao maswali yao hayakujibiwa, walitarajia kwamba leo yatakuwemo katika *Order Paper* lakini kwa bahati mbaya hayamo; sasa tunataka kuuliza Mwongozo wako kuhusu hili linakuwaje?

SPIKA: Si namna hii; ungeniambia mimi nilikuwa nadhani ni suala la Mheshimiwa Lema kwa kuwa ndiyo msemaji niliyekuwa namzungumzia.

Sasa maswali, ndiyo maana nimekwambieni hapa nitajitahidi sana wale waliouliza swali la msingi wapate majibu. Kwa sababu mkiangalia katika orodha tuliyowagawia, kila Waziri amepewa orodha ya lini atajibu maswali fulani. Sasa tukiendelea kuacha maswali bila ya kujibiwa siku kwa siku, tunaongeza mzigo na kubadilisha. Ninyi nyote mmeshagawiwa ile orodha kuonesha lini swali lako litajibiwa. Sasa ndiyo maana natamani sana angalau maswali ya msingi yapate majibu kuliko haya maswali ya nyongeza yanayokuja hapa hapa, watu wameona mtu amejibu basi na wao wanasmama. Ingawa Kanuni inapendeza tuwe na maswali ya nyongeza zaidi ya mawili, lakini inakuwa mzigo, ndiyo maana najitahidi tupunguze maswali ya msingi. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi nadhani tunadaiwa maswali kama sita, tutayatafutia muda lakini tunajaribu kwenda taratibu kama tulivyowagawia kwanza.

Waheshimiwa Wabunge ...

MWONGOZO WA SPIKA

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Aah! Sasa Mwongozo siutaki, maana ninyi mnafikiri Bunge ni la Mwongozo tu; hili ni Bunge la kufanya kazi pia.

Waheshimiwa Wabunge, jana tulahirisha kikao chetu cha Bunge baada ya Kipindi cha Maswali ili tuweze kupata Viongozi wa Kamati zetu mbalimbali. Tunaendelea kuhitimisha Muundo wa Bunge letu, kwa sababu hawa Viongozi ambao wamepatikana jana, ndiyo wanaouna Kamati ya Uongozi, ambayo inamsaidia Mheshimiwa Spika kwa kumshauri mambo yote yanayoendelea humu ndani. Kwa hiyo, nafurahi kusema kwamba, Kamati zote zilitkeleza azma hiyo ya kuchagua Viongozi wake.

Viongozi waliochaguliwa ni kama ifuatavyo: Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar Kigoda na Makamu wake ni Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa; Kamati yetu ya Hesabu za Serikali, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa John Momose Cheyo na Makamu wake ni Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu; Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema na Makamu wake ni Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan; Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe, naona amekwenda Mtera tayari. Makamu wake ni Mheshimiwa Deo Haule Philikunjombe; Kamati ya Sheria Ndogo Ndogo, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Makamu wake ni Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba; Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na Makamu wake ni Mheshimiwa Mussa Azan Zungu; Kamati ya Huduma za Jamii, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta na Makamu wake ni Mheshimiwa Dkt. Faustine Ingelbert Ndugulile; na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Jenista Mhagama na Makamu wake ni Mheshimiwa Juma Mkamia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Kamati nyingine ni Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa James Daudi Lembeli na Makamu wake ni Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah; Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Makamu wake ni Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid; Kamati ya Nishati na Madini, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Januari Makamba na Makamu wake ni Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo; Kamati ya Viwanda na Biashara, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa na Makamu wake ni Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya; Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Makamu wake ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. (*Makofi*)

Kamati nyingine ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Makamu wake ni Mheshimiwa Angela Jasmin

Kairuki; Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mwenyekiti kwake ni Mheshimiwa Brig. Gen. Mstaafu Hassan Athumani Ngwilizi na Makamu wake ni Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka; na Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o na Makamu wake ni Mheshimiwa Rosesweeter Faustine Kasikila.

Waheshimiwa Wabunge, hizo ndiyo Kamati na hawa ndiyo wanaounda Kamati ya Uongozi ya Bunge na nategemea kupata ushirikiano wao wa karibu tuweze kufanya kazi vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, hizi Kamati zilipaswa kupiga picha, sasa hivi tuko Mezani, ngoja tufanye kazi kidogo tutakwenda kupiga picha baadaye.

HOJA ZA SERIKALI

SPIKA: Hoja za Serikali, tunaendelea na mjadala wa Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Wabunge ambao ningependa waanze kujadili hapa ni Mheshimiwa Mosses Joseph Machali, halafu Mheshimiwa Herbert James Mntangi na Mheshimiwa Lediana Mng'ongo.

MHE. MOSSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Rais, aliyoitoa mwaka jana. Awali ya yote, napenda kuwashukuru wapiga kura wa jimbo langu la Kasulu Mjini, Mkoani Kigoma; ninawaahidi kwamba, sitawaangusha, nitaweza kuwasilisha maslahi yao na kuyasimamia kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi, nitajikita katika Miradi ya Barabara na baadaye nitaendelea. Nimejaribu kuptitia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kubwa ambalo nalionna ni kwamba, Mko wa Kigoma bado unaonekana kubaguliwa. Sasa ushauri wangu na wito ambao ninapenda kuutoa kwa Serikali yetu ya sasa, ningeomba Mko wa Kigoma sasa uweze kukumbukwa na hatimaye barabara za kwetu nazo ziweze kuunganishwa pamoja na mikoa mingine ikiwa ni pamoja na nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu hata kuptitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo ndiyo imekuwa ikipigiwa debe na Chama Tawala. Kimsingi, kwa mfano Barabara ya Kigoma – Kidawe – Kasulu – Kibondo na Nyakanazi haipo katika Ilani ile. Sasa wito wangu, Serikali ifike hatua basi muangalie kwamba sasa Mko wa Kigoma unastahili kuweza kuunganishwa na mikoa mingine kwa lami ili kuweza kupunguza adha ya usafiri ambayo inaukabili mko wa Kigoma wetu hususan tunapokuwa tunasafiri kutoka Mko wa Kigoma kwenda katika mikoa mingine kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali hasa za biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, leo ni aibu, unatoka Mko wa Kigoma unakwenda Mko wa Mwanza, unasafiri zaidi ya saa 10 au 11. Kwa mfano, unatoka Kigoma saa 11.30 alfajiri kwenda Mwanza unafika saa 12.00 wakati mwingine saa 3.00 usiku. Hii hali ikiachwa

inakuwa ni hali ya hatari sana kwa sababu tunajikuta tunatumia muda mrefu sana mahali ambapo tungeweza kutumia saa sita tunatumia saa zaidi ya kumi. Kwa hiyo, wito wangu au ombi langu kwa Serikali, ifike hatua Mkoa wa Kigoma ukumbukwe kwamba, nao pia ni sehemu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iwapo hali itakuwa hivi; sijui na sidhani kama wananchi wataendelea kuwa na imani na Serikali iliyopo madarakani. Naomba Serikali iuangalie Mkoa wa Kigoma kwa jicho pevu sana na kwamba, wananchi tunahitaji barabara na siyo barabara za changarawe, tunahitaji barabara za lami kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna suala la Reli ya Kati; leo Reli ya Kati tukiiangalia ina matatizo makubwa. Pengine nafikiri suala hili linapaswa kuangaliwa sana ili kuhakikisha kwamba, reli inarudi katika hali yake iliyokuwepo siku za nyuma.

Katika kuipitia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba pia kuchangia kidogo kuhusiana na Sekta ya Elimu. Ukipariblu kuangalia Sekta ya Elimu Kitaifa kwa ujumla ni kwamba, ipo katika hali mbaya sana. Tatizo kubwa lipo katika mipango ya elimu. Binafsi, ninaamini hakuna Taifa ambalo linaweza likaendelea kama elimu yake haitolewi katika utaratibu ambao ni mzuri.

Nimejaribu kupitia kidogo kuhusiana na *Primary School Teaching Syllabus*, kwa mfano, somo la hisabati. Tatizo ambalo nimelibaini na ukijaribu pia kurejea *Education and Training Policy* ya Mwaka 1995, iliyosainiwa nafikiri wakati huo alikuwa ni Prof. Sarungi, *in comparison* na malengo ya Elimu ya Msingi katika muhtasari ya Hisabati kwa Shule za Msingi.

Kwa mfano, malengo ya elimu ambayo yameandikwa katika muhtasari ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili wa Hisabati na malengo ya Elimu ya Msingi yaliyoandikwa katika muhtasari wa Hisabati kwa Lugha ya Kiingereza, unakuta ni vitu viwili tofauti.

Kwenye muhtasari ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili, malengo yanaonekana yapo 18. Ukiwa kwenye muhtasari wa somo hilo hilo wa Elimu ya Msingi ulioandikwa kwa lugha ya Kiingereza, malengo unakuta yapo saba. Somo ni moja, kiwango cha elimu ambacho kinazungumziwa ni Elimu ya Msingi lakini malengo yamekuwa *stated* tofauti.

Mheshimiwa Spika, sasa hii *interpretation* yake ni nini? Binafsi imenijengea dhana moja kuona hawa *curriculum planners* au *curriculum developers* wanapokuwa wamekaa katika Wizara yetu ya Elimu, hawapo makini katika *ku-state objectives* za elimu yetu na ndiyo maana unapokwenda kwenye hizo *Primary School Teaching Syllabus* unakuja kubaini kabisa kuna utofauti wa *ku-state* malengo.

Sasa kama malengo yamekuwa *stated* katika mfumo na muundo ambao siyo sahihi katika somo moja tofauti ni lugha tu peke yake; *how comes* tuje tuseme kwamba tunajenga na kuboresha elimu yetu hapa nchini? Hawa watu ambao wana jukumu la kuweza kutekeleza mitaala kwa maana ya walimu wetu; wanawezaje kuwafundisha

vijana wetu kikamilifu na wakati malengo yenewe yametengenezwa katika namna ambayo ni tofauti?

Kwa hiyo, kuna kila sababu, binafsi naona Serikali ijaribu kuangalia kwa kukaa na wataalamu wetu waliopo katika Wizara ya Elimu na ikiwezekana waitwe na wahojive. Serikali iko hapa, Waziri Mkuu yupo hapa na Waziri wa Elimu yupo. Naomba waanze na mihtasari ya Elimu ya Msingi hususan wa somo la hisabati, waende wakaulize ni kwa nini wame-state malengo ya elimu kwa namna mbili tofauti.

Huo muhtasari ulioandikwa kwa Lugha ya Kiingereza unaonesha kuwa malengo ni saba tu ya Elimu ya Msingi, lakini ule ulioandikwa kwa Lugha ya Kiswahili umeonesha kwamba una malengo 18. Sasa kwa nini somo moja lioneckane kuwa lina malengo mawili tofauti?

Lipo tatizo mionganoni mwa watu ambao wanakaa na kutuandalia mipango ya elimu; hali ikiachwa hivyo ni kwamba, tutazidi kuididimiza na kuifanya elimu yetu ionekane haina maana.

Vilevile kuna tatizo moja; sasa hivi tunaona Taasisi zetu za Elimu ya Juu zimegubikwa na migomo pamoja na maandamano ya hapa na pale. Naiomba Serikali ijaribu kuangalia wale watu wanapokuwa wanaorodhesha madai yao mbalimbali wasionekane kwamba, wale watu ni watovu wa nidhamu au hawajui chochote kile.

Suala la msingi, inatakiwa Serikali ikae nao na iwasikilize kwa makini na ijaribu kufanya *analysis* ya madai yao, hapo ndipo inaweza ikatambua kwamba kitu hiki ni sahihi au siyo sahihi. Mimi binafsi naona kwamba ni sahihi.

Ukisema leo unamlipa shilingi 5,000 mwanafunzi wa Chuo Kikuu apate fedha ya *accommodation*, kwa maana ya malazi ikiwa ni pamoja na chakula, ukweli haitoshi. Naliomba Bunge lako Tukufu kwa kushirikiana na Serikali iliyopo madarakani, wajaribu kupitia viwango hivyo, hiyo shilingi 10,000 ambayo wanadai waweze kupatiwa.

Ninaamini wale vijana wanaweza wakawa na moyo wa kujifunza na kusoma vizuri na hatimaye kuja kulitumikia Taifa letu. Vinginevyo, iwapo tutaacha tu wanapo-raise hoja halafu matokeo yake tunawapelekea Polisi, nafikiri inakuwa siyo *best way* ya kuja ku-overcome problem ambayo inawakabili na ambayo inalikabili Taifa letu; hiyo migomo na maandamano tutazidi kui-experience. Niiombe Serikali ijaribu kutumia busara, ikae na watu wale na hatimaye waone jinsi gani ambavyo wanaweza wakamaliza tatizo hilo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wale Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ile *meeting* itafanyika siku ya Jumatatu baada ya kipindi cha Maswali, kwa hiyo sio leo. Halafu hawa *page boys and girls* wataongezwa kwa sababu idadi yetu imekuwa kubwa na wenyewe ni wachache. Wakati mwininge wanashindwa kufanya kazi inavyostahili. Kwa hiyo, tutawaongeza kuanzia wiki ijayo. Tumeshawateua, lakini sare inayohusika ndio inashughulikiwa. Kwa hiyo, baada ya kuwa na sare wataongezeka wengi tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Herbert Mntangi.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia na kutafakari yale ambayo Mheshimiwa Rais aliyazungumza. Naomba niseme kwamba tumempongeza sana Mheshimiwa Rais, tumekupongeza wewe kwa kuwa Spika na tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuteuliwa, lakini naomba pia niwakumbuke wananchi Wilaya ya Muheza ambao wameweza pia kunirejesha upya katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo makubwa mawili. Moja, nitatizama hali ya amani na namna ya kudumisha amani kama alivyozungumza Mheshimiwa Rais. Lakini vilevile nitatizama katika sekta ya maji na mazingira. Nianze kwa kusema haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tusipolijengea heshima Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni dhahiri kwamba ile hadhi yake kama mmiliki mmojawapo itashuka. Bunge ni chombo na mhimili wa kitaifa na lazima hilo tulijue na tuhakikishe tunalijengea heshima Bunge hili. Tusipofanya hivyo, heshima ya Bunge itashuka. Tutizame sana kauli zetu, tutizame sana vitendo vyetu tuweze kuhakikisha tunalo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bunge lisilokuwa na itikadi za chama, Bunge lenye heshima, Bunge linalotarajiwa kufanya kazi kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme tena jambo lifuatalo, “giza haliwezi kuondoa giza.” Methali hii nimeipata kwa Padri mmoja wa Kanisa Katholiki kule Bukoba. Kwanini giza haliwezi kuondoa giza? Tujikumbushe huko tulikotoka, tuna miaka 50 ya uhuru na katika miaka hiyo 50 miaka 34 tumekuwa na mfumo wa chama kimoja na katika mfumo huo wa chama kimoja na Katiba tuliyokwanayo ilikuwa inatuelekeza na kutuongoza na imetuongoza na tumeweza kupata heshima duniani na amani na utulivu katika taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka hiyo ya 1995 tukabdalisha mfumo, tukaingia katika Mfumo wa Vyama Vingi. Ni dhahiri kwamba lazima Katiba ibadilike. Lakini utaratibu wa kubadilisha Katiba ulikwishafanyika na ndiyo maana ile Tume ya Jaji Nyalali ya mwaka 1991 na vilevile Tume ya Jaji Kisanga mwaka 1998 zilifanya kazi kwa kupita na kuwashirikisha wananchi kutoa maoni yao. Ni kweli hali ya maisha inaendelea kubadilika, na kwa msingi huo ni lazima tukubali na sasa wote tunakubali kwamba ipo haja ya kuipitia upya Katiba. Tuweze kwenda na hali ya maisha yetu ya leo. Hilo Mheshimiwa Rais amekwishalikubali na sisi wananchi tumeridhia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, giza haliondoi giza. Giza lilikuwepo na lipo kwenye Katiba na ndiyo maana lazima tufanye marekebisho. Tutaondoje giza hilo? Si kwa giza, tutaliondoa giza kwa kuweka mwanga. Mwanga kwetu sisi maana yake nini? Mwanga kwetu sisi ni elimu. Elimu ya nini? Kwanza wengi hata hiyo Katiba iliyokuwepo sasa hivi tunayoitumia ambayo imetuwezesha hata sisi kufika hapa Bungeni leo kwa nafasi mbalimbali wengi hawaifahamu. Giza hilo. Lakini ni kweli tunasema yapo matatizo yanayohitaji marekebisho katika Katiba. Matatizo hayo ni yapi? Giza hilo. Mwanga ni elimu.

Kwa hiyo, lazima tutoe elimu ya Katiba kwanza iliyopo na pili kuchambua na kutathmini mapungufu yaliyopo katika hiyo Katiba na la tatu ni kupendekeza na kuridhia marekebisho ya mapungufu ya Katiba iliyopo kwa kuwashirikisha wananchi wote. Tumpe nafasi Mheshimiwa Rais, aunde Tume ya kuanza mchakato mzima wa marekebisho ya Katiba. Tuunge mkono na tufanye kazi kwa dhati. Tutakuwa tumepata elimu, tutafanikiwa kuliondoa giza. Giza haliondoi giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanaotaka kutekelezwa kwa Katiba mpya ambayo wala haijaanza kuandaliwa wala hajafanyiwa tathimini ndiyo wanaotuletea matatizo na migogoro katika nchi. Wanawashawishi watu ambao hata hao wananchi, hata yale mahitaji muhimu ya hiyo Katiba mpya bado hawayafahamu. Migogoro isiyokuwa na sababu, kauli zetu viongozi tuzitathimini tunapozizungumza. Zipo kauli, hamnijui mimi! Hamumjui Fulani! Tanzania haitatawalika? Hiso kauli gani? Tuziondoe, hazitusaidii, zinawaweka watoto wetu mahali pabaya, familia zetu na Watanzania kwa ujumla. Likitokea tatizo, sisi wenye uwezo ndio wa kwanza kukimbia tunawaacha wale wasiokuwa na uwezo, wao ndiyo wanapambana na hayo ambao tumeambiwa hapa si mabomu yale. Tunayaita mabomu. Giza haliondoi giza.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye maji na mazingira. Muda unakimbia sana. Ahadi za Mheshimiwa Rais ni nyingi, lakini nina uhakika Baraza alilounda litasaidia kuziondoa. Maji Muheza na hali ya mazingira ni mambo ambayo ni muhimu sana. Hiso ndiyo ahadi zilizoko mbele yetu katika Wilaya yetu ya Muheza na kwa uhakika viongozi mliopo mumsaidie Mheshimiwa Rais kuhakikisha yanatekelezwa. Maji Muheza Mjini, Mheshimiwa Waziri wa Maji yupo, najua jitihada anazofanya, tunakuombea Mwenyezi Mungu akubariki na asaidie Taifa hili tatizo la maji Muheza Mjini litakwisha.

Lakini vilevile barabara, ahadi za Mheshimiwa Rais, barabara ya Muheza kwenda Amani, mashamba makubwa ya chai, chai inachelewa kufika katika masoko ya kimataifa, minada inayofanyika Mombasa, lakini tunategemea sana mapato ya fedha za kigeni kutokana na mashamba makubwa ya chai yaliyoko Amani Muheza. Tusaidie barabara ile kwa hakika itengenezwe.

Mheshimiwa Spika, ahadi kubwa nyingine ya Mheshimiwa Rais inahusu mashamba. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, yupo pale, ni mtaalam mzuri sana. Asilimia 60 ya ardhi ya Wilaya ya Muheza imechukuliwa na mashamba ya katani, mashamba ambayo hayaendelezwi mpaka sasa. Tumeomba hati zifutwe, mashamba yarejeshwe kwa wananchi wapate ardhi, Kilimo Kwanza iwe kweli Kilimo Kwanza kwa

dhati na kwa vitendo. Nitaendelea kukumbusha, Wizara zinazohusika nilizozitaja kuhusu maeneo hayo.

Lakini mwisho niwakumbushe pia Watanzania wote hali ya hewa sio nzuri sana, hali ya mazingira tumeharibu sana mazingira, ukame unakuja kwa kasi kubwa. Matatizo ya maji yatazidi kuongezeka kwa sababu tumeharibu sana kwa kiasi kikubwa vyanzo nya maji. Wizara inayohusika na mazingira isaidie Halmashauri zetu. Wapime maeneo ya vyanzo nya maji na kwa hakika tutunze vyanzo nya maji. Muheza tunategemea Mto Zigi na umeanza kukauka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika ahsante sana kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza, naanza kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa kwanza mwanamke toka enzi ya uhuru na leo tukiwa katika miaka 50.

Pili, napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wanawake wa Mkao wa Iringa kwa heshima kubwa walionipa ya kunichagua tena kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili. Napenda niahidi kwamba sitawaangusha, nitafanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa. Napongeza pia na nakukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kilichowenza kunituea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya masuala ya UKIMWI kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao na kwa kunipitisha bila kupingwa na nawaahidi kwamba nitafanya kazi hii kwa kushirikiana na Wabunge wenzangu kuweza kuangalia majukumu ambayo Kamati hii imepewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kura alizopata na kikipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa, hotuba ambayo imetoe mwelekeo wa kazi ambazo ziko mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la amani na utulivu. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuweza kudumisha amani, mshikamano na utulivu katika kipindi chote cha miaka 50 ya uhuru. Naomba amani hii tusiichezee. Amani hii ikipotea hatutaipata tena. Ninaomba Watanzania wenzangu waendelee kuitunza hii amani ambayo Tanzania imeendelea kuwa kisiwa cha amani na kufanya kuwa kimbilio la wananchi wa nchi nyengine. Sisi viongozi tusiwe vyanzo nya migogoro kwa kuhamasisha migomo na kuhamasisha maandamano yasiyokuwa hata na msingi maalum.

Ninaomba sisi ndiyo tuwe watangazaji wa amani kwa ngazi zote tukiwatetea na kuwalinda wananchi wetu. Naelewa kwamba tatizo hili likitokea, wa kwanza kuumia ni wanawake na watoto. Ninaomba tulinde amani ili tulinde wanawake na watoto na

wananchi kwa ujumla kwa sababu sisi wengine wenye uwezo kama alivyosema msemajii aliyetangulia tutakuwa wa kwanza kukimbia na kuacha wananchi wetu ambao tunawahamasisha wakiwa wanapata taabu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo imefanya ya kuhamasisha wananchi kujiletea maendeleo ikiwa ni pamoja na kuanzisha mifuko mbalimbali ya kuwezesha wananchi wakiwemo wanawake kiuchumi ukiwemo mfuko unaojulikana Mapesa ya JK. Mifuko hii imesaidia sana kuweza kuwawezesha wananchi kujiletea maendeleo na wengi wao wamejiunga katika *SACCOS* na *VICOBA* na kuweza kupata mikopo. Ninaomba mifuko hii iongezewe mitaji ili wananchi wa ngazi za chini hasa waliopo vijijini waweze kupata na *SACCOS* ziweze kufikiwa na hii ninazungumzia pia na Benki ya wanawake. Ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuweza kuanzisha Benki ya Wanawake Tanzania na Tanzania imekuwa ni mfano wa nchi nyingi za Afrika, zinapenda kuja kujifunza jinsi ambavyo Tanzania imeweza kuanzisha Benki ya Wanawake. Sasa lililopo mbele yetu ni kuongeza mtaji ili Benki hii iweze kufika ngazi za vijijini na mikoani.

Itaweza tu kuonekana ni Benki ya ukombozi wa mwanamke kama haitaishia mijini. Itakuwa imefanya kazi nzuri kama na wanawake wa vijijini wataweza kufikiwa na hiyo ndiyo azma ambayo lengo lake ni kwamba iwafikie wanawake wote wa vijijini, wanawake wa mijini lakini pia na wanaume kwa sababu haikuundwa kwa ajili ya kuhudumia kundi moja tu, imeundwa ili isaidie wote kupata mitaji. Lakini tunaomba uwepo utaratibu hata kama haijaanza kupanuka kufika mikoani, basi viongozi wa Benki hii watembelee mikoa na kuweza kukutana na *SACCOS* za wanawake ili wawekewe utaratibu ambao utawawezesha hata kama iko Dar es Salaam, basi hao wanawake wa mikoani na vijijini pia waweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la ajira kwa vijana, naipongeza Serikali kwa kazi ambayo imefanya ya kuweza kuhakikisha kwamba vijana wanapata ajira. Lakini kwa vile kuna ongezeko kubwa la vijana ambao wamesoma ina maana ajira zilizoko Serikalini hazitoshi. Kwa hiyo, kazi iliyopo ni kuwafundisha vijana wanapokuwa shulenii kuanzia Shule za Msingi wafundishwe somo la kujitegemea. Kuanzia ngazi za juu kama ni Sekondari au Vyuo Vikuu, elimu ya ujasiriamali ifundishwe ili wanapotoka vyuoni wawe tayari, aidha, kuajiriwa au kujajiri na kwa maana hiyo wapewe mitaji ambayo inawezesha kuanzia maisha ikiwa ni pamoja na mikopo.

Kwa vile Serikali ina mpango mzuri wa kuanzisha Benki ya Kilimo, nina uhakika kwamba kama mafunzo yatakuwa yametolewa vizuri, vijana wetu wataweza kujiajiri kwa kuanzisha miradi mbalimbali ikiwemo pamoja na miradi ya kilimo. Kama itakuwa ni miradi ya kilimo, basi Serikali ihakikishe masoko ya bidhaa zinazozalishwa yaweeze kupatikana ili wananchi pamoja na vijana waweze kuuza bidhaa zao.

Lakini napenda kuishauri Serikali ihakikishe kwamba kunakuwa na vituo hata vijijini (*youth centres*) ambako wanaweza wakabadilishana mawazo, lakini pia

kuweza kupata taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za ajira, taarifa za shughuli mbalimbali ambazo zinaendelea ndani na nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongelee suala la afya. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri, lakini pia kwa kuanzisha mpango wa afya ambao utahakikisha kwamba kila kijiji kinakuwa na zahanati na kila Kata inakuwa na Kituo cha Afya na pia kuhakikisha kwamba kila Wilaya inakuwa na Hospitali ya Wilaya na Hospitali za Mikoa zinakuwa Hospitali za Rufaa. Sasa lililoko mbele ni Serikali kuhakikisha kwamba Hospitali hizo au mpango huo unavyoteklezwa, basi wataalam wawepo na isiwe tu ni majengo wataalam wakiwa ni pungufu tatarudi kulekule.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kwamba tukiboresha tutakuwa tumeweza kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na kwa hatua hii tutakuwa tumeimarisha afya za wananchi wetu. Pamoja na kwenye Hospitali za Mikoa ambazo zitakuwa ni Hospitali za Rufaa, napenda kitengo cha *Physiotherapy* (kitengo cha masuala ya mazoezi ya viungo) kiimarishe. Hospitali nyingi zina hivi vitengo, lakini havina wafanyakazi.

Kwa mfano, Hospitalia ya Mkoa wa Iringa ina mfanyakazi mmoja tu ambaye anashughulikia masuala ya *physiotherapy* na tunaelewa kwamba matatizo haya ni makubwa, kuna ajali nyingi sana ambazo zinasababisha wananchi wengi kuwa na ulemavu na wengine kuhitaji mazoezi ya viungo. Kwa hiyo, kama Hospitali zitaboreshwa, basi hiki kitengo kipewe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, toka juzi tumeletewa taarifa ya msiba kutoka Chuo Kikuu cha St. Johns' hapa Dodoma. Kuna Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga ambaye alikuwa *Deputy Vice Chanselor Academics of the University* amefariki Dar es Salaam. Maiti nadhani inafika leo, lakini kuzikwa ni kesho hapa hapa Dodoma, Ipagala kule ambako alikuwa anaishi.

Mheshimiwa Prof. Daimon Mwaga alikuwa Mbunge hapa. Alikuwa Mbunge *very active* na mimi binafsi amenifundisha. Kwa hiyo, nadhani wale watakaopata nafasi, wanaweza kushiriki kwenye mazishi. Saa ngapi, bado hatujui, lakini tarehe 11 hapa hapa Ipagala, Dodoma. Kwa hiyo, nimetoa hii taarifa kusudi wengine mnaomfahamu au mngependa kushiriki, msije mkashindwa kufanya hivyo. Haya, ahsante.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza kuchangia hoja toka nimekuwa Mbunge wa Bahi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Bahi kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao. Nawashukuru sana.

Nakishukuru sana chama changu cha Mapinduzi kwa kupitia Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kuniamini na kunteua kugombea Ubunge katika Jimbo la Bahi. Nakishukuru sana Chama changu. Naishukuru sana familia yangu, namshukuru sana mke wangu, watoto wangu kwa namna ya pekee ambavyo wamenisaidia na kunitia moyo wakati wote wa mchakato mgumu wa kugombea Ubunge.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee naomba niwashukuru wazazi wangu kwa kunilea vizuri hatimaye wananchi wa Bahi wakaniamini kwa uadilifu wangu na uchapakazi wangu na wakanipa Ubunge wa Jimbo la Bahi. Nao nawaahidi mbele ya Bunge hili kwamba sitawaangusha, nitafanya kazi kwa bidii ili kukidhi matumaini yao na mahitaji yao kwangu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza viongozi wote akiwemo Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa kuwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu ya pili, kuwapongeza Mawaziri, Manaibu Mawaziri, kuwapongeza Wabunge wenzangu wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa katika Majimbo yao na leo tuko hapa pamoja tukichapa kazi kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo aliiwasilisha hapa Bungeni. Hotuba ile imetupa mwelekeo sisi Wabunge namna ya kushikamana na Serikali katika kufanya kazi ili kuwaleta Watanzania maendeleo katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Tunapongeza Mheshimiwa Rais kwa mambo mengi, nami nikiwa mkazi wa hapa Dodoma katika Mkoa wa Dodoma, ingawa ilionekana kwamba Mheshimiwa Rais hajathubutu, lakini nataka niseme Mheshimiwa Rais amethubutu na siyo katika jambo moja, amethubutu katika mambo mengi toka ameongoza katika miaka mitano iliyopita. Sisi tunapongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uthubutu wake wa mambo mbalimbali.

Kama hoja ya wenzetu kwamba Mheshimiwa Rais lazima aje apongezwe na Rais ajaye, mimi naamini Rais ajaye mwaka 2015 atatokana na Chama cha Mapinduzi na siku akitembelea Chuo Kikuu cha Dodoma, basi atampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wake wa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Dodoma ni Makao Makuu ya nchi yetu na kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma umebadilisha kabisa mandhari na ushiriki wa watu katika shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Dodoma. Sisi tunafurahia watu wa Dodoma na tunaamini Chuo Kikuu kadri kinavyoendelea kukamilika kitatuletea manufaa makubwa kwa Mkoa wa Dodoma na pia kwa wananchi wote wa Tanzania hii. Dodoma ni katikati ya nchi yetu na wanafunzi watakaokuwa wanakuja hapa, watakuwa wanakuja karibu na mahali walipotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Watanzania wenzangu kwa kweli kwa kushiriki Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu wa hali ya juu. Nawashukuru sana Watanzania kwa kupuza vishawishi vingi vilivyokuwepo katika

Uchaguzi Mkuu. Viko vishawishi vizuri kama vilivyotolewa na Chama cha Mapinduzi kuititia Ilani, na viko vishawishi vibovu vilivyotolewa vya ukabila na udini. Lakini, wananchi wa Tanzania wamevikataa, wamewachagua Wabunge, wamewachagua Madiwani, wamemchagua Mheshimiwa Rais kutokana na uwezo wake wa kufanya kazi aliyoionomba mbele yake. Nao nawapongeza sana. Ushahidi mzuri ni mimi ambaye natoka katika Jimbo la Bahi, mimi sio Mgogo, lakini walinchagua kwa asilimia 95 na kuwa mionganoni mwa Wabunge waliopata kura nyingi kuliko Wabunge wengi katika nchi hii. Nao nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie habari ya suala la Sekondari za Kata. Waheshimiwa Wabunge wamelizingumzia vizuri, wamesifu Serikali yetu kwa kuthubutu kuanzisha Sekondari za Kata, Sekondari ambazo tunaamini miaka michache ijayo zitatoa matunda mazuri kwa wananchi wetu wengi kupata elimu ya sekondari. Sekondari zetu za Kata zimekuwa na changamoto, lakini huwezi kukabili changamoto kama kitu hicho hujakianzisha. Lakini kwa kuzianzisha sasa tunaanza kuipanga kujua namna gani changamoto hizo mbalimbali tunaweza kuzitatua ili sekondari zetu hizo ziweze kufikia viwango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini nipongeze sana uamuvi wa Serikali kuzihamishia sekondari hizi katika Halmashauri za Wilaya. Wakati huo tulikuwa na sekondari chache, kwa mfano katika Wilaya ya Bahi kulikuwa na sekondari nne tu. Kwa kweli kuititia Wizara wangeweza kuzi-control. Lakini sasa tuna sekondari 20 katika Wilaya ya Bahi, kwa kila Kata ina sekondari yake. Ilikuwa siyo rahisi ukijumuisha na sekondari nyingine zote katika nchi nzima Wizara kuweza kuendelea ku-control hizi sekondari. Lakini kwa kuzirudisha katika Halmashauri sekondari hizo zinaweza kupata huduma ya karibu ya viongozi na kusimamiwa kwa karibu na zinaweza kupiga hatua ya haraka.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge Mmoja Alipita Mbele ya
Mbunge aliyekuwa akizungumza na hivyo kukatisha
kati ya Mzungumzaji na Spika)*

SPIKA: Mheshimiwa, samahani! Ulipokuwa unapita, ulikuwa unakatisha kati yangu mimi na msemaji, kitu ambacho Kanuni inakataza. Yaani ulivyo simama hapo, tayari umenizua mimi nisimwone yule na umemzuia yule asinione mimi.

Waheshimiwa Wabunge, hatukuwafundisha hili, kwa hiyo, unapoingia au unatoka kama kuna msemaji angalia usikatishe katikati ya msemaji na Spika. Kwa hiyo, alivyofanya huyu siyo sahihi. Hatukuwa tumewafundisha, na wengi wamekuwa wanafanya hivyo, lakini ni mara yenu ya kwanza, naomba mzingatia hilo. Mheshimiwa Badwel endelea.

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Lakini, katika kuzihamishia sekondari hizi katika Halmashauri zetu, yako bado mambo ambayo yameshikwa na Mkoa. Mimi ningelifurahi sana kuona kwamba kama tunavyoziendesha shule zetu za msingi kuititia Halmashauri na kwa kweli tuziendeshe hivyo hivyo hizi sekondari za Kata. Zibaki zile shule ambazo ni za ki-Mkoa. Kwa mfano, unamtoa

Mwalimu Wilaya hii unampeleka Wilaya nyingine, yale yaendelee kuwa *controlled* na Mkoa. Lakini hata kumpadisha cheo Mwalimu, wewe kama Mkurugenzi uliyemwona kwamba anafaa kutoka sekondari moja kwenda sekondari nyingine, lazima jambo hili ukapate ridhaa ya Mkoa.

Nilidhani mambo haya yangerudishwa Wilayani pia kwa sababu pale ndipo tunafanya nao kazi kwa karibu na Mkurugenzi anajua kabisa Mwalimu fulani ambaye ni wa kawaida katika sekondari fulani anaweza kufaa kuwa Mwalimu Mkuu katika sekondari nyingine kuliko kusubiri Mkoa waje watoe maamuzi. Kwa hiyo, nilidhani huo usambazaji wa madaraka ungerudi vizuri, yabakie mambo machache tu ili Halmashauri ziweze kusimamia vizuri sekondari.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoendelea kuzikabili sekondari hizi ni nyingi kama walivyoeleza Wabunge wenzangu ukiwemo upungufu wa madarasa, upungufu wa walimu, upungufu wa vitendea kazi na kadhalika. Lakini uko mpango ambao umezinduliwa na Serikali na mimi nataka niupongeze unaosema Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa Pili ambao nikiangalia na nilivyouona fedha zake nyingi sana zitatoka kwa wafadhili.

Lakini, mimi nilidhani umefika wakati pia sisi kama Serikali kuamua na kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, kama yako matumizi ambayo kwa kweli sio matumizi ya lazima, yangesimamishwa kwa kipindi cha miaka miwili au mitatu ili fedha hizo ziende katika sekondari zetu ziweze kutatua matatizo yaliyopo kwa haraka zaidi. Nami naamini Serikali ikifanya utafiti itayaona hayo matumizi ambayo siyo ya lazima sana na matumizi hayo yatengwe na yaanishwe yaweze kupelekwa katika sekondari zetu ili pamoja na Mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa Pili ambao fedha nyingi zinatoka kwa wafadhili, lakini na sisi wenyewe kama Watanzania tuonyeshe kwamba tunajali na tuna haja ya kuhakikisha kwamba Sekondari hizo zinakamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, mtihani wa *Form Two*, leo tunasikitika sana kwamba watoto wetu wamefeli sana *Form Four*, lakini kwa kweli chanzo pia kimojawapo ni kuondoa mtihani wa *Form Two*. Mimi nashauri mtihani huu wa *Form Two* urudishwe kwa sababu kazi ya mwanafunzi ni kusoma na kufanya mitihani, sisi tunaogopa nini mwanafunzi kuendelea kufanya mtihani? Tunapoona kwamba shule za *private* zinafaulisha, wao wanafanya mitihani. Wanafanya *weekly test*, *monthly test* na miezi sita na kadhalika. Lakini sisi Serikali tunasema mtihani huu sasa uwe mtihani wa kawaida ambao haumfanyi mwanafunzi kuwajibika zaidi. Kwa hiyo, nadhani mtihani wa darasa la kumi urudishwe, utaongeza kuwajibisha wanafunzi wetu na tutaona matokeo yake wanafunzi wataendelea kufaulu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Zahanati kila kijiji, mimi nafurahia sana mpango huu, lakini nilikuwa naiomba Serikali tusifanye mpango huu kwa kukurupuka, lazima mpango huu uandaliwe vizuri.

Tumeona matatizo ambayo tumeyapata katika kuanzisha Sekondari za Kata, na katika Sekondari za Kata unaweza ukasubiri mpaka wanafunzi wafeli ndipo ujue tuna tatizo. Lakini katika kuanzisha Zahanati, huwezi kusubiri kupeleka Zahanati pale! Au Zahanati haina daktari, ina muuguzi, ndiye anayefanya kazi ya daktari, watu watakuwa papo hapo! Huwezi kungojea matokeo ya kesho au kesho kutwa. Kwa hiyo, lazima tuijandae vizuri, kama watalaam, waandaliwe vizuri ili waweze kwenda katika Zahanati zetu mapema.

Leo wananchi wamefungua Zahanati nyingi, lakini watendaji hawapo. Katika Wilaya yangu ya Bahi tuna Zahanati nne mpya, nzuri, hazijafunguliwa mpaka leo kwa sababu hazina watendaji. Wananchi hawatuelewi, wanaona haya majengo yamekamilika, mazuri, yanaanza kutumiwa na popo. Kwa hiyo, nilidhani kwamba tuijandae vizuri ili mpango huu wa kujenga Zahanati kila kijiji uweze kufanikiwa vizuri pamoja na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo, inaonekana kabisa hali ya hewa inavyotupiga chenga kwa haraka. Hali ya hewa inabadilika kwa haraka na kubadilika kwake hakutuletei matumaini, kunatuletea hatari. Kwa hiyo, nilidhani suala la Kilimo Kwanza kwa kweli liangaliwe upya, tusilichukue kijumla jumla kama tunavyolichukua sasa. Yapo maeneo yanayoweza kuimariswa katika suala la umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Wilaya ya Bahi ni Wilaya ya ukame katika Mkoa wa Dodoma, lakini ni Wilaya yenye fursa ya pekee katika kilimo cha umwagiliaji. Tuna *scheme* 10 za umwagiliaji katika Wilaya ya Bahi, lakini hakuna hata *scheme* moja unaweza kuona hii inazalisha, ikapunguza matatizo ya wananchi wa Jimbo la Bahi. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikaangalia maeneo kama hayo yaweze kuimariswa katika suala la kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofit*)

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza napenda kuchukua nafasi ya kwanza kuwapongeza wananchi wa Tarime kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kupitia Chama cha Mapinduzi. Nawaahidi nitashirikiana nao kwa hali na mali pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza yale yote tuliyowaahidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, napenda kwa dhati niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hii hotuba ya Mheshimiwa Rais ambayo ina sifa nyingi tu. Kwanza, ni hotuba inayoonyesha uzalendo, inaonyesha umoja na mshikamano katika nchi yetu, inasisitiza upendo, amani, utulivu na kuvumiliana. Ni hotuba inayoonyesha dira na mustakabali mwema wa maendeleo ya nchi yetu, ni hotuba yenye kusisitiza haki na usawa kwa Watanzania wote. Ni hotuba inayoweka mbele maslahi ya Taifa bila kubagua tabaka lolote lile.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alishawahi kutuambia, tunapogombea nafasi za uongozi, kila mmoja ajiulize ataifanyia nini Tanzania na sio Tanzania

itamfanyia nini. Vile vile alishawahi kusema, “Tanzania na tusipoisaidia, tumwombe Jalia atumulikie njia, Tanzania tuilinde, waovu wasiingilie”.

SPIKA: Haya msemaji wangu mzuri, usisome. Ni marufuku kusoma!

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, samahani nilikuwa nanukuu, baadhi ya nukuu nikasoma! Tanzania hii imeingiliwa na...

SPIKA: Maana hukusema nanukuu. Sasa unanukuu nini sasa?

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia nukuu za Mwalimu!

SPIKA: Aaah, haya!

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, Tanzania hii imeingiliwa na watu wa kila aina, watu waovu ambao hawaitakii mema, ambao wanasisitiza kuvunja umaja na mshikamano katika nchi yetu. Mimi ninalowaombeni wananchi wa Tanzania, hapa sisi ni viongozi, kila mmoja wetu ana wajibu wake wa kutoa mchango kwa kadri alivyochaguliwa na wananchi wake. Tushikamane wote kwa pamoja tuweze kuisaidia Tanzania. Mambo ya vitisho, kudharauliana, kusema mambo ambayo hayawezekani, hadithi za Alinacha, za kudhani, mimi naombeni tuziache. Tuweke maslahi ya Taifa mbele, mengine yote yatafuata. Kwa mfano, wale waliokuwa wakibeza hotuba ya Rais kusema kwamba yenye haina mwelekeo, Rais ametoa vipaumbele 13.

Mheshimiwa Spika, samahani, naomba ninukuu au nisome sehemu ya hitimisho la Rais. Rais amesema hivi; “Naomba nimalize kuwahimiza Watanzania wenzangu kwamba sote, mmoja mmoja na kwa umaja wetu tuamue kwa dhati kukusanya nguvu zetu, akili zetu na maarifa yetu yote kama ndugu wa Taifa moja kuifanya Tanzania kuwa mahali bora pa kuishi. Maisha bora kwa kila Mtanzania yawezekana.” Rais ametoa rai, hakubagua mtu yejote yule, hakubagua dini yoyote ile.

Lakini, jamani ninachowaombeni, tusipuuze kile ambacho Mheshimiwa Rais ametuagiza au Mheshimiwa Rais amesisitiza ili tuweze kushirikiana kwa pamoja kujengwa nchi ya Tanzania. Mimi naamini kabisa kwamba tukiweka maslahi ya Tanzania mbele, kila mmoja wetu ataweka falsafa ya kwamba Tanzania kwanza na mengine baadaye.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kwamba, Mwanafalsafa mmoja alishawahi kusema: “kuna akili za aina nne zinazomwongoza binadamu. Kuna akili ya kufikiri ambayo unatumia akili ya kuzaliwa. Kuna akili ya kuambiwa ambayo Rais wetu anasisitiza kwamba akili ya kuambiwa changanya na ya kwako. Kuna akili ya kuona ambayo inahitaji kufikiri zaidi na kutafakari, na kuna akili ya kusikia, si kila unachokisikia unakifanyia maneno. Kwa hiyo, naomba Watanzania tutumie akili ya kufikiri zaidi kuliko akili ya kuambiwa, tutaweza kujengwa Tanzania yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengine yote ambayo nitayachangia katika hotuba hii, suala la umoja na mshikamano katika nchi yetu linaletwa na amani. Mimi binafsi ninaposafiri nje ya nchi, najivunia sana ninavyoitaja nchi ya Tanzania mbele ya watu na zaidi nasisitiza kwamba Tanzania ina amani sana na hiyo amani ndiyo inayoleta umoja wetu na mshikamano wetu. Tusipoangalia hii amani yetu ambayo ilianzishwa na mababu zetu, waasisi wa Taifa hili wakairithi na sasa hivi tunataka kuichezea, mimi naamini kabisa tutakuja kuhukumiwa katika historia. Naomba Waheshimiwa Wabunge, historia isije ikatuhukumu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda nichangie suala la elimu kulingana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Ili tuweze kufanikisha suala la elimu katika nchi yetu, mimi naamini kabisa kwamba tuwashirikishe watalaan mbalimbali, wachapishaji wa vitabu pamoja na wale wadau wengine wote wa elimu. Mitaala ikibadilika, maana naamini kabisa kwamba matokeo ya sasa hivi yamekuwa mabaya kutokana na mitaala iliyobadilishwa mwaka 2005 na mwaka 2008.

Watalaan hao wakishabadilisha mitaala, wachapishaji wa vitabu wapewe taarifa mapema, wakishachapisha vitabu ndipo vitabu vikishatolewa, nafikiri mitaala ianze kutumika rasmi shulenii. Hii itatusaidia sana kuboresha elimu katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niongelee suala la madini kama sekta rasmi ya kuisaidia Tanzania kujiletea maendeleo. Naamini kabisa kwamba mikataba iliyopo katika sekta ya madini mingi ni mibovu. Naomba tuipitie upya na zaidi zaidi iwashirikishe wazawa. Wale wote waliobomolewa nyumba zao katika sehemu za madini, wanaodai fidia walipwe na vile vile mikataba hiyo iwe wazi. Hii itasaidia sana Watanzania wenzetu kupata ajira na vile vile itasaidia sana kuleta maelewano mionganii mwa wawekezaji na wale wazalendo.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba nchi yetu ina matatizo mengi sana. Tukikaa na kuanza kulumbana pasipokuwa na sababu, haitaweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Tuiombee Tanzania. (*Makofii*)

SPIKA: Haya, ahsante. Haya! Ananiambia nina maneno mazito sana, naomba uniongezee dakika! Nimemwambia tumekubaliana hizo hizo ,basi inatosha. Haya nimwite Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Titus Kamana.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuweka mchango wangu katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo, nafasi yangu ya kwanza nichukue kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kuwa na imani nami

na ninapenda niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwatumikia wakati wote kwa uaminifu na kwa uadilifu mkubwa ili tuweze kupunguza matatizo tuliyo nayo.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kusikiliza wachangiaji wenzangu waliotangulia toka jana na katika kufanya hivyo nilikuwa najaribu kujifunza ni kitu gani tunacho-*address* kinachohusu wananchi wa Tanzania. Lakini, katika kufanya hayo yote, nimegundua kila mmoja anajaribu kusema jambo linalohusiana na amani ambapo katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ndiyo kipengele chake cha kwanza. Mheshimiwa Rais anahimiza umoja, amani na mshikamano katika nchi yetu akiamini kwamba kama hakuna umoja, amani na mshikamano kwa Watanzania wote, basi yote tunayoyafanya ni bure.

Mheshimiwa Spika, wakati mwengine unashindwa kuelewa pengine unapomkuta mtu msomi tu, anajaribu kujadili na kulisema jambo ambalo pengine halina ukweli wowote ule katika mazingira ya kutaka watu waamini huo uwongo na wakati akiamini kwamba uwongo huo pengine unaweza kuhatarisha amani ya nchi yetu, mimi naamini kwamba kwa namna yoyote, iwe ni kwa maslahi yoyote yale, ya mtu binafsi au kikundi fulani cha watu, hawatapata maslahi hayo kama amani hii tuliyonayo itakuwa haipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimpongeze sana Rais kwamba ameweka kipaumbele cha kwanza kwa sababu ya mambo aliyoyaona, na kauli inapokuwa imetolewa na Rais wa nchi maana yake ni jambo zito.

Mheshimiwa Spika, nadhani pengine watu tunasahau historia ya nchi yetu. Mimi kwa umri wangu mdogo, nakumbuka nimesoma Shule ya Msingi nina kaptula moja, viatu sivijui. Katika miaka 50, tumefanya mambo mengi sana ya maendeleo, lakini hakuna maendeleo duniani kote ambako hayana changamoto. Tuna miaka 50 ya uhuru. Ukipata uhuru toka mwaka 1961 miaka pengine 10 mpaka unafika 70 tulikuwa bado tunahangaika kujenga uhuru wetu na kufurahia tu uhuru, ndiyo ikaja uhuru ni kazi, Mwalimu akatupa maneno hayo, tukaendelea kufanya hivyo, lakini baadaye tukajikuta tunahitaji kujenga nchi yetu sasa, hayo yamefanyika, wasomi wamepatikana, leo tupo kwenye Bunge zuri kama hilii ni hatua za maendeleo hayo hayo.

Lakini wasomi wameongezeka, hali ya maisha imeongezeka pamoja na changamoto zinatukumba kutokana na kwamba maendeleo ya binadamu sasa katika mahali fulani hapa duniani yanataka yaende sambamba na duniani kwingine kote. Changamoto hizi hata angekuja nani bado zitabakia kuwepo pale pale. Watanzania wasikatishwe tamaa, waelewe kwamba tunaendelea na tunasonga mbele, changamoto tutaendelea kuzishughulikia, tumeshuhudia maendeleo mbalimbali hususan hata kwenye sekta ya elimu ambapo sasa tunazungumzia sekondari hizi za Kata na zimefanya vizuri miaka iliyopita, mimi nina sekondari zangu za Kata ambazo zimepeleka wanafunzi mpaka Vyuo Vikuu. Hii ajali ya juzi ni matokeo tu ya Walimu wengi waliokuwa wamepangiwa kwenye shule zile kwenda shule kuongeza elimu wakaziacha shule hazina Walimu.

Kwa hiyo, ni jambo ambalo linazungumzika na ninaamini kabisa Serikali yetu makini, sikuvi ya Chama cha Mapinduzi na kama ahadi zake ilivyokuwa katika tamko rasmi la Serikali kwamba wataliangalia jambo hili, kwa kweli mliangalie ili tuweze ku-clear hii *atmosphere* ambayo inataka kuonesha kwamba yote yaliyofanyika ni kazi bure.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba katika utekelezaji wa ilani za Chama cha Mapinduzi kuanzia zilikotokea na hasa hii iliyokwisha muda wake mwaka 2010 na sasa tunaianza nyingine hii ilani ya mwaka 2010/2015, basi izingatie katika kuleta matokeo halisi ya mambo tuliyoyafanya katika sekta zote. Manung' uniko na malalamiko yaliyopo yanatokana na kwamba mambo mengi hatujayamalizia, hebu tuyamalizie na tujikite katika kutenga bajeti itakayomalizia mambo yetu ili watu wayaone matokeo.

Mheshimiwa Spika, wanazuoni wanasema *the ends justifies the means*. Tukitoa matokeo sasa watu watajua kumbe hata utaratibu mzima tuliokuwa tunaufanya tulifanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili nataka kulizungumzia ni juu ya uwajibikaji wa watumishi wa umma. Hata kama tutakuwa na fedha nyingi namnagani, lakini watu wakaacha kuwajibika, kila mmoja akashindwa kutekeleza wajibu wake unaompasa kufanya huku akiweka mbele uzalendo, uadilifu na uaminifu na upendo kwa Watanzania wengine, hakika hatuwezi tukafika. Mimi naamini Serikali inatenga fedha za kutosha katika miradi ya kilimo, afya na elimu, lakini inawezekana pengine hatupati matokeo ya haraka kwa sababu uzalendo, uaminifu na uadilifu haupo kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa Watanzania wenzetu watumishi wa umma, kwamba yale ambayo wanayafanya yasifikasiwe kwa kasi inayotakiwa na kwa malengo ya sisi tunaongoza nchi kwa maana ya Chama cha Mapinduzi, wanatupa mzigo mkubwa na mgumu sana katika kujitetea mbele ya macho ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, makosa mengine ni ya watumishi wa umma, lakini Chama kinawajibika. Tutafanya nini? Lakini naamini kwa kasi wanayoiona ya malalamiko mbalimbali, basi wajaribu kutuhurumia kwamba sisi tunaahidi kwa wananchi na hivyo wao ndio wasimamizi na watekelezaji, wawe wazalendo na waweke uzalendo mbele.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tu suala la uwezeshaji na uwajibikaji, kwamba mimi sikubaliani na siamini sana kwamba eti Serikali haiwezi ikafanya biashara au haitakiwi kufanya biashara. Mimi nadhani kuna kila sababu pale panapokuwa pana shirika lenye maslahi makubwa, lenye faida ya haraka Serikali ni lazima iwekeze ili tuweze kupata fedha za kutosha. Kusema kwamba hatupaswi kuwekeza, tunajitoa, wakati mwingine tunakuwa hatueleweki maana yake unakuta kwa mfano mashirika ya simu haya yana faida kubwa sana, Watanzania wanapiga simu sana, unakuta kuna shirika lipo tu la watu fulani na mjanja mmoja pale ndiyo kasema anawakilisha Watanzania wenzake, sisi hatupati chochote. Mimi nadhani kodi peke yake haitoshi, tunahitaji magawio na sisi kwa sababu ndiyo wenye nchi tukisema tunataka hisa hapo tunazitaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, naomba nizungumzie suala zima la watu kuoneana wivu. jamani kuna watu wanafanya kazi sana, kuna watu hawalali, sasa imekuwa nchi ya manung'uniko, kila mmoja ananung'unika. Sasa *fashion* imekuwa migomo. Huyu anaona kupata maslahi yake ni kugoma, wanafunzi wanagoma, watumishi wanagoma, walimu wanasema hatufundishi, ni kama vile wanataka kutelekeza kazi kwa sababu ya kauli zetu sisi wanasiaya, kwa maana hiyo kauli zetu tuziangalie kwamba tunaliua Taifa.

Mheshimiwa Spika, watu ambao wangewajibika wanapotoa kauli kwamba kuna mafisadi wamefanya hivyo wakati kitu chenyewe hakina ukweli wowote, maana yake unawakatisha moyo wale wanaofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namwuliza ndugu yangu mmoja ni Mwalimu wa shule ya msingi, anasema toka ameanza kazi mwaka wa tatu leo hajakaguliwa na Mkaguzi. Zamani Mkaguzi alikuwa anakuja anakaa nyuma ya darasa anaangalia Mwalimu anavyofundisha. Je, fedha haitolewi ya kukagua shule? Mimi nadhani hapa kuna mambo ya kufanya. Lakini kubwa kuliko yote tusitelekeze kazi kwa kudhani kwamba kuna mtu fulani anafaidi, anafanya hivi, tunaliua Taifa hili, na hatuna mahali pengine pa kwenda, tutaendelea kuishi humu humu na matokeo yake utakuja kujikuta ulichokifanya ulimfanya mwanaao ulimfanya mjukuu wako.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Watanzania wenzangu tuwajibike na tufanye kazi kwa nguvu zote kwa ari na kasi inayostahili ili tuweze kuleta maendeleo ya nchi yetu. Ahsante sana, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia katika hotuba hii ya Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunijaalia afya njema na kwa kunipa nafasi nikateuliwa kama Mbunge wa Jimbo la Busega. Vile vile niwashukuru wapigakura wa Jimbo la Busega ambao walionesha imani kubwa kwangu na Chama cha Mapinduzi kikaniteua kugombea na nikashinda kwa kishindo. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Wabunge wenzangu ambao tumepita kwenye kinyang'anyiro kigumu cha uchaguzi na sasa leo tupo kwenye Bunge hili, naomba niwapongeze, lakini tufanye kazi kwa imani na kwa uadilifu ili tusiwaangushe wapigakura wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda na mimi niipongeze sana hotuba ya Rais, wakati anazindua Bunge hili, kimsingi hotuba hiyo imeleta matumaini makubwa kwa Watanzania. Ilikuwa ni hotuba nzuri na mimi kwa ufupi tu naweza nikasema imeonesha upeo mkubwa alionao Rais wa kimaono kuhusu Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tu kwa kuonesha shukrani za kwanza za jinsi mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kwa kuifanya Busega kuwa Wilaya kitu

ambacho kilikuwa kilio cha muda mrefu. Hii inaendana kweli na dhamira ya Serikali ya kusogeza maamuzi na huduma muhimu kwa wananchi. Kwa hiyo, wananchi wa Busega wanapongeza sana Serikali, lakini wamenituma niseme kwamba wangeomba sana mchakato wa kukamilisha taratibu za Wilaya kuanza kufanya kazi, zifanyike na zikamiliike kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie kwenye kipaumbele cha pili katika hotuba ya Rais, katika kuimarisha, kukuza uchumi wa wananchi na kwa kutumia kilimo kama njia muhimu sana ya kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo kinaajiri takribani asilimia themanini ya Watanzania, na kwa kushughulikia suala la kilimo ina maana ndiyo njia ya uhakika na ya haraka ya kupunguza umaskini wa watu wetu. Lakini tunapozungumza kuleta mapinduzi ya kilimo ambayo kweli yamekwenda sambamba na mpango wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi wa Kilimo Kwanza, kuleta mabadiliko ya haraka, hatuwezi tukakwepa suala la *Agro Mechanisation*, yaani matumizi ya zana kuondokana na jembe la mkono kwenda kwenye zana kubwa na za kisasa. Lakini kwa hali ilivyo hadi sasa bado matumizi ya matreka uko chini sana. Kwa mfano, katika Wilaya yetu ya Magu ambako tangu mwaka jana 2010 watu 17 waliomba kupatiwa mkopo wa matrekta kuitia mfuko wa pembejeo, hadi leo hii mwaka mzima baadaye hawajapata. Kwanza matrekta 17 ni machache sana kwa Wilaya, lakini vile vile mlolongo mrefu wa namna ya kuyapata unafanya dhamira yetu ya kufikia haya mageuzi uende polepole sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali iweke mpango wa makusudi kuwezesha upatikanaji wa matrekta kwa haraka zaidi, lakini kwa wingi zaidi ili wananchi wengi wahame sasa kwenye kilimo cha mkono kwenda kwenye kilimo kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji. Tanzania ina bahati nzuri kwamba ina maji mengi, tunayo maziwa makuu, ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, ziwa Nyasa, lakini inasikitisha kwamba kunapotokea kiangazi hata cha muda mfupi tu, watu wenye mashamba wanaoishi hata mita mia tano tu kutoka ziwani mazao yanakauka kwa sababu tu hawawezi wakayatumia yale maji. Kwa kweli hali hii ni muhimu sana, tufanye juhudhi za makusudi.

Mheshimiwa Spika, Busega, Mkoa wa Mwanza, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Kagera watu wana hamasa ya kutumia kilimo cha umwagiliaji lakini maarifa, teknolojia ya kuyavuta yale maji na kwa bahati nzuri sana yale mabonde hata hayana mwinuko mkubwa kwamba utapata shida sana kusukuma maji, lakini yake maarifa ya kutumia bado hawana. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ielekeze nguvu, aidha, kwa *scheme* ndogo ndogo, lakini nyingi hata *scheme* kubwa ili tuhakikishe kwamba tunanufaika na maji ya maziwa yetu haya.

Mheshimiwa Spika, nipongeze tu wakati fulani aliyekuwa Waziri Mkuu alishiriki kwenye mchakato wa kupinga ule mkataba gandamizi ambao ulikuwa unafanya Watanzania tusiwe na ruhusa ya kuyatumia maji ya Bonde la mto Nile na Ziwa Victoria. Kwa kweli haifai wala haipendezi Sudan, Misri wananaufaika na kilimo cha umwagiliaji

cha maji ambayo yanakusanya huku kwetu na sisi tunakufa njaa na kulia njaa hata sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nafikiri Serikali iweke juhudhi ya makusudi, watu wanufaika na maji ya maziwa haya. Mipango hii ikifanyika vizuri, kwenye Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Ziwa Tanganyika, Bonde la Ziwa Nyasa hii hali ya kulalamika njaa ya kila mwaka isingekuwepo na ninahakika ingekwisha kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningependa kulizungumzia ni suala la masomo ya kilimo na mazao ya mifugo. Tukiwa na masoko mazuri ya mazao na hata tukaingia kwenye *processing*, naamini kwamba wafugaji wetu, wakulima wetu watahamasika na kuanza kufuga na kulima zaidi kwa sababu watakuwa na hakika ya masoko. Kwa mfano, mifugo, tunazungukwa na nchi nane ambazo wakati wote zina upungufu wa mifugo. Hatuwezi tukanufaika na masoko hayo kwa sababu minada yetu iko duni na hivyo Serikali inakosa mapato, lakini na wafugaji wetu hawapati mapato.

Mheshimiwa Spika, upunguzaji wa umaskini ungekwenda sambamba sana na kuimarisha Vyama vya Ushirika, *SACCOS, VICOB*A. Ushirika ni mwokozi na mkombozi wa watu maskini. Nafikiri ni muhimu sana Vyama vya Vshirika Wilayani vikaimarishwa, havina vitendea kazi, havina wafanyakazi. Ni muhimu sana eneo hili likaimarishwa ili waweze kufanya kazi kuwafikia wananchi wengi zaidi waweze kushiriki.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ningependa kuipongeza Serikali kwa kuimarisha mamlaka za *EPZ* na *SEZ* (*Export Processing Zone* na *Special Economic Zone*). Mamlaka hizi kimsingi zilikuwa zinafanya kazi zinazoshabihiana, lakini kwa sababu sasa tunataka tuimarishe utengenezaji wa bidhaa za kusafirisha nje, lakini nafikiri hili lingekwenda sambamba na kuyatumia maeneo yetu ya mipaka vizuri. Maeneo yetu ya mipaka ukienda Sirari, ukienda Horiri, Kajumulo, maeneo ya upande wa Tanzania hayakupimwa na hayakupangwa vizuri. Hayavutii uwekezaji. Hii ni rasilimali ambayo tunaiachia, maeneo hayo sasa ni vizuri yakapimwa tukavutia uwekezaji na watu wakafanya biashara kubwa ili wenzetu waweze kuja kuchukua bidhaa kwetu tupate kodi na wananchi wapate mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nimekwenda pale Holili upande wa Kenya ambako kimsingi ni pakame kama jangwa na upande wa Tanzania ndiyo wenyne neema, wenyne ardhi yenye rutuba, wenzetu wametengeneza soko zuri sana ili wavutie bidhaa za Tanzania ziende kwao, lakini Serikali yao inakusanya kodi, sisi kwetu hatukusanyi chochote. Kwa hiyo, nafikiri sasa kuna daraja la mto Ruvuma limejengwa la umoja, nafikiri tuanze mapema kuweka maeneo hayo vizuri kwa uwekezaji na mipaka mingine ya Rwanda, Burundi na Uganda kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa nafasi.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini kabla sijasema lolote, natoa shukrani za dhati sana kwa wananchi wote wa Jimbo la Tunduru Kusini kwa namna tulivyoshirikiana katika uchaguzi uliopita

na Chama changu kikaibuka kuwa mshindi. Nawaahidi kwamba utumishi wangu utakuwa wenye kutukuka na yale yote ambayo tumekusudia kuyafanya tutamwomba Mungu tuweze kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimponeze sana Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya miaka mitano iliyopita na timu yake, na nimponeze kwa hotuba nzuri ambayo imejaa mambo yote ya msingi ambayo ndiyo matarajio ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikianza mchango wangu kwa upande wa sekta ya kilimo, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuanzisha *mechanisation* kwenye kilimo. Tulianza na *power tiller* na sasa hivi yameshaingizwa matrekta makubwa, lakini katika hili la matrekta makubwa na hata zile *power tiller* kuna kasoro kadhaa ambazo zimejitokeza na hasa kwa wenzetu wakusanya ushuru.

Mheshimiwa Spika, ninavyoolewa mimi na ninadhani Watanzania wote kwa ujumla kwamba trekta peke yake haliwezi kulima, linahitaji majembe, *harrow*, *tiller* na ili kilimo hicho kiweze kwenda vizuri ni lazima kuwe na pampu za kumwagilia maji. Lakini hivi vyote vinabebwa na *trailer*. Cha kushangaza, wenzetu wa *TRA* wanasema kwamba hawatatoza ushuru trekta, majembe pamoja na *harrow* zake, lakini pampu pamoja na *trailer* watatoza ushuru kwa sababu wanasema pampu zile pamoja na trela zinaweza zikatumika kwa shughuli nyingine ambazo siyo za kilimo. Lakini msingi wa haya matrekta huwezi kutumia *tractor* bila kuwa na *trailer* kwa sababu huwezi kubeba majembe, huwezi kubeba mafuta, huwezi kubeba na vifaa vingine vyote vinavyohusiana na *kilimo* bila kuwa na *trailer*. Sasa wasiwasni wangu kesho na kesho kutwa Mungu aepushie mbali, nchi hii inaweza ikaingia njaa halafu na wafanyabiashara wakaruhusiwa kuingiza mahindi katika nchi hii nayo watayatoza kodi?

Licha ya Serikali kusema kwamba mahindi haya yaingie bila kodi kwa sababu mahindi hayo hayo yatatumika kwa chakula, lakini kuna watu wengine watatumia mahindi hayo kwa kupika pombe. Sasa madhali mahindi yanaweza yakatumika kwa shughuli nyingine, basi nayo yatozwe kodi. Kwa hiyo, naiomba Serikali suala la kutoza kodi hizi *trailer* pamoja na *water pump* liangaliwe na kama ni la kisheria, basi ni vyema ikaletwa hiyo sheria hapa Bungeni tuifanyie mabadiliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikija upande wa nishati, miaka na miaka Bunge hili Tukufu limekuwa likisisitiza kwamba tungeweza kuyatumia maporomoko ya *Stigler* kuzalisha umeme na watalaan wamethibitisha kwamba pale panaweza pakazalishwa zaidi ya *megawatt* 2,000, bado tunaiangalia *Stigler Gorge* inatiririsha maji mpaka baharini mwaka hadi mwaka na kilio cha umeme bado kinaendelea. Nawaomba sana katika miaka hii mitano Serikali iangalie uwerekano wa kuanzisha umeme pale ili tuweze kupata umeme wa uhakika na wa kutosha.

Lakini sambamba na hilo, kama kweli tumedhamiria kupata umeme na umeme huu uwafikie wananchi, tuangalie taarifa zetu na hasa zile gharama za kuvuta umeme. Wenzangu waliotangulia wengi wamechangia katika hili kwamba gharama za kuvuta umeme ni kubwa ambazo Watanzania walio wengi hawawezi kuzimudu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tumesitisiza hapa na nadhani karibu Watanzania wote wanapenda mazingira yawe mazuri katika nchi yetu, wote tunapenda miti, lakini: Je, hizi *tariffs* za umeme bei za mafuta ni kweli zina mwelekeo wa kutaka kujenga mazingira yaliyo mazuri katika nchi yetu? Kwa sababu leo *tariffs* za umeme ni kubwa na zinaendelea kupanda mwaka hadi mwaka. Matarajio ya Watanzania ni kwamba watumie umeme huu katika matumizi ya kawaida ili waepukane na kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa. Leo bei ya umeme ni kubwa na Mtanzania huyu ni lazima ale, apike chakula chake kiive atafanyaje? Hatuwezi kumzuia kukata miti hata tukisema kwamba kata mti, panda mti, hivi kweli tutaweza kuwa na kasi hiyo ya kupanda miti kulingana na matumizi tunayotumia? Sasa mimi napendekeza kwamba *tariffs* hizi za umeme ziangaliwe na ikibidi hata ruzuku ya Serikali iingizwe kama kweli tunadhamiria kupambana na ukataji miti ovyo na kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika suala la miundombinu, kwanza naipongeza sana Serikali kwa uamuvi wake wa kuigawa Wizara ya Miundombinu kuwa Wizara mbili; Wizara ya Uchukuzi pamoja ya Wizara ya Ujenzi. Ninaomba sana Mawaziri hawa wawili na Wasaidizi wao wajikite miaka hii mitano kuhakikisha kwamba bandari zetu zinaboreshwu, zinakuwa nzuri na za kisasa zaidi zenye vifaa vizuri zaidi.

Upande wa Reli, tujitahidi miaka hii mitano tutafute fedha kokote zinakopatikana ikibidi hata za ndani tutumie tuhakikishe kwamba *gage* ya reli zetu inapanuliwa ili reli zetu ziweze kwenda kwa kasi na ziweze kubeba mizigo mikubwa.

Mapato ya mashirika haya mawili, reli pamoja na bandari yanayo uwezo wa kuchangia zaidi ya nusu ya pato la Taifa. Naomba sana katika hilo na vile vile Wizara ya Miundombinu nayo ijikite kuhakikisha kwamba thamani ya fedha za Mtanzania zinalingana kabisa na thamani ya kazi iliyofanyika. Barabara zetu sasa hivi ni vichekesho.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI SAID JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii mchana wa leo nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyeziwezesha mimi kuhakikisha leo hii ninakuwa katika jengo hili Tukufu la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwa kweli kwa dhati ya moyo wangu ningependa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa kufanya maamuzi sahihi ya kumchagua kijana wao shupavu Selemani Said Jafo leo hii akiwa katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli nimefarijika sana. (*Makofi*)

Mchango wangu wa leo katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, kuna mambo nataka niyazungumzie. Mimi katika kikao chetu cha kwanza nilijua kikao kile lengo lake kubwa ni kwa ajili ya kutuapisha sisi Waheshimiwa Wabunge na suala la pili kwa ajili ya kupokea Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hilo nilikuwa najua kwamba ndio dhununi sahihi

la kikao chetu cha kwanza. Kwa hiyo, nilikuwa natumaini Wabunge wote mara baada ya kuapishwa watacaa kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Maana Hotuba ya Mheshimiwa Rais, maana ndio *terms of reference* ya nini tunataka kufanya ndani ya miaka mitano ijayo, ndio maana nilishangaa sana kuona baadhi ya wenzangu wengine wakiinuka na wakiondoka. (*Makofi*)

Inawezekana walikuwa hawajasoma vizuri Katiba japokuwa wengine wanadai Katiba lakini walikuwa hawajaisoma vizuri. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara 63 (2) inasema, kazi kubwa ya sisi Wabunge, ni kusimamia na kuishauri Serikali na vyombo vyake vyote. Hili ndio jukumu kubwa sana la sisi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Rais aliyepita na Chama chake cha Mapinduzi alikuja kutupa nini kinatarajiwa kufanya baada ya kushika dola ndani ya miaka mitano ijayo. Lakini hotuba siyo jambo la ajabu sana, maana yake alishatoa hotuba nyingine katika kipindi kilichopita. Tukumbuke Bunge la Tisa, Mheshimiwa Rais alikuja na hotuba nzuri kama ile ile. Nilitarajia wenzetu wote tungekaa pamoja tufanye tathmini nini yamepatikana katika hotuba ya Bunge la Tisa Mheshimiwa Rais alivyohutubia hapa.

Mheshimiwa Rais katika Bunge la Tisa tukifanya tathimini ya haraka haraka aliweka vipaumbele kama hivyo tunavyoona hivi sasa. Jambo la kwanza, mpasuko wa Zanzibar. Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia hali ya Tanzania yetu ikoje, kwa kweli huwa ninafadhaika sana kuona kwamba hata hili jambo kubwa ambalo Watanzania na wenzetu wa nje wanaona ni jambo la faraja, lakini wengine wanashindwa kujivunia. Ndugu zangu Tanzania tunafanya mambo mengi sana mazuri. Lakini kwa bahati mbaya inawezekana hatujivunii yale mazuri tunayoyafanya. Hili ndio tatizo kubwa sana.

Kwa hiyo, ndugu zangu, naomba niwaeleze Bunge hili Tukufu hasa kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais, naomba lengo letu ni kuishauri Serikali. Bahati nzuri Waziri Mkuu na timu yake iko hapa. Lengo la Kikao hiki ni kwamba nii sisi kama Wabunge tunaishauri nini Serikali kupitia vile vipaumbele vilivyowekwa na Mheshimiwa Rais? Je, ni mikakati gani tuiweke kwa kuishauri Serikali ilimradi iweze kupanga vizuri, ili ndani ya miaka mitano utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ambacho kimeshika dola kiweze kufanyakazi kwa usahihi zaidi? Jamani ndugu zangu hili ndilo jambo la msingi na ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya kujivunia, kwa sababu sisi Wabunge kutoka Chama cha Mapinduzi tuna kila sababu ya kutamba na kujitanua kwa hali zote. Kwa sababu Mheshimiwa Rais alifanya kazi kubwa miaka mitano iliyopita na ndio maana Wabunge vijana wa Chama cha Mapinduzi, mwaka huu tumeingia wengi kuliko wazee wa Chama cha Mapinduzi. Wabunge vijana wa Chama cha Mapinduzi katika Bunge hili ni wengi kuliko Wabunge wote wa Vyama nya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuko hapa, lengo letu ni kujenga hoja. Mimi nashangaa baada ya hapa kuweka mipango mikakati baada ya kuisoma hotuba na kuichangia inawezekana watu sasa hivi wengine wamejifungia kukariri kanuni. Ndugu

zangu kanuni hizi ni kifaa kinachotusaidia kuyatekeleza yale wananchi waliyotutuma. Watanzania wanatuangalia nini tunakuja kufanya. Ndugu zangu uongozi ni dhamana na sote tujue kwamba tutakuja kuulizwa kwa hii dhamana tuliyopewa. Tuko hapa kuwakilisha wananchi wote wa Tanzania, hatuko hapa kwa ajili ya kusoma kanuni ilimradi uweze kuuliza swali, hatukufuata hayo. Kanuni zitatusaidia kutekeleza taratibu zetu za Bunge na ustarabu unavyoendelea. Bahati mbaya tunakariri Kanuni lakini tunashindwa kuzitumia kanuni kama zinavyohitaji. Ndugu zangu tujenge hoja. (*Makofi*)

Wanasiasa, sisi kama Wabunge, nasikitika sana kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaendeshwa na migomo eti ndio agenda yetu. Wananchi hawakututumia kwa agenda ya migomo. Inawezekana kwamba hata hayo yanayoendelea inawezekana kuna watu wana-*provoke* makusudi. Ni huzuni kubwa sana. Mimi ndugu nawasihi kwamba katika hotuba hii imeainisha vipaumbele mbalimbali. Vipaumbele hivi tuweze kuviweka nguvu ya kutosha, nini tunatakiwa tukifanye.

Kwa mfano, katika kipengele namba 13 kimesema kwamba: “kuhakikisha kwamba tunaenzi yale yote mazuri yaliyotekelzeza ndani ya miaka mitano na miaka mingine ya nyuma.” Yako mengi yamefanyika ndugu zangu. Ukiangalia suala la kilimo jinsi gani tumefanya, agenda ya Kilimo Kwanza imeainishwa sasa hivi na watu tunalifanya kazi. Kila Mbunge leo hii anajitamba kuhusu suala la *power tiller* ni kutokana na mpango mzuri wa Chama cha Mapinduzi kwa miaka mitano iliyopita. Lengo letu kubwa hivi sasa tunasema kwamba kikao hiki kinajadili katika miaka mitano ijayo. Inawezekana kuna sehemu fulani kulikuwa na upungufu, basi ikiwezekana kuhakikisha kwamba tunaongeza matreksa makubwa kwa ajili ya kubadilisha kilimo chetu.

Ndugu zangu, watu wanalamika kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa *ku-stabilize* suala zima la uchumi hasa kushindwa kulinda thamani ya shilingi. Lakini hawagundai kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndio iliyoweka uwigo, vijana wengi sasa hivi ukienda Kariakoo pale hata sisi magari yetu yanapoharibika *spare* zote zinapatikana pale. *Spare* na magari na vitu vyovoyote vinavyonunuliwa havipatikani bila pesa ya kigeni. Ina maana kuna uwigo mkubwa wa watu wanaokwenda sehemu mbalimbali kufuata bidhaa, lakini ina maana lazima tuwe na *balance of trade*.

Lengo letu ni kwamba sasa hivi kuhakikisha kwamba ikiwezekana sasa kama kilimo sasa hivi ndio mtaji muhimu na tukiangalia kwa mfano, Kenya ukiangalia taarifa ya habari ya jana watu wanahangaikia suala la chakula. Sisi tuangalia jinsi gani tunainvest katika suala zima la chakula kuongeza mahindi na mpunga. Tuhakikishe kwamba chakula hiki tunakizalisha kwa wingi kwa ajili ya kuwauzia wenzetu wa nchi ya jirani. Hilo ndio jambo la msingi ndugu zangu.

Agenda ya maji, wananchi sasa hivi wana agenda kubwa, kwa mfano mimi kwangu Kisarawe ukizungumza agenda kubwa ni agenda ya maji. Kwa hiyo, haya ndio mambo ya kuhakikisha kwamba jinsi gani tutayafanya. Kwa mfano, tuna mradi wa *World Bank*... (*Hapa kengele iliila kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waliokuchagua hawakukosea. (*Makofi*)

MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kunifikisha mbele ya Ukumbi huu nikiwa mzima. Lakini nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Magomeni kunirudisha tena kuwa Mbunge. Inshallah Mungu atanisaidia niwatumikie kama vile walivyotegemea.

Baada ya shukrani hizo na mimi ningependa nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Rais katika kipengele cha kwanza kabisa katika vipaumbele vyake. Mheshimiwa Rais, alitoa Hotuba yake nzuri sana na yenye ufanuzi wa kina na kubwa zaidi kama alivytangulia kusema kwamba hili suala la usalama na kudumisha Muungano ya Jamhuri yetu ya Tanzania. Kama tunavyofahamu tuna miaka karibu 40 na kitu ya Muungano wetu.

Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu wakati Muungano huu unaundwa nilikuwa tayari nimeshazaliwa. Kwa sababu hiyo, basi nina kila sababu ya kuweza kutofautisha kabla ya Muungano na baada ya Muungano. Muungano ukiwa unaundwa nilikuwa na umri wa miaka kumi na kitu. Kwa hiyo, huwa nawashangaa sana wale wanaojaribu kuuchokoachokoa huu Muungano lakini siwalaumu kwa sababu walikuwa labda wengine hawajaona kabla ya Muungano ilikuwaje. (*Makofi*)

Nakusudia kusema hilo kwa sababu ni kitu muhimu sana ambacho tunapaswa Watanzania kujivunia kuwa na Muungano ambao umetuunganisha kiinchi, kiutamaduni, kila aina, kwa sababu Mzanzibar na Watanzania Bara, sisi sote ni kitu kimoja kwa maana ya kila aina. Sasa jambo hili ni jambo kulitunza na jambo la kujivunia sana. Hivi karibuni tulijaribu kuweka mambo yetu mazuri kule Zanzibar kwa nia hiyo hiyo ya kuweza kudumisha Muungano badala ya kutofautiana. (*Makofi*)

Lakini mimi huwa nawashangaa sana wale ambao wanabeza Muungano huu, lakini pia kujaribu hata kuweza kujilinganisha kwamba hawa wachache. Lakini hivi vitu sitashangaa kule Zanzibar, sisi watu kama hawa ambao wanaona ukweli halafu hawataki kuukubali kweli huwa mtu kama huyu tunamwita kifuu, tena kifuu tundu. Hakifahamu kitu. Huwa tunapuuza tu, huwa tunasema kifuu tundu hicho. Tunaachilia mbali. Wazanzibar hili lisiwastue, msimamo wetu upo, tudumishe Muungano tuhakikishe Muungano unakwenda daima. (*Makofi*)

Kasoro zilizokuwepo tuna wajibu kuzisawazisha. Kama leo asubuhi kulikuwa na masuala kuhusiana na kosoro mbili, tatu au kero mbili au zinazoudhi baadhi ya wananchi, basi ni jambo la kulifuatilia kwa karibu sana hasa tukiona kuna baadhi ya watu ambao mbali ya kwamba wako nje, lakini kuna wengine wako katika taasisi ambazo zinashughulika na mambo haya ya Muungano hasa suala hili la TRA. Tatizo la TRA ni

zito na ni tatizo ambalo linahitaji kuchukuliwa hatua za haraka sana kwa sababu Zanzibar ili iendelee inahitaji kuwe na mpango mzuri wa biashara.

Kile ni kisiwa ambacho hakina ardhi ya kutosha, wala hakina madini ya kuweza kututoshaleza katika uchumi wake ni biashara tu ndio kitu ambacho kitaweza kuibua vipaumbele vingi vya kazi, maendeleo na kila kitu na uchumi kwa ujumla.

Sasa itakapokuwa chombo kile ambacho kinasimamia masuala ya forodha ambayo forodha yenyewe ndio inayopitisha bidhaa na kusafirisha ikiwa haiko sawa au kuna mwingiliano au tofauti ya maamuzi, basi kutakuwa na kosoro kubwa sana itakayoleta mtafaruku wa uchumi wa visiwani. Kwa mfano, mimi mwenyewe binafsi baada ya kusikia malalamiko ya wafanyabiashara wengi sana kule Zanzibar, niliifanya kazi siku kabla sijaja Bungeni kuona utaratibu hasa wa *TRA* inakwendaje.

Nilitoa gari Zanzibar nikaileta Dar es Salaam nikaangalia gari ambayo nililipia kutoka mwezi wa tano ushuru kule Zanzibar na *TRA* ya Zanzibar kamili nikaisafirisha mpaka Dar es Salaam nikaanza kuanzia Afisa wa chini kwa utaratibu nikaenda mpaka kwa *supervisor* nikaenda mpaka kwa Meneja, nikaenda mpaka kwa Kamishna mpaka Kamishna Jenerali.

Mheshimiwa Spika, humo mote kulikuwa na vikwazo vya kuipitisha ile gari kutoka Zanzibar kuja huku. Nilikwenda mpaka kwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha akasema hana muda wa kuongea na mimi, aliniudhi sana, lakini nimemsamehe. Hapo ndiyo mwanzo au ndiyo kitu ambacho nilichokiona kwamba maamuzi ya Ofisi ya *TRA* ya Zanzibar hayatambuliki wala hayaheshimiki na Ofisi ya *TRA* ya bara.

Mheshimiwa Spika, hilo ni tatizo kubwa sana na ilifika wakati wale wafanyabiashara kule Zanzibar wanasema afadhali kule *TRA* ifungwe, kwa sababu Zanzibar kuna chombo ambacho kinaitwa *ZRB* kinachokusanya mapato kwa ajili ya kodi zote za Serikali ya Zanzibar, kile kiweze kuchukua kodi kwa sababu Ofisi ya *TRA* Zanzibar haina maamuzi yanayotambulikana na Ofisi ya *TRA* Dar-es Salaam au kwa maana ya Bara.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa sijui ni watu binafsi au sijui ni utaratibu, kunahitaji mambo ya kuchukuliwa hatua haraka sana kabla mambo hayajaharibika ili sisi Zanzibar kule tuzidi kuendelea kama tulivyokusudia na tumekusudia na mtatuona na watu watatuona. Kuendeleza nchi yetu na kuendeleza Zanzibar tuwe katika ule mwito wa zamani Zanzibar njema atakaye aje. (*Makofî*)

Wazanzibari msishughulike na maneno ya watu wanaoubeza Muungano wetu, wanaobeza yale mambo ambayo sisi tumeshajiamulia msihangaike, hawa watu hawayajui, sisi tunayajua na tunajua Zanzibar na tunajua kila aina ya mambo, Zanzibar tuna mifano mingi sana. Kwa umri wangu nimeona mambo mengi sana, kama ni mapinduzi nimeyaona kwa macho yangu na sithubutu kuomba hata siku moja litokee jambo kama lile, hata siku moja. (*Makofî*)

Kwa hiyo, Wanzazibari msishughulike, sisi wawakilishi wenu tupo na tutahakikisha kwamba Zanzibar inang'ara na Muungano unadumu daima.

Mheshimiwa Spika, sitaki kumaliza muda wote, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. MASSOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nichukue fursa hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtambile kwa kunichagua tena kuwa Mbunge, naahidi kwamba tutaendelea kushirikiana kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, nataka niende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 27 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais alipogusia suala zima la fursa ya kupata elimu kwa wanafunzi. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao wanaishi katika Visiwa vya Bahari ya Hindi au katika Victoria na Mito wanapata shida sana ya usafiri. Tarehe 5 Agosti, 2010 vilio vilisikika katika Wilaya ya Sengerema, Ziwa Victoria wanafunzi 18 walikufa maji walipokuwa wakisafiri kutoka Kisiwa cha Kitandale kwenda Lukumbi. Wanafunzi watatu ambao walishikilia mtumbwi waliokoka. Mwezi mmoja kabla katika Mto Rufiji wanafunzi pia vile vile wakisafiri walipoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naiomba Serikali chondechonde kwa dhati kabisa, iandae mazingira ya kuwasaidia wanafunzi walioko katika Visiwa hivi, usafiri wa hakika ili kuepusha madhara yanayotokea. Si vyema hata kidogo Serikali kuandaa mazingira ya kupeleka ubani kwa haraka, lakini tatizo la uhakika linaachiwa.

La msingi la pili, ni vyema Serikali iandae mazingira ya kuweza kujenga shule kwa dharura ndani ya visiwa vidogo vidogo, hawa ni Watanzania, tusiwabeze kwa sababu ya uchache wao katika Visiwa hivi. Hilo lilikuwa ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 43 wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aligusia suala zima la nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma. Akasema uzembe, wizi, ubadhififi hautavumiliwa na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitapewa uzito unaostahili. Kuanzia mwaka 2006 mpaka 2009 jumla ya Halmashauri 30 ziligundulika kuwa na matumizi mabaya ya fedha na watumishi 921 walifikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la kusikitisha ni watumishi 14 ndiyo adhabu iliyotolewa, walishushwa madaraka. Mtumishi mmoja alipewa onyo, mmoja akashushwa mshahara, inaonekana wazi kuna kila aina ya dalili za rushwa ndani ya Mahakama. Inakuwaje mabilioni ya Watanzania yanapotea lakini hukumu inayotolewa ni hiyo?

Mheshimiwa Spika, lakini kuanzia mwaka 2001 mpaka 2006 jumla ya shilingi bilioni 4,403,000,000 zilihusishwa na wizi, ujisadi na ubadhififi, Serikali ikaenda Mahakamani ikashtaki kesi ya tarehe 21, chombo ambacho kinatoa haki Mahakamani ni ajabu kubwa. Bilioni 4.4 hazikupatikana. Wakati tukiihoji Serikali hapa Bungeni ikuambia kwamba fedha hizo hazikupatikana kwa sababu wahusika wametoroka, au

shahidi hakupatikana, ni aibu kubwa kwa Serikali. Inakuwaje Serikali mnakwenda Mahakamani kwenda kushtaki kuna wizi, ubadhirifu na ufisadi wa mabilioni ya fedha, leo mtuambie kwamba wahusika wametoroka, wametoroka kwenye mikono ya nani? Hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwa kuwa aligusia kwamba ripoti atazipa uzito unaostahili, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2007 ilibainisha waziwazi kwamba kuna upotetu wa fedha za Umma bilioni 2.3. Lakini pia vile vile ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2008 kuna wizi, ubadhirifu na ufisadi wa bilioni 3.5, ongezeko la asilimia 52, sasa hili ni tatizo kubwa. Ni tatizo kubwa, fedha za umma zinapotea, hakuna hatua zilizochukuliwa na imebainika wazi kwamba wale wote ambao wanaiba fedha nyingi Tanzania hawafungwi, wale ambao wanaiba kuku, mbuzi na ng'ombe ukienda gerezani wamefungwa miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiiba kweli Tanzania haufungwi, ndiyo ukweli ulivyo. Nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya Ulinzi na Usalama kipindi kilichopita, nimekwenda magerezani, watu wameiba ng'ombe na mbuzi miaka mitano, lakini walioiba mabilioni ya fedha upelelezi haujakamilika, tutafika? *Are we serious?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amegusia suala la uzembe, hata mafao ya wastaifu wetu wanapostaifu basi hawapati kile kinachowastahili. Ukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2007 katika majalada 7014 yaliyokaguliwa, majalada 514 yamelipwa pungufu shilingi milioni 416 ya wastaifu, wanapunjwa. Ripoti hiyo hiyo ukiangalia inayoishia tarehe 30 Juni, 2008. katika majalada ya wastaifu 5313, majalada 142 yamelipwa pungufu shilingi milioni 288, ni hatari kubwa, ni aibu kwamba hata kumbe wastaifu wazee wetu masikini wanapostaifu haki yao wanayopewa sio halali. Naiomba Serikali ipitie tena majalada yote ya wastaifu kwa miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha hayakuishia hapo. Ukiangalia hata Balozi zetu na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje bila shaka hili analijua, Balozi zetu za Tanzania zilizoko nje zinatumia matumizi mabaya ya fedha za Umma. Tunataka diplomasia ya kiuchumi, lakini kinachoonekana hivi sasa Balozi hizi zinaendelea kutesa fedha za Umma, pesa za maskini lakini hakuna hatua ambazo zinachukuliwa. Naiomba sana Serikali Mabalozi wote ambao wanatumia fedha vibaya basi wawajibishwe na warejeshwe nyumbani. Hatukuwatuma huko waende wakatumie fedha vibaya, tumewatuma wakaangalie matatizo ya Watanzania, watusaidie kipindi hiki ambacho tuna matatizo ya uchumi, ya chakula, waandae mazingira mazuri ili tuweze kupata chakula cha kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la walimu. Madeni ya walimu wamezungumza wenzangu walio wengi, lakini naiomba Serikali iandae mazingira ya kulipa madeni ya walimu kwa wakati unaostahili. Haya mambo yanayotokea, matokeo mabaya, basi tuangalie utaratibu maalum wa kuweza kuwasaidia walimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ambayo kwa kweli ni adimu sana kwa Bunge letu la sasa. Nawashukuru sana wananchi wenzangu ambao walinifanya niwe Mbunge katika Bunge hili la 2010, nawashukuru hata wale wanaopita katika Jimbo langu kwenda sehemu mbalimbali kwa sababu wanajua fahari na heshima ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia sana ukurasa wa tisa (9), 10, 11 na 13. Kurasa hizi zinazungumzia juu ya Muungano, Umoja wetu, Usalama wa nchi yetu pamoja na maamuzi ya wananchi wa Zanzibar kuunda Serikali ya pamoja. Hii nchi yetu ya Tanzania iliundwa baada ya viongozi wetu wawili wakubwa kukubaliana. Mzozo huu umekuwa wa muda mrefu; ooh hawakupata idhini ya wananchi, wengine wakajitetea ilipita kwenye Bunge, mwengine akasema imepita kwenye Baraza la Mapinduzi, tumekwenda mpaka tumefika sasa. Tumejua matatizo mengi yalitokea Zanzibar, Vyama Vikuu viwili, Chama cha *CUF* na Chama cha CCM vilikuwa ni maadui wakubwa sana vikatusababishia vyama hivi kukosa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nenda katika ukurasa wa 13 ambao Rais katika hotuba yake aliwashukuru sana Dokta Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Zanzibar na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*) Maalim Seif Sharif Hamad. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tendo ambalo limetendeka Zanzibar ni sifa ya Tanzania na ukitaja Tanzania huwezi kukiacha CCM, ni sifa ya CCM na ni sifa ya Chama cha Wananchi (*CUF*). Katika Afrika, haijatokea nchi ambazo zilikaa kwa pamoja na zikaamua kwa maneno tu tutaishi pamoja, tutaendesha Serikali kwa pamoja, hakuna, tena matatizo yaliyokuwepo, hakuna virungu, hakuna mabomu, sasa hiki ni kitu ambacho nafikiri na Bunge hili lingetoa heshima kwa Viongozi hawa kwa jinsi walivyotujengea heshima katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niingie kwenye suala hili la uchaguzi kidogo, *Zanzibar population* yake ni laki tatu au wapiga kura wote ni laki tatu au tano. Jimbo la uchaguzi la Zanzibar lina kura elfu nne, elfu tano, imezidi sana elfu nane. Tanzania Bara Jimbo moja lina kura sitini elfu, sabini elfu. Tunapokuja kwenye suala la Viti Maalum tunaambiwa tunahesabu kura za Mbunge walizopata Chama kile, sasa Majimbo matano ya Bara ni kura laki tatu, Majimbo matano ya Zanzibar ni kura laki tatu, Majimbo ya Bara ni kura zaidi ya elfu, laki tatu tu. Chama kimoja kinapata viti 24 kutoka Pemba, Ungunja mpaka Bara. Chama kimoja kinapata viti 22, lakini kwa sababu viti vile 22 vimepatikana katika upande ambao una wapiga kura kila Jimbo sitini elfu, tunakosa haki yetu ya Kikatiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu sio utaratibu wa watu wanaopendana. Naomba marekebisho haya ya Katiba tutafute mbinu ya kuwawakilisha wanawake, tuweze kupata wanawake ambao wanatoka katika Majimbo yetu, hata ukiwatazama wanachama wako au wenyeviti hawa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar ukizihesabu kura zao zote na

ukaziunganisha utakuta ni sawasawa na Jimbo moja la uchaguzi la Bara. Ni bahati nzuri mnawagawia kama walivyokuwa wanagawiwa wengine. Sasa tuondoe hii sifa kwamba tuna wanawake wengi, wanaingia kwa sababu tunawapa, tunawaingiza kwa maonevu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nimesikia kengele yako ya mwanzo, lakini ninachokuomba sana kabisa, mipaka yetu ya Muungano ni salama, watu wanaishi kwa salama na tutadumisha umoja wetu na nchi yetu kwa gharama yoyote. Pia tujitahidi kuondoa mambo madogo madogo ambayo hayatatusaidia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia na mimi katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa tarehe 18 Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuchangia hotuba hiyo, napenda kwanza niwashukuru wananchi wa Jimbo la uchaguzi la Mbogwe walionipa ridhaa ya kuweza kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu alitoa hotuba makini na inayoeleweka. Hotuba yenyewe ililenga kutoa mwelekeo wa namna gani Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya miaka kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 itakavyofanyiwa kazi. Kitu cha muhimu hapa ni kuliomba Bunge lako liunge mkono namna gani tutakavyoitekeleza Hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu katika Hotuba niombe tu nijikite katika baadhi ya masuala ya msingi. Jambo la kwanza ni kipaumbele namba tisa, kipengele hiki kinaelezea juu ya masuala muhimu ya ufanuzi wa huduma za kijamii hasa masuala ya afya, maji, umeme, barabara, reli, bandari na anga. Suala la afya ni la muhimu sana na bahati nzuri sana ndani ya ilani yetu ya uchaguzi kuna ule mpango wa maendeleo ya afya ya msingi. Mpango huu unapaswa uungwe mkono kwa dhati ili kusudi kwenye kila kijiji zahanati ipatikane na kituo cha afya kwa kila Kata kijengwe.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yote yanaweza yakaja pale ambapo kuna wananchi wenye afya bora. Wananchi wakiwa na afya mgogoro habari ya uchangiaji wao katika maendeleo ya Taifa itakuwa hauna msingi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweke msimamo makini kuhakikisha kwamba jambo hili linafikia mahali pake.

Mheshimiwa Spika, tukija kwenye suala la kilimo, Mheshimiwa Rais hakuliacha nyuma na Serikali yetu inazungumzia habari ya Kilimo Kwanza. Jambo hili ni la msingi pia kutokana na kwamba wananchi wetu walio wengi wanategemea zaidi shughuli za kilimo. Niombe basi yale ambayo yameainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais hakika yafanyiwe kazi likiwemo lile suala la kuanzishwa kwa Benki ya Wakulima.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wakulima kama ilivyoanzishwa Benki ya Wanawake na yenyewe basi ipewe kipaumbele ili kusudi wananchi wengi waweze kupata sehemu ya kuanzia kupata mikopo itakayowawezesha kuwa na uwezo wa kulima kilimo chenye tija. Sambamba na hilo maeneo yao basi yawekwe katika mfumo rasmi, maeneo yao yapimwe, suala la hati miliki za kimila Serikali ilitazame jambo hili kwa makini kusudi wananchi wetu watakapokuwa na hati hizo za kimila waweze kuwa na nafasi ya kupata hiyo mikopo itakayowasaidia katika kuboresha shughuli zao za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naomba tena niweze kuelekea katika suala lingine la nishati. Suala la nishati ni suala muhimu sana kwa sababu mapinduzi yoyote na maendeleo yoyote katika nchi yoyote ile inayotaka kwenda mbele yanategemea sana nishati, kwa sababu nishati ndiyo inayoweza kuongoza kujenga viwanda vya kisasa na kuweza kutanua maeneo ya kutoa ajira kwa wananchi. Nchi yetu inaongezeka kuwa na vijana wengi ambao hawana kazi. Lakini tukiwa na nishati ambayo inaonekana kuwa ni ya kupatikana kwa uhakika litakuwa ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri ni kwamba nchi yetu imejaliwa kuwa na madini ya makaa ya mawe na kwa sasa hivi nchi yetu imebainika kwamba ina madini ya *uranium* ambayo yanaweza yakasaidia katika kutengeneza umeme kwa kutumia zile *nuclear reactors*. Nchi zingine zinatumia hiyo. Sasa bahati nzuri kwa sababu Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na madini ya aina hii katika nchi hii basi ni vema nchi yetu na Serikali yetu ijiandae kikamilifu, tuweze kuwa na mpango kabambe wa kuweza kuyatumia madini haya pindi yatakapokuwa yanazalishwa katika nchi yetu basi vinu vya namna hii vya kuweza kuzalisha umeme vipatikane na mkakati huo uanze mara moja.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu. Ahsante sana.

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika hapa na kuwawakilisha Watanzania kwa ujumla wao na vile vile wananchi wa Wilaya ya Kilombero hususan wanawake wa CHADEMA kwa kunipendekeza kwenye Kikao cha awali kabisa cha Jimbo hususan Taifa kwa kunitfea kuingia kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo nakishukuru sana chama changu na Watanzania kwa ujumla waliopiga kura kwa wingi na matokeo ya kura walizopiga ndani ya CHADEMA kwa Wabunge wetu zikafananishwa na zikathaminiwa na tukapatikana Wabunge takriban 25 kwa uwiano wa uwakilishi sawasawa kwa kura walizopiga Watanzania. Hivyo nawapongeza sana Watanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Kwa CHADEMA mmezidi nusu kwa nusu.

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Kwa sababu ni uwakilishi mzuri sana kidemokrasia.

Pia napenda kukupongeza ukiwa kama mwanamke na mama ambaye umechaguliwa kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na naamini kwamba mama wakati wote anajawa na huruma na ni mwaminifu na nina hakika kwamba utasimamia Bunge letu kwa haki na demokrasia iliyo pana ili kila mmoja apate kutoa mawazo yake na yaheshimiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea au kuchangia kwenye hotuba ya Rais kama ilivyo haki yangu kama Mtanzania mwingine ambaye hajapata fursa ya kuingia kwenye Bunge wamechangia kwenye vyombo vyahabari hata kama hawakumsikiliza Rais ndani ya Bunge, lakini wamechangia katika maeneo mbalimbali kwenye magazeti na kwenye redio. Kwa hiyo, ni haki ya kikatiba, siyo lazima umsikilize ana kwa ana lakini unaweza ukachangia hata kama hukuwepo katika eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais nimeisoma, nimeiangalia na kuichambua kwa uwezo wangu niliokuwa nao na kuangalia vipaumbele vilivyopo katika hotuba hiyo ambavyo ni 13. Kwa uelewa wangu labda ni mdogo, naona kipaumbele kinapokuwa cha kwanza ni muhimu. Kulingana na mtiririko wa vipaumbele basi suala la usalama Rais wetu ameweka kipaumbele cha kwanza na ni muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika kipaumbele hicho kuhusu usalama wa Taifa letu, usalama huo na amani unaweza ukadumu ndani ya nchi yetu kama utaendana na haki. Hakuna amani inayosema amani na utulivu bila haki. Kwa hiyo, hivyo ni vitu viwili vinavyofuatana kama uji na mgonjwa. Kwa hiyo ni muhimu vitu hivi tunavyovizungumzia kuhusu usalama huo tuangalie je, haki kuanzia uhuru mpaka sasa vikoje?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli haki zinafuatiwa kwa karibu, ukizingatia suala zima la demokrasia ni haki ya kimsingi kwa Mtanzania na demokrasia inakuwepo ndani ya nchi yetu na hii ndiyo maana yanatokea mambo mengi ndani ya nchi yetu ni ukuaji wa demokrasia, ni kupanuka kwa demokrasia na demokrasia ni pana. Kwa hiyo demokrasia inapokua kuna changamoto zake na ndipo unapoona kwamba Watanzania wengi wanaelewa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati vyama vingi vinaanza si watu wengine ni viongozi kabisa, wengine wa Kiserikali, wengine wa Chama kilichopo madarakani walikuwa wanakwenda vijijini kuwadanganya Watanzania kwamba Vyama Vingi vina vita. Hii imetokea ndani ya nchi yetu. Lakini kadri demokrasia inavyozidi kukua na miaka mingi inavyopita wananchi wanazidi kuelewa, wanaona kumbe Vyama Vingi siyo vita, bali Vyama Vingi ni maendeleo ndani ya Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo chama kilichopo madarakani lazima kivumilie, kiwe na uvumilivu mkubwa, kikubali demokrasia, demokrasia ina upana wake, ina machungu na mazuri yake. Demokrasia jinsi inavyozidi kukua na kupanuka ni kwamba chama kilichopo madarakani kama kisipokuwa makini kinaweza kikapoteza uongozi kwa kuwa demokrasia inaruhusu kufanya hivyo. Sasa basi na kupoteza uongozi ni uchungu,

kwa sababu kama mtu ulikaa madarakani miaka mingi leo unapoteza uongozi yaani hujisikii vizuri. Kwa hiyo, ni vema kuwa na moyo mgumu wa kuvumilia, wewe ni baba, mtoto ashakumu si matusi, aliyenyea kwenye mkono huwezi kuukata mkono, lazima unawe maji. (*Makofi*)

SPIKA: Na si unamchapa kidogo. (*Kicheko*)

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, dawa ya mtoto anapolia mzazi hutakiwi kuchukua kiboko kumchapa. Mzazi mwema mwenye busara anajua tatizo kwa nini mtoto analia, anachunguza, mtoto mdogo hajui kusema analia tu. Kwa hiyo, mama mwema, au mzazi mwema anaangalia kwa nini mtoto analia. Pale unapoona kwamba ukimchunguza unaona kumbe labda sikio linatoa uchafu ndio maana mtoto anapata maumivu analia. Kwa hiyo, dawa ya mzazi ni kumchukua mtoto kumpeleka kwenye matibabu na mtoto atatulia.

Hivyo basi tatizo la migogoro, maandamano, migomo, lazima tuangalie vyanzo vyake ni nini? Kama hatutajua vyanzo vyake ni nini hatutaweza kutibu hiyo migogoro wala maandamano. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie chimbuko lake na hiyo iko ndani ya uwezo wa Chama ambacho kimeshika Serikali, ye ye ndiye baba na ye ye ndiye mama na hao ni watoto ambao wanafanya maandamano na migomo. Kwa hiyo, tuangalie tatizo ni nini.

Mheshimiwa Spika, wala huhitaji kuwa na digrii ili kufanya utafiti. Ni mambo ya kawaida yanatokea katika jamii. Unaangalia leo mfumko wa bei, kilo ya sukari kuanzia shilingi 1,400/= mpaka shilingi 2,000/=. Kipimo cha mafuta ya kula kule mtaani mimi naishi Us wahilini tulikuwa tunanunua kipimo cha mafuta ya kula shilingi 100 mpaka leo shilingi 200, kipande cha sabuni kuanzia 100 mpaka 200. Kwa hiyo Mtanzania wa kawaida kipato chake cha kawaida kiko pale pale, mwanafunzi wa Chuo Kikuu zamani alikuwa anasoma akipatiwa huduma zote pale ndani ya vyuo vyao. Kuna mayai, kuna maziwa, kuna mkate na *blue band*.

Mheshimiwa Spika, leo tuangalie wanafunzi wetu wa vyuo vikuu wanaishi vipi. Kwa mazingira yetu, kwa posho ya shilingi 5,000, wamevumilia na njaa haivumiliki. Ndiyo maana watoto wa maskini wale, wazazi wao hawana uwezo, wameshukuru Mungu mtoto alipofaulu, amemsomesha tangu msingi mpaka sekondari, mpaka eeeh hatari kabisa.

Mheshimiwa Spika, naomba niende haraka haraka kuhusu elimu. Naona tatizo hapa siyo kwamba eti tufanye uchunguzi. Nilikwenda kufanya ziara kwa kipindi kifupi katika baadhi ya Kata katika Wilaya ya Kilombero. Katika shule 11 nilizotembelea za sekondari, shule tisa zilikuwa hazina walimu wa sayansi wala hesabu. Kuna walimu watatu watoto 900, kuna matundu ya choo manne walimu na wanafunzi humo humo. Sasa shule kama hizi unategemea vipi zitatoa watoto ambao wanakwenda kwenye kidato cha tano.

Kwa hiyo, tatizo ni maboresho ya elimu hiyo ambayo tumeianzisha ya shule za Kata, sasa tunaboresha vipi. Walimu wapatikane, vifaa vipatikane, mishahara iboreshwe ili watoto wasome, hakuna umeme kwenye hizo shule. Ikifika saa 11 kule giza limeshaingia watoto wanarudi nyumbani, nyumbani anaporudi kibatali atawezaje kufaulu huyo mtoto. Kwa hiyo, bado miundombinu yetu kule chini ni midogo sana kumfanya mtoto aendelee kufaulu na kusoma vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kuhusu afya na zahanati. Katika ziara hiyo nimekwenda kutembelea vituo vya afya karibuni 10. Katika vituo hivyo daktari tunamwuliza anasema kwamba *MSD* ina miezi sita haijawahi kupeleka dawa kwenye hivyo vituo. Kwenye vituo hivyo madaktari wanatibu kama waganga wa kienyeji. Hawana mtu wa maabara, hawana vipimo. Sasa hapo afya itaimarika vipi.

Mheshimiwa Spika, naamini katika kuondoa umaskini tukiimarisha elimu, nchi yetu itapata maendeleo kwa sababu Daktari, Wabunge, Walimu wanatokana na elimu. Tukiimarisha afya katika ngazi ya chini kabisa watu watapata nguvu, watachangia maendeleo na nchi yetu itasonga mbele. Lakini bila kuweka hivi vipaumbele na kuviangalia kwa karibu itakuwa bado tunahangaika, tunatafuta mchawi lakini maendeleo yanazidi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, natokea Wilaya ya Kilombero, kwa hiyo, nisingependa kumaliza bila kusema mambo ya Wilaya ya Kilombero. Wilaya ya Kilombero kutoka Kilombero kwenda Ifakara/Ulanga ni kilometra chache sana. Lakini unatembea kutwa nzima. Barabara ni mbovu, mashimo kila kukicha, mvua ikinyesha kidogo tu hata kama waliweka *morum* yote inachimbika. Kwa hiyo, hali ya Kilombero na Ulanga na kwenye lile daraja la kuvuka kwenye ule mto kuelekea Wiilaya ya Ulanga hali ngumu. Rais wetu aliahidi tangu alipoingia madarakani angejenga daraja la Ulanga/Kilombero. Lakini mpaka leo bado liko kwenye makaratasi. Sasa sijui Serikali itatekeleza lini hiyo ahadi yake, wananchi wanazidi kuteseka. Barabara ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa asubuhi hii tumejadili vizuri, lakini muda uliobakia siwezi kumpa mtu mwingine. Ni mfupi mno. Kwa hiyo tukirudi jioni ataanza Mheshimiwa Bura, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Rashid Abdallah, Mheshimiwa Salum Barwany, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Ahmed Salum, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Aliko Kibona na Mheshimiwa Charles Mwijage. Kwa hiyo, mjiandae.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Chama cha Mapinduzi. Anaomba niwatangazie kuwa kutakuwepo na kikao cha Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi. Sijui kuna Kamati ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi, leo tarehe 10 mwezi wa pili katika Ukumbi wa Spika, jioni baada ya

kuahirisha Bunge hili. Tukahirisha ile saa 1.45 basi hao wanaofahamu ni viongozi wa Kamati ya Uongozi waende pale kuna kikao chao. Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa asubuhi hii. Niwatakie mchana mwema. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 6.57 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana, nilikuwa nimewaita Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Mheshimiwa Felister Bura? Mheshimiwa Salim Hemed Khamis.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Tatu nawashukuru wapiga kura wote wa Jimbo la Chambani, kwa kura zao na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu leo wamenirudisha Bungeni na naahidi kwamba nitashirikiana nao kwa kila hali katika miaka hii mitano.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia hoja hii kwa dhati kabisa nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa namna alivyoshughulikia mpasuko wa kiasasa Zanzibar. Wakati alipokuja hapa kuzindua Bunge la Tisa alisema namna anavyosononeka na hali ya kisiasa ya Zanzibar na kwamba angependa kutumia kila hali ili kuona kwamba hali ya kisiasa ya Zanzibar inatengemaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo Wazanzibari tumeelewana na ushahidi ni kwamba katika Uchaguzi Mkuu uliopita wa 2010 ulifanyika kwa hali ya utulivu na usalama mkubwa, haijapata kutokea. Lakini ushahidi mwengine ni kwamba jana tu kwa mara ya kwanza katika historia ya Vyama Vingi Wabunge wa CUF na CCM tumekutana katika Ukumbi wa Pius Msekwa chini ya Mwenyekiti na Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Dokta Balozi Ali Iddi Seif, kuzungumzia maslahi ya Zanzibar. Wazanzibari tumeelewa na tunasema kwamba tutaendelea kukutana na kushauriana kuhusu masuala ya nchi yetu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile Zanzibar sasa hivi kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kuna Rais Mheshimiwa Ali Mohamed Shein kutoka CCM, kuna Makamu wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Seif Sharif Hamad kutoka Chama cha Wananchi (CUF) na kuna Mheshimiwa Dokta Balozi Ali Iddi Seif, kutoka CCM. Halikadhalika Zanzibar sasa hivi kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Baraza la Mawaziri 16, ambalo limechaguliwa kwa uwiano wa kura za Urais ambazo zilipatikana katika uchaguzi uliopita. Kwa uwiano huo Chama cha Mapinduzi kimetoa Mawaziri tisa kati ya Mawaziri 16, Chama cha Wananchi (CUF) kimetoa Mawaziri saba katika Mawaziri 16 na kuna Manaibu Mawaziri ambao wamechaguliwa kwa uwiano huo.

Mheshimiwa Spika, Wazanzibari tumeelewana. Sasa kama kuna watu ambao wana wasiwasi juu ya ukubwa wa Majimbo yetu ya Zanzibar au idadi ya wapiga kura, nasema kwamba hiyo sio hoja. Wakati nchi hizi mbili zinaunganishwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliliona hili akasema kwamba kuna hatari ya kumezana katika nchi hizi mbili tukiziunganisha. Nchi kubwa kama Tanganyika kuungana na Zanzibar nchi ndogo kuna hatari kwamba huenda Zanzibar ikamezwa. Kwa hivyo, walikubaliana kwamba katika Serikali ya Zanzibar kuwe na Rais wake, Baraza la Mawaziri bila shaka na Katiba yake. Sasa suala la kwamba Zanzibar ni ndogo, Majimbo ni madogo au wapiga kura ni haba, hili halina mantiki hata kidogo. Wapo watu wanaleta chokochoko mbalimbali kuhusu makubaliano haya, lakini tunasema haturudi nyuma, tunasonga mbele, *aluta continua*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya sasa nianze kuchangia hoja. Watanzania wengi wameisoma au kuisikiliza hotuba ya kuzindua Bunge la 10 ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Wapo walioiunga mkono na kuipongeza, lakini wapo ambao wameitoa makosa au wameikosoa, haya ni mambo ya kawaida. Lakini mawazo yangu ni kwamba, hotuba hii imegusia maeneo mbalimbali ambayo yakifanyiwa kazi vizuri tunaweza tukajkwamua hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msingi ninaloliona ni kwamba, utekelezaji wa ahadi za Serikali au mipango ya Serikali ndio tatizo kubwa la msingi. Si katika hili tu lakini ukiangalia kwa ujumla Watanzania tupo mstari wa mbele katika kupanga na mara nyingi watu kutoka nchi mbalimbali huja Tanzania kusoma mipango yetu; lakini kwenye utekelezaji tumekuwa tupo nyuma sana. Sasa katika hili nafikiri maelezo ambayo Mheshimiwa Rais, ameyatoa ni mazuri kabisa, lakini utekelezaji wake kwa kweli sio mzuri, nitatoa mfano.

Mheshimiwa Spika, katika kifungu cha nishati, kwa mfano, nanukuu, katika Bunge la Tisa, Mheshimiwa Rais alisema hivi: "Mheshimiwa Spika, nishati ni sawa na chembe ya damu mwilini. Serikali ya Awamu ya Nne itatoa kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza upatikanaji wa nishati ya uhakika na rahisi vijijini na mijini. Tutapanua wigo wa aina ya vyanzo vya umeme na nishati kwa ujumla ili kuwa na nishati ya kutosha na yenye gharama nafuu kukidhi mahitaji ya uzalishaji viwandani, utoaji wa huduma za kijamii na matumizi ya nyumbani. Tutashughulikia kwa kipaumbele cha hali ya juu matatizo ya sasa yanayohusiana na upatikanaji wa umeme nchini." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia maelezo haya ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ni mazuri sana. Lakini utashangaa ni kwa vipi basi baada ya kupita miaka mitano, tatizo la umeme liko palepale na kwa kweli limekuja kwa nguvu na kwa kasi zaidi. Lakini kana kwamba hiyo haitoshi, ni kwamba nimesoma kwenye gazeti moja la hapa nchini kwamba *TANESCO* imeongeza bei ya umeme kwa 62.3% ndani ya miaka mitatu; hiyo ni hali ya hatari kweli kweli. Ikiwa nchi maskini kama hii inayoendelea, bei ya umeme inakuwa kiasi hiki basi inakuwa ni hali ngumu sana. Kwa kawaida wataalam wanasema kwamba upandishaji wa bei ya umeme katika nchi kama zetu usizidi 3%.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kupandishwa kwa umeme ni kwamba huduma muhimu kwa maendeleo ya binadamu zinakuwa ghali kama vile vyakula, usafiri, lakini vilevile uzalishaji wa viwandani unashuka sana na mara nyingine hata wale wawekezaji wanaikimbia nchi. Kwa hiyo, nafikiri jambo la msingi hapa ni kuona kwamba Serikali inajitahidi kuupa kipaumbele kweli kweli uzalishaji wa umeme nchini ili uchangie kwa hali kubwa kabisa maendeleo ya nchi hii, kama tunavyoambiwa kwamba umeme unaweza kuchangia zaidi ya 40% ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika shughuli ya kifungu cha pili cha vipaumbele vya Rais. Katika kifungu kile Mheshimiwa Rais, anasema kwamba Serikali itaendeleza juhudzi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini, ni kweli. Kazi hii imefanywa kutoka Awamu ya Kwanza ya Baba wa Taifa, kulikuwa na juhudzi hizo hizo, Awamu ya Pili ya Mzee Ruksa kulikuwa na juhudzi hizo hizo, Awamu ya Tatu ya Mzee Mkapa, halikadhalika juhudzi zilikuwepo. Lakini sasa ukiangalia ukweli ni kadri awamu zinavyozidi kusonga mbele ndio hali ya uchumi wa Mtanzania wa kawaida inavyoshuka. Hata kwamba wanauchumi wanasema kwamba uchumi umepanda, kwa mfano mara hii 7% lakini tuangalie ukweli, hali ya kiuchumi ya Mtanzania wa kawaida, imepanda au imeshuka?

Mheshimiwa Spika, nadhani hilo halitaki mwenge na kila mtu anajua kwamba Mtanzania wa leo anahitaji angalau apate mlo mmoja kwa siku ili aweze kuishi. Sasa ukisema uchumi umepanda kwa kweli! Lakini kuna ripoti ya utafiti wa bajeti ya Kaya ambayo imefanywa Tanzania Bara. Kwa kwa ripoti hii inayosema kwamba 34% ya Watanzania 40,000,000 wamo katika hali ya umaskini mkubwa ambao huwa wanatumia chini ya dola moja ya Kimarekani kwa siku. Lakini kuna 17% ambao kwa kweli hawa ni mafukara.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika na ukaweka rekodi katika *Guiness Book of Records* kuwa mwanamke wa kwanza Tanzania. Nimpongeze Naibu Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote wa zamani na wapya waliofika Bungeni hapa.

Pia napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mkanyageni kwa kunirejesha tena hapa Bungeni na naahidi kwamba Mwenyezi Mungu atujalie atupe moyo wa subira na wa kusaidiana wao na mimi na tufanikishe yote tulioahidiana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo nijikite katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Tarehe 18, kwanza kwa kumpongeza yeze kwa maneno mazito aliyoaeleza ya busara na hekima kubwa katika dunia hii ya leo. Katika jambo kubwa ambalo ningependa nijikite ni lile la kwenye ukurasa wa tisa mpaka kumi alilozungumzia Mheshimiwa Rais, kwamba tudumishe umoja wa nchi yetu na muungano wetu. Haya maneno ni mazito na yana mantiki kubwa. Tunayajua matatizo yanayotokea

duniani kote na hali ilivyo hapa Tanzania. Umoja huu tunaudumisha na Mungu akijalia tutaudumisha milele na Muungano wetu utakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa katika hali kama hii kinapotokea chama ambacho kinajaribu kuuvuruga Muungano huu au umoja huu ni jambo ambalo ni la kusikitisha hasa katika karne yetu ya leo. Mafanikio ya Zanzibar yaliyopatikana ya mpaka kufikia kuundwa Serikali ya pamoja, yalitokana na vuguvugu na matatizo makubwa ambayo leo tunaona aibu kuyazungumza yaliyosababisha mauaji ya watu zaidi ya 30 na wengine vilema wengi. Njia hiyo tulioitumia na baadaye tukaona haifai, viongozi wetu kwa busara za Maalim Seif Sharif Hamad na Rais wa Zanzibar aliystaa fu, Mheshimiwa Karume, tukafikia mahali tukapata maridhiano. Njia tulioitumia sisi sio vyema na si busara kuigwa tena na chama chochote kwamba kipitie njia zile zile za mapambano mpaka kufikia kuelewana na CCM. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikiwa miaka ya nyuma shulenii watu walikuwa wanatumia *slide rule* na leo kuna *calculator*, tukasema tukatumie njia ile ile ya *slide rule* tuache kutumia njia ya leo ya *calculator* hili litakuwa si jambo la busara. Chama chochote makini kitatafuta njia ambayo haitasababisha mauaji ya watu wake, kitatafuta njia ya kufanikisha umoja uliopo, kitatafuta njia ya kufanikisha Muungano wetu. Miaka 47 ya utawala wa CCM hatukusikia Mbunge hata mmoja wa CCM kukejeli udogo wa Majimbo ya Zanzibar na uhaba wa watu wa Zanzibar. Ni kitendo cha hatari na anayejua historia ya Muungano hawezi kufanya hivyo. Leo hii akitokea mtu akakejeli ni matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa vina mfumo wa Kitaifa; ilikuwa ina maana kubwa vyama vya kisiasa viwe na mfumo wa Kitaifa. Chama cha *CUF*, ni chama pekee cha Kitaifa chenye uwakilishi Pemba, Unguja na Bara. Isitoshe Chama Cha *CUF* ambacho kina Wabunge 24 wa kuchaguliwa, kimeweza kuingiza Bungeni Wabunge sita wa Viti Maalum kutoka Bara; huo ndio umoja wa Kitaifa. Bunge lililopita CHADEMA ilikuwa na Wabunge sita wa viti vya kuchaguliwa, hatukumwona hata mmoja wa kiti kutoka Zanzibar. Safari hii wana Wabunge 25 wa Viti Maalum, kuna Wabunge wawili tu wa kutoka Zanzibar. Ni nani anayeonesha umoja wa Kitaifa? Hili ni suala ambalo ni lazima lizingatiwe, tusirejee maovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningekuwa Mwanasheria ningewambia *my Learned friend*, kwamba tafsiri ya kusema Zanzibar inavunja Muungano aliyoitoa sio sahihi. Wala sishangai ikiwa mtu ameshindwa kutafsiri Kanuni za hapa Bungeni, akaweza kutafsiri hilo. CCM ipo Zanzibar ipo Bara, CCM wanakutana, hajatokea mtu akasema Zanzibar imevunja Muungano kwa kutengeneza marekebisho yale ya Katiba, naomba tuwe waangalifu. Siamini kabisa kwamba ni Wabunge wote wa Chama cha CHADEMA wana mawazo kama hayo na nawasihi tushirikiane kama tulivyoonesha ushirikiano kwa Bunge lililopita na tukawa pamoja na tukamstahi Dokta Slaa na wenzie wengine wote na tukashirikiana na safari hii ningeomba tufanye hivyo. Si busara kugawana, wananchi wanategemea umoja wetu. Naamini hivyo kwa sababu hata leo Mheshimiwa Akunaay, aliniambia tuelzane maneno haya lakini baadaye tufikie mahali tuelewane. Namshukuru sana kwa uono wake wa mbali Mheshimiwa Akunaay. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, ni pale katika kipaumbele cha pili alipoelezea masuala ya kukuza uchumi, kupunguza umaskini na akachukua hatua thabiti ya kuharakisha mapinduzi ya kilimo, uvuvi, viwanda na kadhalika. Haya maneno ni mazuri na naamini Mheshimiwa Rais, anania nzuri, lakini nina wasiwasi na watendaji. Maneno kama haya tumeyazungumza mara nyingi nyuma, lakini inavyoonekana kuna *vacuum* mahali hapa katikati. Hili ni jambo ambalo Serikali iliyopo madarakani ichukue hatua. Ni kitendo cha aibu kwamba sisi Watanzania 1978/1979 dola moja ya Kimarekani ilikuwa ni shilingi saba za Tanzania, leo hii shilingi 1450 za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo na ni tatizo tunapolinganisha uchumi wa nchi jirani zetu ambao tumewapita kwa rasilimali za kila aina. Mfano mdogo ni Malawi, inawezekanaje leo Malawi ambao vitu vingi sana wanachukua Tanzania, labda sisi tunachukua sukari tu, uchumi wao na fedha yao iwe nzito kuliko fedha yetu inayodondoka kila siku? Miaka mitano iliyopita Mozambique, ukitaka kitu chochote ni mamilioni ya mitikasi; leo hii miaka mitano tu iliyopita fedha ya Mozambique ipo *strong*. Haipo haja hata ya kuzungumzia Uganda tunaowajua, tuliofunga mikanda na sasa hivi fedha yao inakuja juu kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, ni kitu gani kilichopo Tanzania, Benki Kuu ikashindwa kuwa na mipango mizuri ya kiuchumi na kuipa fedha yetu thamani? Nia nzuri ya Mheshimiwa Rais, ya kuwa na uchumi bora, uvuvi, kilimo, uwekezaji mzuri, hatutafanikiwa ikiwa kwanza hatatalinda thamani ya fedha yetu. Imedondoka vya kutosha duniani, pamoja na matatizo ya uchumi yaliyopo duniani lakini kwa hili naiomba Serikali ya CCM ilizingatia kuna makosa *somewhere*, ni lazima yarekebishwe. Hatuwezi kuendelea na kudondoka thamani ya fedha yetu kwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu tunaotaka hauwezi kubadilika ikiwa hili halitopatiwa ufumbuzi na ushahidi upo *dolarization* ambayo hata Mheshimiwa Waziri alilitolea tamko hapa Bungeni hatuwezi kujilinganisha na *dolarization* ya Dubai halafu tukasema Tanzania *dolarization* kama hivi, haiwezekani kwenda dukani ukununua dola, nime-suffer mimi mwenyewe na Mheshimiwa Mwadini Japan, ninayo dola wameikataa nchi yenye uchumi mkubwa nataka maji ya kunywa nimeshindwa kupata maji ya kunywa lazima nikanunue kwa *Yen*, tusigeuze leo Tanzania kila kitu tunathamini dola tunaacha thamani ya fedha yetu inadondoka, naomba lichukuliwe hatua inayofaa, vinginevyo itakuwa hadithi tu za kukuza uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tatu ni kuboresha mipango na kusaidia wajasiriamali wadogo, hili nalo ni azma iliyokuwepo kuanzia hata miaka mitano iliyopita na kuna hata *terminology* likaitwa mabilioni ya Kikwete lakini yalivyotumika Jimboni kwangu hakuna mtu hata mmoja mpaka leo aliyefaidika na mabilioni ya Kikwete *plus* mabilioni ya Karume aliyoaingiza, fedha hizi zinatolewa katika mfumo gani? Tuwe wazi na kuwaambia wananchi ukweli. Ya kwanza hiyo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ya pili, lakini umemaliza vizuri.

MHE. MOHAMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoivasilisha tarehe 18 Novembra, 2010.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nianze kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mbozi Mashariki kwa kunirudisha tena katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana na nawaahidi kwamba sitowaangusha nitaendelea kufanya kazi kwa ari, nguvu na kasi zaidi ili tuweze kuendelea kusukuma gurudumu la maendeleo katika Wilaya yetu ya Mbozi lakini pia katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ambayo leo ndiyo tunajadili hapa tangu majuzi kuangalia mambo aliyoyaandika mle. Nina mambo mengi lakini kwa sababu ya muda nitachangia mambo machache sana.

Mheshimiwa Spika, wazungumzaji wengi wamezungumzia suala la amani ambalo kimsingi ndiyo kilikuwa kipaumbele cha kwanza katika vile vipaumbele kumi na tatu ambavyo Mheshimiwa Rais amezungumzia. Nilitaka niwakumbushe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Chama cha Mapinduzi, kama kuna watu ambao wanajali amani katika nchi basi viongozi na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanajali sana amani ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili linathibitishwa na maneno ambayo tumeyaweka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kwa idhini yako naomba ninukuu: “Kwenye ilani yetu tumetambua hilo na tunesema zimeanza kujitokeza dalili kwamba wanasiwa wanapandikiza mbegu za udini, ukabila na hisia nyingine zinazowatenganisha Watanzania, lengo lao ni kupata madaraka ya kisiasa bila kujali madhara makubwa kwa Taifa yanayoambatana na sera hizo za kibaguzi”. (*Makofi*)

Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inasema hivyo, kwa hiyo, kama ni suala la kutunza amani viongozi wa Chama cha Mapinduzi na viongozi wetu ambao wanaongoza Serikali wamejali amani ya Watanzania. Kwa hiyo, naomba niwakumbushe wenzangu kwamba Tanzania, pamoja na mambo machache yanayolenga kuvuruga amani yanayojitokeza katika nchi yetu lakini bado Tanzania inabaki kuwa kisiwa cha amani katika nchi nyingi zilizopo duniani lakini pia na katika nchi ambazo ziko katika Bara letu la Afrika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa vyama vyote tuienzi amani, amani ambayo Mwalimu Nyerere na wenzake waliomfuata wameendelea kuienzi na kutuachia, tusivuruge wala kujaribu kuchezea amani. Maana amani ikivurugika

hakuna wa kusalmika ni kama vile boti au meli iko baharini, unataka kutobia izame na wewe kwa vyovoyote vile utazama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie suala la kilimo. Mimi natoka Mbozi, nikizungumza hotuba ya Rais bila kuzungumzia kilimo ni kama vile nitakuwa sijazungumza. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wote tunajua wanashiriki kwenye shughuli za kilimo, lakini tumekuwa tunasema miaka mingi sana, Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amezungumza sana namna ya kuimarisha na kuboresha kilimo. Lakini naomba niishauri Serikali kwamba mapinduzi ya kilimo hayatakuja kama hatutafanya mpango wa makusudi kuonyesha kwamba tunafanya mapinduzi kwenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tunapozungumzia mbolea, tunazungumza viwanda vya mbolea, leo mbolea tunayozalisha katika nchi hii ni mbolea, nadhani mbolea ya Minjingu peke yake, mbolea iliyio nyingi tunaagiza kutoka nje na mbolea hii bei yake ni kubwa na Watanzania wengi hawawezi kumudu bei hizo za mbolea. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukue hatua za makusudi, kuna maeneo ambayo lazima tuchukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba tunajenga viwanda angalau katika mpango wa *Public Private Partnership (PPP)*, ili tushirikiane na wawekezaji wengine kuonyesha kwamba viwanda vya muhimu vinakuwepo katika nchi yetu, lazima tuamue vinginevyo kama wakati wote tunategemea matrekta ya kutoka nje, zana za kilimo kutoka nje na mbolea kutoka nje, mapinduzi ya kilimo tunayoyasema hayatafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, leo mbolea ya ruzuku wananchi wanunua kwa karibu shilingi 40,000, mwananchi gani maskini ambaye atamudu bei ya shilingi 40,000 na hapo ndiyo kuna ruzuku ya Serikali! Lakini bei ya mbolea, mfuko mmoja wa *DAP*, unauzwa kati ya shilingi 60,000 na 65,000, ni Watanzania wangapi watamudu bei hizo. Kwa hiyo, hapa lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba tunajenga viwanda vya mbolea, najua upo mpango wa kujenga Viwanda vya Mbolea kwa maana ya wawekezaji lakini mpango huo uharakishwe zaidi ili tuweze kwenda mbele na kuweza kupiga hatua. Hapo tukizungumza mapinduzi ya kilimo tunaweza tukawa na uhakika wa jambo ambalo tunalizungumza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alishazungumza na kwenye hotuba yake amerejea kuweka ruzuku kwenye mbolea ya kahawa yaani *CAN*, naomba Waziri wa Kilimo anapokuja kwenye bajeti yake basi atuhakikishie kwamba ahadi ya Rais imeshatimia kwa maana ya kwamba wananchi wanaozalisha kahawa kule Mbozi na maeneo mengine katika nchi hii wanawenza sasa wakapata mbolea yenye ruzuku ya Serikali ambayo wanaitumia kwa ajili ya uzalishaji wa kahawa. Maana mazao mengine yanapata ruzuku ya mbolea ambayo inatumika katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi pia maeneo mengine ya viwanda. Naomba niishauri Serikali ili mazao yetu mengine tunayozalisha yaweze kuwa na maana zaidi. Pia tujenge viwanda ambavyo vinaweza vikayafanya mazao yetu yaongezwe thamani ili yanapokwenda kwenye soko yaweze kutupatia fedha nyingi, kuliko kutoa mazao hapa nchini, tunapeleka nje ya nchi yakaongezwe thamani halafu

yarudi tena kwetu na wakati mwingine tunayanunua tena kwa bei kubwa zaidi. Kwa hiyo, naomba tuchukue hatua za makusudi ili tuwe na viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya mazao. Mathalani tunaweza kabisa tukajenga Kiwanda cha Kusafisha Tanzanite, tunaweza tukajenga viwanda vya kusafisha almasi katika nchi hii na tukifanya hivyo tutadhibiti hata haya madini ambayo tunazalisha hapa nchini. Lakini leo dhahabu inachimbwa, almasi inachimbwa na madini mengine yanakwenda kusafishwa au kuongezwa thamani katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mwendo huo nasema lazima Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda ambavyo vitafanya kwa manufaa ya Watanzania na Serikali, hapa hatuna namna. Kama tunataka kudhibiti uchumi wa nchi, lazima hatua hizo tuzichukue.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Benki ya Kilimo. Mheshimiwa Rais amezungumza kuanzisha Benki ya Kilimo, tumelizungumza muda mwingi, naomba Serikali na hasa Waziri anapokuja atueleze kwamba mipango ya kuanzisha benki ya kilimo inakwendaje.

Mheshimiwa Spika, tuna dirisha la kilimo kupitia *TIB*. Naomba niseme, dirisha la kilimo *TIB*, bado halijawanufaisha Watanzania walio wengi na hususan wakulima wadogo wadogo. Wakulima wote ambao wamekopa kutoka Mbozi mpaka ninavyosema leo sina hakika kama amefanikiwa hata mmoja mtu, masharti yake ni magumu, masharti hayawezekani na kwa maana hiyo ile benki kwa leo iko kwa ajili ya wakulima wakubwa katika nchi hii. Sasa wakulima wengi katika nchi hii ni wakulima wadogo wadogo na hawa ni zaidi ya asilimia 70 mpaka 80 ya wakulima wote katika nchi hii. Sasa kama masharti ya benki yataendelea kuwa yalivyo leo nina hakika dirisha la kilimo kupitia *TIB* itakuwa haina maana kwa wakulima wadogo katika nchi. Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue hatua za makusudi kwanza kupitia masharti, Mheshimiwa Waziri Mkuu kipindi fulani katika Bunge la Tisa lililopita aliahidi kwamba tunaangalia masharti upya ya benki hii ili wakulima wengi zaidi waweze kufaidika na benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nizungumze kwa sababu kengele imegonga, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 19 alizungumzia suala la kuendeleza mikakati ya kuanzisha kanda za kilimo na kuhamasisha kilimo cha mkataba. Tumeshalizungumza sana nchi yetu ina kanda tofauti tofauti na kuna kanda za kilimo, kanda za ufugaji, kanda za uvuvi na kanda zingine. Naomba niishauri Serikali na kama Mheshimiwa Rais alivyosema Serikali inapokuja na bajeti ijayo na kwa sababu Mheshimiwa Rais hapa alisema tunaanza mchakato basi Wizara zinazohusika katika maeneo hayo basi zije na mpango unaoelezwa katika bajeti tuone kwamba yale Mheshimiwa Rais aliyokuwa anazungumza sasa yanawekwa kwenye utekelezaji, vinginevyo hotuba ya Rais haitakuwa na maana, kwa sababu kama Mheshimiwa Rais ameyazungumza haya yakabaki kwenye maandishi hayatakuwa na maana hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda na kwa sababu nilisema nina mambo machache ya kuchangia basi naomba niseme, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais

na niiombe Serikali iendelee na utekelezaji wa yale ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, awali ya yote nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima, kunipa afya njema na kuniwezesha tena kuingia ndani ya Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Pia nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi na wanachama wa Wilaya ya Urambo, Mkoa wa Tabora kwa kunichagua na kuniwezesha kuwa mwakilishi wao na pia niwashukuru viongozi wangu wa Chama cha *CUF* Taifa kunituea kuweza kuwa mwakilishi wa Chama cha Wananchi *CUF* ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaahidi wote kwamba nitakuwa mwaminifu na utendaji mwema na nitawatumikia Watanzania wote kwa uaminifu mkubwa. Nakwenda moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais, nami nakwenda kwenye kipaumbele namba saba, Mheshimiwa Rais amezungumzia jinsi atakavyoweza kusaidia kuboresha ukusanyaji wa mapato katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa mara nyingi sana imekosa mipango ya uhakika ya kuweza kuwa na vyanzo vipyta vya mapato, tumekuwa mara zote tunategemea vyanzo vile vile, kwa hiyo, unakuta kwamba uchumi wetu na bajeti yetu inakuwa tegemezi miaka nenda miaka rudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni, Kambi ya Upinzani tumekuwa tunatoa ushauri na kuonyesha kuainisha kabisa vyanzo vipyta vya mapato, lakini vimekuwa havifatiliwa. Kwa hiyo, tunakuta kwamba kila siku vyanzo ni vilevile utakuta ni sigara inaongezwa ushuru, bia inaongezwa ushuru, lakini tuna vyanzo vingi sana ambavyo vinaachwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kukosekana miundombinu ya uhakika ya reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari kwenye mikoa iliyo pembezoni iliyo mipakani kama Kigoma, Tabora, Lindi, Tanga ni chanzo kikubwa sana cha kukosa mapato kwa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitaweka mipango makini ya kuhakikisha kwamba maeneo yote muhimu miundombinu inakuwa ya uhakika, barabara zinakuwa za uhakika, badala ya watu wanaotoka Malawi kwenda kutafuta nchi nyingine kupitisha biashara zao kama wanataka kupita barabarani apite Kigoma, aje Tabora aende Dar es Salaam. Kwa hiyo, tunapoteza mapato mengi kutoptana na kushindwa kuwa na miundombinu mizuri kwa ajili ya kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuwepo kwa ukiritimba kwenye bandari zetu. Kwa muda mrefu tumekuwa tunaongea, ukiritimba upo kwenye bandari, unaanza katika bandari kubwa ya Dar es Salaam na bado unaendelea kuwepo. Wafanyabiashara wengi

wanatumia bandari nyingine za Mombasa, wanatumia kwingineko na tunakosa mapato kwa kushindwa tu kusimamia bandari ifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna pia suala kubwa sana la uwepo wa mianya ya ukwepajji wa kodi, wafanyabiashara wakubwa hawalipi kodi, bandarini ipo, mizigo inapita, nina uhakika na ni taarifa za uhakika inapita bila kulipiwa kodi. Wanatumia njia za kona kona, ujanja na pia wanatumia rushwa kwa ajili ya kupitisha mizigo bila kulipiwa, nayo Serikali inakosa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima tuhakikishe kwamba tunaboresha sehemu zote muhimu, huko Serikali za Mitaa wanashindwa kukusanya mapato vizuri kwa kutokuwna na utaratibu unaotumika ambao umepitwa na wakati. Serikali za Mitaa wanatumia kukusanya kodi kwa kutumia risiti, Serikali za Mitaa hakuna watendaji waaminifu, kwa hiyo kukosekana kwa uaminifu wanachukua risiti wana *duplicate*, wanatoa fotokopi, wanakusanya mapato hawapeleki Serikalini kwa sababu wanatengeneza vitabu vyao. Ukiangalia vitabu vya CAG miaka iliyopita ameainisha kabisa anapokwenda kwenye ukaguzi unakuta Halmashauri nyingine vitabu havioneckani kabisa kwingine watendaji wanakimbia ofisi yote hayo ni kiasi kwamba pesa iliyokusanya haikuingia Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kuwa tumeendelea sasa hivi tumekuwa na hali nzuri tumeingia kwenye sayansi na teknolojia, wabuni utaratibu mpya utakaowawezesha kukusanya mapato kwa uhakika na yahakikishe kwamba yamefika Serikalini, Serikali za Mitaa, Serikali Kuu yaweze kusaidia wananchi wengi walio maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la Rais, ameainisha ana nia ya kuhakikisha kwamba anasaidia kuwepo kwa juhudhi za uhifadhi wa mazingira. Katika nchi yetu hali ya mazingira ni mbaya sana na kwa hali tuliyokuwa nayo sasa hivi nishati zote zimepanda, chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira katika nchi yetu ni matumizi ya mkaa yaliyopita kiasi. Asilimia 80 ya wananchi wanaoishi mijini wanatumia mkaa kwa sasa hivi, hata Wabunge wote hapa *almost* ni wachache wanaoweza kutumia nishati nyingine, kwani nishati imepanda.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia mwaka 2009, Serikali kwanza ilipunguza kodi kwenye gesi, ikapunguza kodi kwenye moto poa, ikapunguza kodi kwenye mafuta ya taa, kwa sababu iweze kusaidia wananchi waweze kutumia nishati hii na hivyo kuweza kupunguza matumizi ya mkaa. Lakini 2009 gesi ya kilo 15 ilikuwa 35,000 mpaka 38,000, leo ujazo ule ule kilogram 15 shilingi 48,000 mpaka 56,000. Kwa hiyo, wengi wamehama kutoka kwenye gesi, wamerudi kwenye mkaa. Tukiangalia mafuta ya taa yalikuwa 9,000 na 8,000, leo lita ni 1,280 mpaka 1,300 wengi wanashindwa kutumia. Moto poa kwanza umepanda bei, pia huwezi kupikia maharage yale maana asilimia kubwa tunakula maharage, inatuwia vigumu ule ni wa kupashia chakula huwezi kusema moto poa utamsaidia mwananchi wa hali ya chini wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, umeme, haushikiki, hakuna anayeweza kulipa gharama za umeme sasa hivi, umepanda kwa zaidi ya asilimia 62.3, sasa Serikali inawezaje kupambana kuweza kudhibiti mazingira wakati huo huo inashindwa kuanza na chanzo cha tatizo. Watanzania lazima wapike, Watanzania lazima wale vyakula vilivyoiva, wanakwenda kutumia *resources* gani? Kwa miaka kumi sasa tumekuwa tunasikia kwamba kuna makaa ya mawe Tanzania tena mengi, yapo wapi kwa nini yasije sokoni watu watumie?

Mheshimiwa Spika, mikaa inakatwa kwa kiasi kikubwa, ukipita barabara ya Morogoro Dodoma, ukienda Kilwa ni hatari, miti inayokatwa ni miti ya asili, mvua ni chache sasa hivi hata uotaji wa miti ya asili umekuwa mdogo na hakuna anayepanda, hata ukipanda huwezi kunyweshea miti ya asili wakati hata mahindi yenyewe yanakauka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali tusipokuja na nishati mbadala kwa kweli tunakaribisha jangwa, hakuna jinsi kwa sababu huwezi kuzuia wananchi watatumia nini. Naiomba sana Serikali ihakikishe kwamba imekuja na nishati mbadala na imepunguza gharama za nishati zilizopo, Serikali isinyamaze kimya, umeme unapanda wametulia, gesi inapanda wametulia, mafuta ya taa yanapanda wametulia, inasahau kwamba walaji wanaoumia ni Watanzania na hawana jinsi zaidi ya kutafuta nishati ambayo itawasaidia kwa ajili ya kuweza kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, suala lingine dogo ni suala la wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa kweli ninaguswa sana na jinsi ambavyo wafanyabiashara wadogo wadogo hasa mijini wanavyonyonyaswa na mgambo wa miji. Hawa ni Watanzania, hawa wana familia, wana watoto wao, wanatafuta riziki za watoto wao, hebu tuweke utaratibu. Unakuta hawa mgambo wa miji wamegeuza wafanyabiashara wadogo kuwa vitega uchumi, wanachukua rushwa kwa wale wafanyabiashara, wasipowapa rushwa wanawaburuza kwa namna ya ajabu sana. Unamkuta mwanamke amefunuliwa mpaka nguo yote, yuko uchi anapelekwa nguo yote ya ndani inaonekana mgambo wanaofanya kazi hii ni mgambo wa kike wakishirikiana na migambo wa kiume, huwezi kuamini kwamba hawa ni binadamu wenzao.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linauma sana, naomba sana akinamama hawa ambaa mitaji yao ni midogo, pengine ni shilingi 10,000 wanatembea kwa ajili ya kuza matunda madukani, hebu waandaliwe utaratibu utakaowawezesha na wenyewe pia waweze kupata riziki za watoto wao. (*Makofii*)

Suala lingine ni suala la Machinga *Complex*. Limejengwa sasa hivi ni karibu mwaka wa tatu, asilimia karibu 80 ya majengo yale hayafanyi kazi hayatumiki kwa sababu sehemu ilipojengwa walaji hawaji pale. Kwa hiyo, wameleta mazao yao pale, wameleta biashara zao lakini haziuziki. Matokeo yake wengine wamebaki kulala pale wanachukua biashara zao wengine wameamua kurudi mitaani kwa ajili ya kwenda kutafuta riziki.

Naomba Serikali ifanye utafiti ijue ni kwanini Wamachinga wamekataa kuhamia Machinga *Complex* na kifanyike nini ili kuhakikisha kwamba eneo lile linatumika kwa sababu limechukua mabilioni ya fedha na kwa nia njema kabisa Serikali ina nia njema. Lakini bila kuendelea kutumika tatizo litaendelea kuwepo na bado wafanyabiashara hawa wataendelea kunyanyasika kwa sababu huwezi kukaa mahali siku mbili, tatu hujauza wakati huo huo una mkopo unakusubiri, watoto hawajala, una mahitaji kibao, kwa kweli ni lazima utafute *other means* ya kupata maisha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Yangu ni hayo machache. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais, alikupongeza kwa kuteuliwa kwako kuwa Spika, na kwa kweli wote hapa ni mashahidi kwa jinsi unavyoimudu nafasi hiyo, maana kuanzia Jumanne uliumudu vizuri sana mchakamchaka wa humu ndani. Sasa tunakuomba kasi hiyo iendelee na wala usirudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho wa siku wananchi watatuuliza kuhusu masuala ya maji, barabara, zahanati na mambo mengine ya huduma kwao, sasa sijui kama mimi nitajibu kwamba kwa miaka mitano nilikuwa Bungeni nasimamia Kanuni! Wananchi hawatakula Kanuni. Ninheshimu sana Kanuni, lakini hatuwezi kuwa watumwa wa Kanuni. Kwa hiyo, ningeliomba sana wenzangu tuwe waangalifu, tuna nafasi ndogo sana. Tunapewa wiki mbili ambazo hazitoshi kabisa na ni bahati kusimama hapa kuzungumza, wengine hawatapata bahati.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba ndugu zangu Wanasheria, tunawaheshimu sana na taaluma zenu tunaziheshimu, lakini kama kila mmoja atakuja kutumia taaluma yake hapa kutuendesha mchakamchaka hatuwezi kuendelea. (*Makofi*)

Nawaomba sana, ni afadhali mrudi mka-*practice* kwenye *bench* kule, basi kwa sababu watu wanahitaji maji, barabara, wana shida zao, wana njaa, sasa hivi kama ingekuwa mjadala huu kutoka Jumanne tunazungumza habari ya njaa na mambo mengine, nadhani ingelikuwa tija kubwa sana. Kwa hiyo, ninadhani Kanuni zetu zinakidhi kabisa na zitatusaidia kutuongoza na tunawaomba sana wenye taaluma hiyo watusaidie watuongoze ili tuweze kusonga mbele vizuri na tuwalettee watu wetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi niko hapa nimerudi mara ya pili, naishukuru sana Serikali ya CCM kwa jinsi ilivyionongoza kwa mara ya kwanza. Wengi wenu ni mashahidi hapa jinsi nilivyokuwa nalalamika kuhusu eneo langu, nina Kilomita za Mraba 18,000, ilikuwa ni duni kabisa, nililalamika sana kuhusu masuala ya barabara lakini leo hii barabara zimefunguka. (*Makofi*)

Barabara ya Manyoni-Itigi kwenda mpaka Chaya Tabora inajengwa kwa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Mkiwa – Itigi kwenda Lungwa –Mbeya sasa hivi inashughulikiwa. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa John Magufuli, kwa kuanza kwa kasi kabisa na ninamwomba aendelee na kasi hiyo ili barabara hiyo iweze kukamilika mapema kama ilivyopangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umeme tulikuwa hatuna kwa maeneo mengine, ulikuwa umedumaa pale Itigi lakini Serikali imetusaidia umeme unasambazwa kwenda Mgandu (*Mgandu Triangle*), tayari nguzo zimesambazwa, na haya ni mafanikio. Nilikuwa sina Ofisi ya Jimbo, nilikuwa nafanya kazi Manyoni, lakini sasa hivi Ofisi ya Jimbo ipo Itigi. Tulikuwa hatuna Benki, sasa hivi tuna Benki, tulikuwa hatuna Sekondari za kutosha, zilikuwa mbili tu eneo lile lakini leo ziko 11, tisa tumeongeza, tulikuwa hatuna mitandao sasa hivi watu wetu wana minara na wana mitandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hatuna chakula mashulen, sasa hivi watoto wetu wanakula wanashiba vizuri na wana-*concretate* katika masomo. Tulikuwa hatuna mambo mengine, juzi tumepata Kambi ya Kujenga Taifa. Serikali imeridhia kwamba niweze kupata Kambi ya Kujenga Taifa Jimboni kwangu, nashukuru sana. Sasa haya ndiyo mafanikio. Watu wanasema Serikali ya Awamu ya Nne haijafanya kazi, mambo haya niliyoordhesha mimi nimeyaona jimboni kwangu. Siko hapa kuzungumzia masuala ya Jimbo la mtu mwingine, mimi ninazungumzia Serikali imefanya nini katika jimbo langu. Naishukuru sana.

Mheshimiwa Spika, katika mafanikio hayo basi, niwashukuru wananchi wa Jimbo langu kwa kuona hayo na mwishoni wakaamua kunirudisha, na ninadhani watanipa imani hiyo niweze kufanya kazi yangu kwa ushirikiano pamoja nao ili tuweze kumaliza miaka mitano hii vizuri. Haikuwa rahisi kwa kila mmoja, kama huku-*perform* mahali popote walikuwa wanakwambia ‘no way’ na ushahidi ni kwamba tulikuwa wengi lakini tumerudi wachache ingawa wengine wa CCM nao walifanikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika vipaumbele vya Rais katika hotuba yake, ningombwa nizungumzie suala la Reli. Reli hii ya kutoka Dar es Salaam – Tabora – Kigoma, najua kwamba kuna kazi ‘*feasibility study*’ imeishafanyika kuihuisha hii Reli kati ya Dar es Salaam – Tabora na Isaka kwenda Mwanza, na tatizo linalosemekana sasa hivi ni *funding*.

Mheshimiwa Spika, ningombwa Serikali ijaribu kuliona hili tatizo. Reli ni muhimili muhimu sana kwenye suala la uchumi, kwa hiyo, ningeliomba hilo liangaliwe, *funding* iweze kupatikana mapema ili angalau ikifika miaka mitano, hili tatizo liwe limeshaondoka. Maeneo hayo ya kwetu sisi tuliishi kando kando ya reli hivyo tunajua maana yake. Hii ni utamaduni wetu, ilikuwa ndiyo inatuingizia uchumi wetu na mtu wa Itigi na maeneo mengine ya Tabora, Kigoma huwezi ukamwambia lolote bila reli. Kwa hiyo, ningeliomba Serikali iweze kulishughulikia suala hili haraka ili tuweze kuondokana nalo.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa demokrasia, naomba Serikali ijaribu kushirkiana na Bunge hili iweze kuliimarisha Bunge kwa maana ya fedha. Maana tunaposema tuimarishe demokrasia, huu ni mhimili na wala siyo Idara ya Serikali. Kwa hiyo, naomba kama kuna uwezekano, basi iwekwe katika mfuko maalum wa matumizi (*Consolidated Fund Services*) ili iweze kuwa na fungu lake la uhakika.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na matatizo kwamba mara nyingine tunakuja tunaambiwa tunakaa wiki tatu *then* unakuja unaambiwa unakaa wiki mbili. Nini tatizo? Fedha. Sasa naomba sana hili tatizo liweze kuangaliwa walirekebishe sisi tuweze kufanya kazi zetu vizuri kwa utulivu. Hatuombi fedha za bure, lakini tunaomba pale ambapo taratibu zimebekwa, basi zifuatwe ili watu wengi waweze kuchangia. Ndugu yangu Mheshimiwa Godfrey Zambi juzi alisema hapa, tuna maswali mengi katika Bunge lililopita ambayo hayakujibiwa, nayo ni kwa sababu ya muda, hakuna muda hakuna pesa, kwa hiyo, naomba hili liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, watu wetu wengi mwezi Oktoba hawakutoka kwenda kupiga kura, ni 42% tu waliotoka kwencda kupiga kura. Sababu watu wameeleza ooh, wameichoka Serikali. Sio kweli, sababu mojawapo kubwa ni watu kuwa *laser fair* tu, basi. Mtu siku ya kwenda kupiga kura anaamua kwenda kufanya mambo yake, sisi Wataturu, Wabarabaigi kule unatoka kwenda kuchunga ng'ombe wako, kwenda kuangalia maji na nini.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri uletwe Muswada hapa, basi tutunge sheria kwamba iwe ni lazima mtu kwenda kupiga kura. Kuna nchi kama Australia wana Sheria hiyo, usipokwenda kupiga kura, basi upewe miezi sita uende Chuo cha Mafunzo kule ukajaribu kuzalisha mali ujue wajibu wako, maana wengine wanakataa wajibu wao. Naomba tulitazame hili, tusilete visingizio kwamba watu hawaitaki Serikali, hawafanyi nini, wengine hawawezi wajibu wao bila kuelekezwa. Kwa hiyo, naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningeliomba katika hivi vigezo....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini la pili sina budi kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu na ninawataki kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake. Ni hotuba nzuri na inafahamika, hotuba hii siyo ya Wabunge tu, ni hotuba ya Watanzania wote, kila mmoja ana haki ya kuijadili na kutoa mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, mimi ni vyema niende katika kipaumbele cha kwanza kinachozungumzia amani, utulivu na Muungano wetu. Mheshimiwa Habib Mnyaa

ameeleza zaidi kuhusiana na dhana nzima ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nasema kwamba, katika Bunge la Tisa, Mheshimiwa Rais aliona hali hii tete ya kisiasa Zanzibar na akaahidi kutafuta ufumbuzi kwa kushirikiana na viongozi wa siasa kule Zanzibar na bahati alifanikiwa sasa Zanzibar iko tulivu, wananchi wanaelewana, wanafanya kazi pamoja bila bughudha yoyote, wanachangia Taifa lao na maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa sana kwa baadhi ya Waheshimiwa kuubeza umoja wetu. Nashangaa kwa sababu ni sawasawa na mtu anakwenda Dar es Salaam, akaambiwa aingie kwenye gari, yeche akasema atakwenda kwa mguu, kwa hiyo nitamshangaa sana. Niseme kwamba, Serikali ya Zanzibar chini ya Ibara ya 102 ina mamlaka yake. Zanzibar wenyewe ni Wazanzibari wana haki ya kuamua ni aina gani ya Serikali wanayoitaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Zanzibar ni ya Wazanzibar wenyewe, wana haki ya kuamua kubadili vifungu vya Katiba au kuiandika upya. Wazanzibari wameamua kwa 64.2% kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Hakuna hata mmoja awe wa ndani au wa nje ambaye anaweza kubadili maamuzi ya Wazanzibar. Tutaendelea kuheshimu Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa gharama yoyote ile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii sina budi kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa juhudili kubwa alizozifanya ili kufika hapa alipofikia sasa. Pia sina budi kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Aman Abeid Aman Karume, lakini pia sina budi kumpongeza kwa dhati kabisa Katibu wangu Mkuu wa Chama cha Wananchi (*CUF*) na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar, Maalim Seif Shariff Hamadi. Wote nawatakia umri mrefu na maisha bora. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, sasa niende katika ukurasa wa ishirini na nne kuhusu ukuzaji wa ajira Tanzania. Naelewa kwamba ziko Wizara zinatoa ajira, yako makampuni binafsi yanatoa ajira, viko viwanda vinatoa ajira na ziko sekta binafsi zinatoa ajira, lakini ni ukwerli usiopingika kwamba ajira ni chache Tanzania. Ajira ndiyo inayoleta heshima ya mwanadamu na kama huna ajira basi huna heshima, utakuwa ni omnia omba tu. Hata kule nyumbani kutakuwa hakuna amani.

Mheshimiwa Spika, bado ajira ni chache, yako makundi ya vijana ambao wanamaliza sekondari kila mwaka, yako makundi ya vyuo vikuu hawa ni watalaam, hawa wanamaliza vyuo kila mwaka na wako wale ambao wanashindwa kuendelea na masomo yao, nao wanamaliza kila mwaka. Kwa hiyo, wengine wanaamua kuihama nchi yao kwa sababu ya ajira. Tunawasomesha kwa gharama kubwa ya Serikali lakini hatimaye wanakwenda kutumikia Mataifa mengine, ni kwa sababu hakuna ajira. Wengine wanaamua kufanya biashara ya madawa ya kulevyia ambayo ni hatari kabisa, lakini wengine wanaamua kujiunga na uhalifu. Hii ni kwa sababu ya ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini kama si hivyo wengine wanaamua kufanya biashara ya ukahaba. Ukienda Dar es Salaam kuna watoto wanaomba omnia njiani, ni watu

wamekwenda kufanya biashara zao na wana Wazee wao wale wanawatuma kwenda kuomba. Hili Taifa tunalipeleka wapi? Litakuwa ni Taifa hatari kabisa, tutaliangamiza hivyo, ni lazima Wizara inayohusika ihakikishe kwamba suala hili tunalivalia njuga na kuongeza ajira ziwe nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwamba wanafunzi wetu wa vyuo vikuu kila siku wanaandamana. Wanafunzi ambao tunategemea waje kuwa Wabunge, kuendeleza Taifa hili, lakini kila siku kuna maandamano. Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya kuchunguza migomo. Naomba litakapopatikana jibu sahihi basi huu mgomo uweze kukomeshwa kabisa. Kwani watu hawalipwi? Wanalipwa shilingi 5,000/=, hii ni pesa kidogo sana. Hebu tumlipe Mbunge hapa shilingi 5,000/= ataishije hapa? Hawa wanasoma, wanunua vitabu, wanafanya shughuli mbalimbali, leo unawalipa shilingi 5,000/=? Kwa hiyo, tunaomba Wizara husika iliangalie kwa makini suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni mara yangu ya kwanza katika Bunge lako Tukufu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote niwashukuru kwanza wapiga kura wa Jimbo langu la Lindi Mjini, wamenipa heshima kubwa, heshima ya kihistoria, pamoja na heshima yangu lakini pia na heshima ya Jimbo la Lindi Mjini. Ni mara ya kwanza katika historia ya nchi hii, Mlemauv ambaye ametokana na kura za wapiga kura wenyewe, hili limeleta heshima katika Taifa letu. (*Makofi*)

SPIKA: Naona kama unasoma, hatusomi.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa familia yangu na wale wote ambao waliniunga mkono katika harakati zangu zote za kisasa. Pia niwashukuru viongozi wangu wa chama ambao wamenipa malezi mazuri mpaka kufika hapa nilipofikia leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja nianze hoja yangu juu ya suala zima la hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwanza katika hili nimpongeze, ni hotuba nzuri, hotuba ambayo imeja matumaini makubwa. Lakini katika yote nianze katika neno moja muhimu sana, tangu tumefika katika Bunge hili hapa la Kumi bado inaonekana kwamba hoja ya amani ni hoja ya kundi dogo la watu. Inaaminika kabisa kwamba tunazungumzia suala la amani, inaonekana kwamba suala la amani ni vitisho kwa Watanzania, kwamba Watanzania wakae katika tahadhari juu ya amani, lakini suala zima la amani halipo katika watu wachache tu, suala la amani ni la Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la amani lichukuliwe kama ni ajenda katika kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maendeleo yao. Taifa hili lina miaka 50 ya uhuru (makumi matano), nusu karne, amani hii imetumikaje katika kuwaletea maendeleo

Watanzania? Kwa miaka 50 ya uhuru ambayo tayari tunayo, haikuwa sahihi kwenda kuomba kura kwa Mtanzania eti kwa ahadi ya maji! Miaka 50 ya uhuru bado tunakaa tunazungumzia habari ya amani, amani, Watanzania wana matatizo chungu nzima, wanatarajia Bunge hili likae, litatue matatizo ya msingi ambayo Watanzania wanakabiliana nayo. Miaka 50 ya uhuru tunashuhudia jinsi gani mgawanyo wa rasilimali unavyojenga matabaka katika Taifa letu. Tunaona jinsi gani mauaji katika nchi hii yanavyoendeshwa ni kwa sababu bado Serikali hajajipanga katika kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi yetu zinawafikia watu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, suala zima la Upinzani, tayari imejengeka kwamba Upinzani ni uadui katika Taifa, hii ndio dhana ambayo imejengeka katika Taifa letu. Upinzani si uadui, ni utaratibu wa kistaarabu wa kugawana madaraka katika Taifa. Leo nchi ambazo zinatufadhili, nchi ambazo zinatusaidia duniani kote, chukua mfano Amerika, wapo ndani ya demokrasia ya Vyama Vingi zaidi ya miaka 200 na ndio Taifa kubwa na tajiri duniani. Ni utaratibu wa kistaarabu kabisa kugawana madaraka katika Taifa na utaratibu ambao tayari unajenga amani katika dunia kwa sababu watu wanasubiri tu baada ya miaka mitano sera zako zimetekelezwa kwa kiasi gani. Ni utaratibu wa kistaarabu, ni utaratibu wa kiungwana kabisa. Isifikiwe kwamba kukubalika kwa Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa katika Taifa letu basi tayari ni uadui mkubwa. Tujaribu kujenga taratibu maalum, tuwaelekeze Watanzania kwamba suala zima la kuwepo kwa Mfumo wa Vyama Vingi katika Taifa letu, ni utaratibu wa kiungwana. Tunabadilishana madaraka, wananchi wanapewa mamlaka ya kufanya lile ambalo wao wanaona kwamba kwa kufanya hivi ndiko kutawaleeta maendeleo katika Taifa letu.

(Hapa Mzungumzaji alikuwa akisoma hotuba yake)

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge kusoma ni marufuku.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, nizungumzie mgawanyo wa rasilimali katika nchi. Imeonekana katika nchi yetu ...

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Uko wapi?

MBUNGE FULANI: Mimi hapa.

SPIKA: Simama sijakuona, haya samahani sana.

MBUNGE FULANI: Okay.

Mheshimiwa Spika, ni kuhusu Mheshimiwa aliyekuwa anazungumza, Mheshimiwa anasoma ni kwa sababu ni mwenye ulemavu, mwenye uono hafifu, kwa

hiyo ameandika *points* zake, anasoma tu *points* lakini maelezo anaeleza. Kwa hiyo, naomba apewe nafasi ya kushika karatasi yake. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa, nakushukuru sana kwa kusema hivyo lakini ndio maana hasomi, ingekuwa anasoma *argument* yako ingekuwa kweli kwamba macho hayaoni anashindwa kusoma, ndio maana tunasema asisome. (*Makofi*)

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, utaniongeza muda wangu kidogo.

SPIKA: Sawasawa.

MHE. SALUM K. BARWANY: Mheshimiwa Spika, nafasi ya mgawanyo wa rasilimali katika nchi yetu tayari imeonekana kwamba maeneo mengi katika nchi hii ni wachangiaji wakubwa katika pato la Taifa letu lakini ni kwa namna gani katika maeneo hayo wananaufaika na rasilimali hizo? Ni mpango gani ambao Serikali umeuandaa kuhakikisha kwamba rasilimali za nchi yetu zinatoa maslahi katika maeneo husika?

Mheshimiwa Spika, leo katika maeneo ya Mikoa ya Kusini, tayari kuna rasilimali za kutosha, tuna gesi ya Songosongo, kuna gesi ya Mnazibay, ni rasilimali ya kutosha kwa maendeleo ya watu wa Kusini. Tuna *gypsum* ambayo tayari inatengeneza saruji lakini maeneo yale yako nyuma katika sekta zote kwa sababu uchumi wake uko chini katika sekta zote, nenda katika sekta ya afya, elimu ni maeneo ambayo yako nyuma.

Mheshimiwa Spika, jana hapa kumezungumzwa katika Bunge lako Tukufu kwamba kuna Hospitali za Rufaa katika nchi yetu na yameelezwa maeneo ambako hospitali hizo zipo lakini haikuonyeshwa kwamba Kusini Hospitali ya Rufaa iko wapi? Katika sekta ya elimu imezungumzwa hapa kuna Vyuo Vikuu Dar es Salaam, Iringa, Morogoro, Dodoma na katika maeneo mbalimbali lakini baada ya miaka 50 ya uhuru wetu bado hatujaona maendeleo ya elimu katika maeneo ya Kusini. Hii ni kuonyesha kwamba pamoja na rasilimali zilizokithiri katika maeneo yale lakini bado wananchi wa Mikoa ya Kusini hawajanufaika na rasilimali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ambayo tayari Mheshimiwa Rais ameeleza, kusimamia na kugawanya rasilimali katika nchi, Bunge hili la Kumi, safari hii lihakikishe kwamba linapeleka maendeleo katika Mikoa ya Kusini. Hii itasaidia kujenga Umoja wa Kitaifa na itasaidia kuleta amani katika nchi yetu. Yale maeneo ambako sasa hivi kuna migogoro katika nchi nyingi ni kutokana na kukosekana kwa mgawanyo rasmi wa rasilimali katika nchi zao. Chukulia leo Sudan ya Kusini na sehemu zingine, ukiangalia ni sababu za kiuchumi hasa ambazo zinapelekea kutokuwa na amani katika nchi zao. Hivyo Bunge letu hili lihakikishe kwamba linajenga utulivu ndani ya Bunge hili kwanza kama Wabunge, ningetarajia Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wamsaidie Rais na sisi Wabunge ambao sio wa Chama hicho, tutakuwa tayari kumsaidia Rais katika kuhakikisha kwamba mipango ambayo ameisimamia, tumeisimamia sote kwa pamoja. Kwa sasa

inaonekana dhahiri tayari kuna mgawanyiko ndani ya Mawaziri, ndani ya Bunge, sasa sisi Wabunge ambao hatupo ndani ya Chama, tunapata maelekezo kutoka wapi?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanatutazama huko, mamilioni ya Watanzania wenye matatizo ya msingi wanajiuliza, je, Bunge letu linafanyaje, Bunge letu linazungumza nini juu ya hali ya maisha yetu. Watanzania ni maskini, umaskini wa Watanzania umekithiri. Tunazungumzia hapa habari ya njaa, miaka 50 ya uhuru Watanzania leo hawana hakika ya kula kwa siku ya leo. Hivyo wana matarajio makubwa Watanzania na sisi kuhakikisha kwamba tunaisimamia Serikali, tunaielekeza Serikali na ndio wajibu wetu sisi kama Wabunge, hatukuja hapa na Vyama vyetu, kazi ya Chama imemalizika kule juu, Watanzania wametuleta hapa kama Wabunge kwa ajili ya utetezi wa maisha yao. Hivyo, suala zima la kusema kwamba mimi *CUF*, CHADEMA, CCM halitopata nafasi katika Bunge hili. Hivyo, ni vyema sasa tukawahakikishia kwamba tupo hapa kwa ajili yao.

Mheshimiwa Spika, mimi nimepigiwa kura Lindi sio na Wanachama wangu tu, naamini nyote pia, Wanachama wa Vyama vya Siasa wako wangapi, ni wachache. Watanzania sasa wameondokana na dhana ya Vyama vya Siasa, Watanzania wanaangalia nani anaweza kuwalettea maendeleo na ndio msimamo uliopo sasa hivi huko nje, hivyo tunawashangaza, tunawastaajabisha kwamba tuko nje ya dhamira ya Watanzania. Tuongoze katika Bunge lako, tumia Kanuni, Taratibu ili kukidhi matakwa ya Watanzania leo. Hali si nzuri, matokeo ya mtihani wa shule za msingi na sekondari ni mabaya, ni Taifa la kesho lile. Tunawaandaje na Serikali tunaisukumaje kusimamia maendeleo ya elimu katika nchi yetu? Tunasimamia vipi vijana ambao leo wapo vijiweni, vijana wanavuta bhangi huko, wamekosa mwelekeo wamekata tamaa ndani ya Taifa lao, tuzingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, nina hoja nzito kabisa, tuweke picha hapa mbele yetu sasa itakayoonyesha taswira ya Mtanzania ambaye tunamsemea kuonyesha yukoje kule nje ambao tumekuja hapa kwa ajili yao. Watanzania wanateseka huko nje, mauaji ya Albino ambayo tayari yametuletea aibu katika Taifa letu, yalipoteza maisha ya watu wengi sio kwamba Albino wameathirika katika mauaji yale, Albino amezaliwa na wazazi na wazazi ndio wameathirika, wengine walikuwa ni tegemeo kwa watu wale. Haya yote Bunge linatakiwa likae katika Bunge la Kumi, litengeneze mazingira bora, miaka 50 ya uhuru sio kipindi kidogo kama kweli tuna dhamira ya kuleta maendeleo. Nchi zingine ambazo leo wanatufadhili hapa ni miaka 10 tu baada ya uhuru wao wameendelea, walichagua mambo, wakayapa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante, nitaanza kuitumia vizuri Kanuni ya 63, mkaisome wote mtaona itakavyofanya kazi yake. Mheshimiwa Masele!

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii, kuwashukuru sana wananchi wa Shinyanga kwa kunichagua kwa kura nyingi. Napenda nichukue nafasi hii kuweka rekodi sawasawa, nilishinda kwa kura nyingi na sio kura moja kama inavyoripotiwa na vyombo nya habari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri. Mheshimiwa Rais wote tunamfahamu, ni mtu makini, mtu mwenye huruma, ni msikivu na mzalendo kwa nchi yake.

Aidha, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais, kwa kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria ambapo sasa hivi wananchi wa Shinyanga wana uhakika wa maji safi na salama. Lakini pia shukrani hizi nizifikishe kwa Wizara ya Maji hususan Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mwandosya, kwa kazi kubwa na mikakati ambayo anaifanya kuhakikisha maji hayo yanawafikia wakazi wengi wa Shinyanga maeneo ya Kolandoto, Ibadakuli, Mwamalili na Mwawaza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza miradi mikubwa mitatu ya umwagiliaji katika Manispaa ya Shinyanga, lakini miradi hii inategemea maji ya mito ambayo si ya kudumu ni mito ya muda. Naomba niishauri Serikali itenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya uvunaji wa maji haya ili yaweze kutumika pindi ambako mvua hazinyeshi na kufanya hivyo itawezesha wananchi wa Shinyanga kuweza kulima katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika eneo la ardhi. Kuna dhuluma kubwa sana inafanyika katika ardhi. Wananchi wanyonge wasio na uwezo wanadhulumiwa haki yao. Wananchi wa Shinyanga leo hii kama Serikali haitachukua hatua za haraka, itatokea shida kubwa ya amani katika Manispaa ya Shinyanga kwa sababu ya dhuluma ya ardhi. Kweli ardhi inapimwa lakini Sheria hazifuatwi na mwenye ardhi ya mwanzo hapati haki ya kupewa, wanapewa watu wengine wenye nafasi. Bahati mbaya zaidi unakuta eneo moja linagawiwa kwa watu wawili mpaka watatu. Namwomba Waziri wa Ardhi afanye bidii ya kufika Shinyanga ili kuweza kusaidia kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pia zipo nyumba zinazomilikiwa na Halmalshauri zetu ambazo kimsingi nyumba hizi zimechakaa sana na watu wale wanashindwa kufanya ukarabati wa nyumba hizo kwa sababu hawana kibali cha kufanya vile. Naomba Serikali ifikirie uamuzi wa kuwauzia wananchi wale ili waweze kuzimiliki na kuweza kuziendeleza kwa maana ya kuzifanya ukarabati mkubwa. Yako maeneo kama ya Majengo katika Jimbo la Shinyanga, wakazi wengi wanaishi kwenye nyumba hizo ambazo zimechakaa na wangependa kuziendeleza kwa kuzifanya ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa natoka katika eneo la wakulima wa pamba na uchumi wetu wakazi wa Shinyanga kwa ujumla na Kanda ya Ziwa, tunategemea zao la pamba, lipo tatizo haswa kwenye bei za pamba, tumeshuhudia mwaka jana bei ya pamba ilianguka sana kwenye soko la dunia. Naomba niishauri Serikali iweke mkakati wa kutunga sheria ambayo itawalinda wakulima wetu. Tuwe na *export ban* ili inapotokea zao la pamba linaanguka na tunashuhudia sasa hivi mvua zetu zimekuwa si za uhakika

basi Serikali iweze kutumia *tool* hiyo kuweza kuwalinda wakulima na kuweza kulinda viwanda vyetu vya ndani kwa maana ya soko zima la ndani. Leo hii tunashuhudia wafanyabiashara wetu wa pamba wanashktakiwa na wanunuzi wa nje. Lakini hii yote inatokana na kwamba hali ya hewa si nzuri na wameshindwa kupeleka mazao kadri walivyosaini mikataba ile. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kutunga sheria ambayo itawezesha Wizara na Waziri kuweza kuzuia uuzaaji wa mazao nje pale inapotokea kwamba kuna uzalishaji mdogo wa zao la pamba. Ziko nchi ambazo zinafanya hivyo na zimefanikiwa kwa mfano Ethiopia na imefanikiwa kuwalinda wakulima, kuwalinda wafanyabiashara kwa maana ya *investors* katika nchi zao, Ethiopia na India wamefanikiwa katika hili.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusiana na *powertiller*. Ni kweli Serikali imeingia kwenye mradi huo wa *powertiller* lakini naomba Wizara ifanye tafiti za kutosha inapofikiria kupeleka *powertiller* mahali fulani, iangalie je, chombo hiki kitaweza kufanya kazi kulingana na mazingira yale. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Shinyanga hakuna *powertiller* hata moja ambayo imeweza kuleta tija katika kilimo. Ng'ombe anayekokota jembe la plau, ng'ombe wanne wanalima kwa eneo kubwa kuliko *powertiller*. Kwa hiyo, naiomba Serikali inapofikiria kupeleka miradi hii, ifanye tafiti kuona kwamba ardhi ya Shinyanga na chombo hiki tunachokipeleka, je, kitaweza kuzalisha?

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye suala la ajira. Ni kweli kuna Makampuni mengi ya uwekezaji hapa nchini, lakini Serikali imezembea katika kudhibiti ajira za wageni wanaokuja kupora ajira za wazawa. Leo hii wako watu wanatoka Paraguay, Mexico wanakuja kufanya kazi ya *Customer Service Manager* ambapo kazi hii ingefanywa na Mtanzania. Naomba Serikali izipitie upya sheria zake na kufanya maamuzi pale inapotokea kwamba sheria hizi zinakiukwa. Leo Watanzania wengi wanakosa ajira na wana sifa na uwezo wa kufanya kazi ambazo zimechukuliwa na wageni ambaa hawastahili kufanya kazi zile.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali katika kutatua tatizo la ajira, iwekeze katika vyuo vyetu hasa Chuo cha Sokoine. Pale wataalam wengi wanatoka, haya mabilioni tunayoyazungumzia, mabilioni ya Kikwete yangeelekezwa pale na vyuo vile vikapewa mamlaka ya kusimamia vikundi vya wataalamu wanaomaliza na kuhitimu katika vyuo vile ili waweze kwenda kujikita kwenye kilimo kwa kusimamia kwa kuwa wana ujuzi, nina hakika nchi yetu itajikomboa na tatizo la njaa na tutaweza kuzalisha chakula cha ndani na hata chakula cha kuweza kuuza nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwenye eneo la bandari. Ni kweli Bunge la Tisa lilijadili ufanisi wa Kampuni inayoshughulika na upakuaji wa Makontena, lakini naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba tatizo lingine linajitokeza la urasimu hasa katika Kitengo cha Forodha katika bandari zetu. Urasimu huu umekuwa unachangia ucheleweshaji mkubwa wa utoaji wa mizigo katika bandari yetu na kusababisha usumbu mkubwa kwa wafanyabiashara wetu. Mwisho wa siku wafanyabiashara wanatozwa faini (*storage charges*) kwa kuchelewesha kutoa mizigo yao katika bandari kwa kosa ambalo wao hawajalifanya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu ananunua kontena lake China, analipia, yeye anataka lifike Mwanza, linafika Dar es Salaam linakaa pale baadaye anaanza kutozwa *storage charge* na ameshalipia kila kitu. Naomba Serikali iangalie kwa umakini katika eneo hilo na inatoka mpaka mizigo mingine ya misaada. Kwa mfano, nimepata misaada ya kutoka Sweden ya hospitali yangu ya Kolandoto, kontena lile mipango yote imekamilika, *documents* zote zimepita lakini limekaa zaidi ya wiki mbili bila kutoka na ukienda pale wanakwambia *storage charges*.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie kwa umakini urasimu huu unaotoka katika bandari yetu na unasababisha wafanyabiashara wetu wengi sasa wanaikwepa. Sasa hivi kundi kubwa la wafanyabiashara wa magari na wafanyabiashara mbalimbali wanatumia bandari ya Mombasa wanaacha kutumia bandari ya Dar es Salaam na Serikali inapoteza mapato mengi kwa sababu ya urasimu ambao tunausababisha wenyewe. Ziko bandari za nchi kavu kwa mfano pale Isaka, kwa nini Serikali ikusanye mambo yote yafanyike Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iweze kutumia maeneo mengine Kikanda, kama mtu analipia mizigo kufika Shinyanga anaweza kwenda kufanya *clearance* zake zote Isaka. Kama mtu anapeleka mizigo wake Mwanza, atumie eneo la Sirari ama na maeneo mengine kama Kanda za Nyanda za Juu, kwa kufanya hivyo, itatusaidia kuupunguza urasimu huu.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la elimu, napenda kuchangia eneo dogo tu, kwamba Serikali kupitia Halmashauri ambazo zimepewa mamlaka ya kusimamia Walimu katika Halmashauri zetu, iangalie suala la mgawanyo wa Walimu. Leo hii Walimu wanapangiwa kwenye Shule zetu za Kata za vijijini lakini hawaendi kuripoti. Unakuta Mwalimu anayekaa mjini anafundisha masomo mawili, lakini Mwalimu kama huyo huyo kwenye Shule zetu za Kata za vijijini anafundisha masomo 10, hapo tusitegemee vijana wetu kwenye Shule zetu za Kata watafanya vizuri. Walimu wapo lakini ugawanyaji wa Walimu hao hausimamiwi vizuri na wengine wakipangiwa kwenye zile shule wanakwenda lakini baada ya muda wanafanya mipango yao wanarudi kwenye shule za mjini. Naishauri Serikali kupitia Halmashauri zetu, isimamie kwa umakini zoezi la ugawanyaji wa Walimu ili kuweza kupata uwiano sahihi katika Shule zetu za Kata zilizoko vijijini na Shule zetu za Kata zilizoko mijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na ni mara yangu ya kwanza, ni vizuri nikupongeze kwa kuwa Spika lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Kigoma kwa heshima kubwa waliyonipa na hakika sitowaangusha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, leo tunajadili Hotuba ya Rais. Ukiisoma hotuba hii, *page* ya kwanza mpaka ya mwisho, unaona Rais wetu alivyo na *vision* kubwa ya kutaka nchi yetu

iende mahala pa kubwa kimaendeleo lakini kwa sababu ya muda, siwezi kuyaeleza yote lakini yako machache hasa kipengele cha pili, cha tatu, cha nne, cha tano na sita, kwa kweli vinashabihiana sana.

Mheshimiwa Spika, wakati naangalia, naijiliza, unaona, ili tuweze kuendelea kiuchumi tunahitaji sasa na kwa haraka maneno haya mazuri tuyaingize kwenye utekelezaji. Mimi ninaloliona hapa ni kwenye utekelezaji zaidi. Ukiona namba mbili mpaka namba tatu, tunaongelea namna ya kukuza uchumi, injini ya *growth* ni ya *private sector*, ili tuweze kuleta *investment in the country*, yote haya ndiyo yanayoongelewa na ili uchumi wetu uweze kukua.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo ambayo lazima tuulizane vizuri. Ukiangalia katika nchi zetu za chini ya Jangwa la Sahara, gharama za kufanya biashara Tanzania ni kubwa sana. Kwa hiyo, maana yake kama mnashindania *investor* wachache, ni wachache sana watakaokuja kwetu kwa sababu gharama za kufanya biashara ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naijiliza kwa mfano leo mtu wa kawaida, wa kati anataka kuandikisha biashara, anatumia muda gani? Ukienda Rwanda mwaka 2007, ilikuwa unatumia siku 38 kuandikisha biashara lakini wamefanya juhudhi leo wanatumia chini ya masaa nane. Kwa hiyo, unaweza ukaona mtu anayetaka kufanya biashara ataenda huko kwa sababu kwanza kwenye kuandikisha biashara peke yake hakuna urasimu. Kwa hiyo, naomba wenzetu wa Serikali angalau tuanzie hapo. Tunasema tunataka watu wafanye biashara, *SACCOs*, vituo vyote hivi ili watu waweze kufanya biashara, cha kwanza tuandikishe biashara, je, ukitaka kuandikisha biashara unatumia muda gani? Hilo ni la kwanza lazima tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiandikisha biashara kinachofuata ni nini? Tuna tatizo la mitaji maana yake sasa unaingiza mabenki yetu lakini mabenki kama tunavyoambiwa kila siku sio marafiki wazuri sana wa maskini. Kwa vile tayari umeandikisha biashara yako unakopesheka lakini ili uweze kukopesheka lazima uwe na dhamana, unafanyaje? Ili uweze kuwa na dhamana nasema Serikali imefika wakati Mungu ametujalia Tanzania, tuna ardhi kubwa sana na naomba Waziri wa Ardhi katika hili atusaidie. Rwanda ni nchi ndogo lakini wamefanya, wamei-map nchi yote kila mtu mwenye ardhi anayoi-own amepewa *Title Deeds*. Maana yake ni nini? Ukipakuwa na ile *Title Deeds* ni rahisi sasa wewe kwenda kukopesheka kwenye mabenki. Maana yake ni nini? *Confidence* ya *Bankers* itaongezeka na ikishaongezeka maana yake watakopesha watu wengi wataweza kufanya biashara, watatoa ajira na wakitoa ajira maana yake tumetatua tatizo lingine la upatikanaji wa kazi na tutaweza kukusanya kodi kwa kiasi kikubwa, kwa kufanya hivyo, uchumi wa nchi yetu utakua, naomba wenzetu hili tusiliangalie kwamba haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, nimeandikisha biashara, tayari mabenki yapo, tayari kila mtu mwenye ardhi ana-*Title Deed* yake, liko jambo lingine ambalo ni *serious* na ni la *judiciary*. Lazima tuhangaike nalo, kesi zetu zinachelewa sana. Mabenki yangejua kama mtu ame-default mkienda Mahakamani jambo hilo linaamuliwa kwa muda mfupi ingesaidia lakini leo mtu amekopa, amekataa kulipa, shauri limeenda Mahakamani

linakaa miaka mitano, maana yake ni nini? Mabenki yata-*loose interest* na matokeo yake *interest* za Tanzania zitapanda siku zote kwa sababu kuna *element* ya *risk* imewekwa huko ndani.

Mheshimiwa Spika, ili uchumi wa nchi yoyote uweze kukua na watu wote waone kweli uchumi wa nchi umekua, maana leo iko *scenario* ukiwaambia watu wa kawaida uchumi umekua wakati bei ya sembe imepanda, bei ya nyama imepanda, bei ya mafuta imepanda, bei ya kauzu Kigoma imepanda, hakuna anayeweza kuelewa. Kwa hiyo, lazima tuyafanye yote kwa wakati mmoja. Mimi nasema ili tuweze kuendelea na iwe kwa kasi zaidi lazima tuhakikishe *judiciary* yetu kwa maana ya Mahakama inatoa haki haraka iwezekanavyo. Tukifanikiwa hapo, maana yake ni moja tu *confidence* ya *Bankers* itapanda, kwa hiyo, ni rahisi kuwakopesha watu na watu wetu watafanya biashara, tutapata ajira, tutapata kodi, *in doing so* uchumi utakua. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia lingine ambalo Mheshimiwa Rais amelisema, ni uwezo wa kutumia nafasi yetu ya kijiografia. Katika hili, watanisamehe wenzangu Serikalini, nafasi yetu ya kijiografia hatujaitumia vizuri na wenzetu wamejua hatuitumii vizuri, wameanza kutumia zingine na baada ya muda mfupi tutakuwa kisiwa. Leo Wazambia wanatengeneza reli kwenda Maputo, kwa hiyo, maana yake tusipokuwa waangalifu, *tusipo-offer efficiency* ya Bandari ya Dar es Salaam na reli yetu ya *TAZARA*, mizigo ile haitakuja tena huku kwetu itapita kule, maana reli tumeipoteza. Reli yetu leo ya kutoka hapa kwenda Kigoma tusipoifanyia kazi iweze kupitika wakati wote, *efficiency* iongezeke maana yake ni nini, Wakongo wale watatafuta *alternative route*. Leo hii Wakenya wanaanza kujenga Bandari ya Lamu, wanajenga reli ya kutoka Mombasa na Lamu kwenda mpaka Rwanda na inakwenda mpaka *South Sudan*, maana yake ni nini? Jiografia yetu ambayo tunatakiwa tuitumie sasa haitotumika na watu watatuacha tutabaki tunaimba sisi tuna jiografia lakini hatuitumii.

Mheshimiwa Spika, lakini leo hii ukiwa unatoka Dar es Salaam una kontena, kontena hili umelichukua bandari ya Dar es Salaam unalipeleka Rwanda, ukitoka Bandari ya Dar es Salaam mpaka unafika Lusumo mpakani, unasimamishwa mara 58, hatuwezi kuwa *competitive*, hakuna anayeweza kuja kufanya biashara na sisi. Unatoka Dar es Salaam unakwenda Tunduma, unasimamishwa mara 58, hakuna atakayeweza kuja na hizi ndizo fursa Mungu ametupa lazima tuwe tayari kuzitumia. Mheshimiwa Rais amesema vizuri sana wenzetu wa Serikali maneno haya tuyaweke kwenye utekelezaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, dunia hii ni ya ushindani na katika mazingira ya dunia ya ushindani usipojiandaa hakuna atakayekusaidia. Mungu ametupa kila kitu, tuna bandari, tuna reli, tuna mbuga za wanyama, *we have everything you can mention* lakini tusipozitumia vizuri, tutakuwa tunatafutana ubaya tu hapa. Kwa hiyo, niwaombe sana na unajiuliza hivi swalii utakaloulizwa kwenye kituo cha kwanza utaulizwa kituo cha pili, kituo cha tatu, utaulizwa mpaka kituo cha 58 unaulizwa swalii hilohilo, tatizo ni nini? Huku utakuna na mizani, huku utakuna na *custom*, huku utakuna na Polisi huku na nani, hakuna atakayekuja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukiagiza kontena kutoka Dubai kufika Dar es Salaam, ni siku 14 lakini kutoka Dar es Salaam kwenda Rwanda ni siku 49. Warwanda hawawezi kuja, Wakongo hawawezi kuja, Waburundi hawawezi kuja, maana yake ni nini? Akitokea mwingine aka-*short circuit* kwamba mzigo wake umefika Mombasa akishaingiza kwenye gari hakuna anayemgusa mpaka anafika, ni *border* mbili tu anaulizwa baada ya pale anatumia muda mfupi atakwenda huko, *these are economics* tu hapa, kwa sababu unapomweka muda mrefu *turnover* haipo huyu anapoteza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni suala la *investment*. Jamani niwaombe sana sisi wanasiwa. Kama kuna jambo litafanya nchi hii tuweze kuendelea lazima tuwe tayari kuheshimu *investors* wa ndani na wa nje lakini wafuate sheria. Lakini ukienda zile nchi ambazo tumeambiwa zimeendelea ni kwa sababu wamehangwaika na *investment* na *investment* maana yake ni nini? Maana yake ni kazi, maana yake ni kodi. Leo hii tumefanya mambo makubwa sana kwenye elimu, Vyuo Vikuu vyetu tumevipanua, tutakuwa tuna wanafunzi wengi kutoka *University*, wanahitaji kazi, wenzangu wamesema hili tusipohangaika nalo ni bomu lingine, litatumaliza sisi Watanzania. Tatalalamika wanakuja Wakenya wanachukua kazi, tuhangaike na *efficiency*. Kwa hiyo, niwaombe ndugu zangu tuhangaike na kutafuta *investment*.

Mheshimiwa Spika, Ilovu walikuja Tanzania wakaanzisha na kuchukua mashamba ya Kilombero baadaye wakaomba ardhi ya ziada, tukapiga danadana kama staili yetu, wamekwend Zambia, ile *investment* ambayo ingefanyika Tanzania wamepeleka Zambia, kesho kutwa Zambia wanakuwa *number two* katika kuzalisha sukari *in Africa*.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, wewe ni Mwenyekiti wa Miundombinu basi kazi kwako.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Mama yangu aliyenizaa na Mke wangu lakini shukrani za kipekee ziwande wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao wamekubali kunipa dhamana ya kuwaongoza katika Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais ina mambo 13 ambayo ye ye mwenyewe ameyaainisha kama ni vipaumbele. Lakini tangu tulivyoanza mjadala huu, nikuhakikishie kwamba ule usemi wa Kiswahili unaosema Baniani mbaya kiatu chake dawa

tumeuthibitisha hapa Bungeni kwa sababu hata wale ambao hawakutaka kumwona wamependa kuchangia Hotuba hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi sitopenda kuzungumzia vipengele vyote ambavyo vimeainishwa humo kwa sababu wachangiaji walotangulia naamini wamechangia vizuri pengine zaidi yangu. Tunazungumzia suala la kuwezesha wananchi kiuchumi. Hili suala ni la makini sana, wapo watu ambao wamechangia lakini na mimi mchango wangu nasema, uchumi sasa tuwawezeshe wananchi kwa kutumia kilimo moja kwa moja. Tuboreshe mioundombinu ya kilimo, kuhakikisha kwamba tunatoa pembejeo na zana zilizobora. Ni vema kabisa tuangalie uwezekano wa kutumia namna yoyote ile tuwakopeshe wananchi vifaa vinavyofaa kulima. *Powertillers* ambazo zimetolewa na Halmashauri hazisaidii sana, tunahitaji matrekta ili tuende kwenye kilimo kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nafasi nzuri ya kilimo ambacho tuko nacho lakini bado hatujawapa fursa wananchi haswa wa maeneo ya Ukanda wa Pwani. Mpaka hii leo mazao yetu ya asili kama vile nazi, embe, machungwa na kadhalika wanalazimishwa kutozwa ushuru. Sasa suala hili liangaliwe kwa makini kama kweli tunataka tuwasaidie wananchi basi tuhakilishe kile kipato kinachotokana na mazao yao kiingie moja kwenye mifuko yao.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia pia tatizo ambalo linajitokeza kwenye suala la mfumuko wa bei. Mimi sijui hata huu utaratibu wa soko huria ambao hauna kikomo tumeuiga kutoka katika dunia gani. Kwa sababu kimsingi ni watu wachache ambao wanawenza wakakaa wakakubaliana, wakapandisha bei ya zao lolote wakati wowote, kama ilivyo kwenye sukari hivi sasa na mazao mengineyo, mtu akipanga tu anapandisha, lakini hatuna *mechanism* nzuri ya kuweza kuhakikisha kweli hii bei inapandishwa kwa uhakika kwa sababu tayari tumewapa uhuru wao wa kufanya wanilotaka. Ipo haja ya kuangalia tena, kama tutaweza kurudisha tena Tume ya Bei sawa lakini Bunge hili litoe mwongozo, tufanye nini kuweza kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, amezungumzia suala la utalii, limeingiza zaidi ya Dola 4,489. Mimi naamini kabisa mapato haya ni kidogo sana ukiangalia na idadi ya watalii wanaoingia hapa nchini. Tujiulize leo Serikali yetu na Wizara imefanya jitihada gani za kuhakikisha malipo yote ambayo wanalipa watalii kwa ajili ya kuingia nchini yanaingia katika mfuko wa Serikali? Mtu ambaye anatoka kwa mfano Uingereza au Marekani ametumia *credit card* au *debt card* amelipa kwenye kampuni ya utalii iliyokuwepo katika nchi aliyotoka, Tanzania sisi tunakusanyaje kodi yetu na tunakusanyaje mapato yetu? Tunategemea wakala aliyemleta ndiye atuambie kwamba huyu mtu nimemchaji kiasi fulani. Ni lazima tuangalie njia bora zaidi na *mechanism* nzuri zaidi ya kuweza kuhakikisha kwamba mapato yanayotokana na utalii basi yanatunufaisha moja kwa moja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la elimu ya msingi na elimu ya juu. Elimu ya sekondari, mwaka huu wanafunzi ambao wamefanya mtihani wa Kidato cha Nne hawakufanya vizuri lakini tusiangalie tulipoangukia, tuangalie wapi tulipojikwaa. Mimi

naipongeza sana Serikali kwa jitihada nzuri za kuboresha, kuweka miundombinu lakini bado inabidi tuhakikishe kwamba tunafanya vizuri zaidi kwa kuongeza tija katika elimu yetu. Kuboresha mazingira ya ufundishaji haswa maeneo ya vijijini kwa sababu Walimu wengi wakishamaliza Vyuo Vikuu ama katika vyuo vingine, hawapendi kuishi vijijini. Kwa nini hatufanyi jitihada tukajenga mazingira mazuri kwa wale Walimu ambao watakubali kwenda kule wakakuta mazingira mazuri zaidi wakawafundisha watoto wetu?

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mimi naamini kabisa kikubwa zaidi ni uwazi. Hii Bodi haifanyi kazi kwa uwazi, ni kama kazi ya msimu na haijulikani pesa zinaingia vipi, zinatoka vipi. Wangetoa semina na kuwaelimisha wananchi na wanafunzi jinsi wanavyopokea na kutoa pesa. Mfumo huu akawa wa wazi zaidi hakuna mtu ambaye angelalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, liko tatizo katika eneo la nishati. Nishati leo imekuwa ni tatizo. Wengi hapa wameshutumu kwa kusema kwamba nchi yetu ina tatizo la umeme, hiyo ni kweli lakini kwanza tujiulize kwa nini umeme umekuwa ni tatizo, ni kwa sababu *demand* yetu imekuwa ni kubwa kuliko *supply*. Kwa hili tukipongeze Chama cha Mapinduzi na Ilani yake imeleta miundombinu na vifaa ambavyo vinafanya umeme utumike zaidi. Lakini katika kukabiliana na tatizo hili, tutengeneze mipango iliyokuwa thabiti, tuharakishe wananchi waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la Songosongo na kwa wanzetu hawa watu wa Mtwara kuna Mnazi Bay mpaka leo tunanufaikaje, hatuvezi kuchaji *royalty* ya gesi ambayo inachimbwa pale ambapo mapato yake yangeweza kutusaidia sisi katika kuboresha jamii zetu, mbona mirabaha mingine inachajiwa katika migodi ya madini na migodi mingine? Naomba hilo nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, wenzangu hapa waliotangulia wamezungumzia sana suala la bandari hasa urasimu wa bandari na kadhalika lakini mimi nitazungumzia moja. Ni sababu ipi ambayo inapelekea leo mizigo ikae Bandari ya Dar es Salaam siku 34 mpaka 40 ikisubiri kupakuliwa wakati Bandari ya Mtwara imekaa haina kazi? Hili ni jambo ambalo linatushangaza sisi hasa watu tunaotoka Kusini kwamba tunatoka katika upande mwingine ambao haustahili ama sisi sio wananchi zaidi kulikoni wenzetu ambao ni wananchi zaidi?

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme mimi sina mengi ya kusema katika hilo, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MHE. AHMED A. SALUM: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kikwete.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuwa Spika wa kwanza mwanamke katika historia yetu ya Tanzania. Niwashukuru wananchi wa Jimbo la Solwa, kwa kunichagua mimi tena kwa mara ya pili. Nawaambia kwamba nitawafanya kazi kama nilivyofanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Tulitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 85 na sasa hivi wembe ni ule ule, kasi ni ile ile na

maendeleo yatakuja kama mvua, nina imani kabisa kwenye Jimbo la Solwa na maeneo yote Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwatoe wasiwasi Watanzania kwa suala zima la amani. Amani Tanzania ni zawadi ambayo Mungu ametupa. Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais yupo, atahakikisha kabisa yeze na Serikali amani inakuwepo. Mimi hilo sina wasi wasi.

Mheshimiwa Spika, vilevile tujipongeze sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi katika suala zima lile, ilipotokea vurugu vurugu hapa na kutoelewana Vyama vyâ Upinzani, tuliooka jahazi hili na kuwaweka Wapinzani vizuri ni sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, suala la amani siyo tatizo kubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na Kilimo Kwanza. Jimbo la Solwa, asilimia 95 ni wakulima. Ukitsemwa Kilimo Kwanza, mimi ni mdau mkubwa sana na katika kutafuta kura na kura nyingi ambazo nimezipata mimi kupitia Chama cha Mapinduzi, ni ahadi kubwa ambayo tumeahidi wakulima wa Jimbo la Solwa kwamba katika miaka hii mitano tunahakikisha kwamba wakulima wanifuika na suala zima la Kilimo Kwanza. Mikopo ambayo tayari imeandikwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tutaisimamia vizuri kupitia Halmashauri yetu na Serikali Kuu yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka zaidi ya shilingi bilioni 160 katika Benki ya *TIB* ili iweze kwenda kuwakopesha wakulima Tanzania ukiwemo Mkao wa Shinyanga na Jimbo la Solwa lakini fedha hizo kama hatutakuwa wakweli na *serious* kabisa kwamba fedha hizi ziende kunufaisha wakulima Tanzania, zitaishia tu kwenye vitabu na meza na hapa sisi Wabunge kuongea tu hivi hivi. Mimi siamini, kwa sababu navyozunguka katika Jimbo la Solwa, wakulima walioko vijijini, kwanza kabisa hata hawaelewi namna gani waanze *process* ya mikopo hii. Maana yake nini? Maana yake wakulima walioko katika Jimbo la Solwa na maeneo mengine hawana sifa za kukopesheka wala hawajui namna gani ya kukopa hii mikopo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba, kwanza kabisa ili wale wakulima na wafugaji kwa ujumla waweze kukopesheka, tuwaandae wawe na sifa ya kukopesheka. Kinyume na kuwaandaa wale wakulima, tutaimba hapa, tutaongea hapa, mambo yote ya kuwakopesha wakulima yatabaki tu hapa hapa kwenye mjadala huu na kwenye vitabu tu. Wakulima wakubwa na wazuri na wenye uwezo ndio watakaofaidika na ile shilingi bilioni 163 iliyopo kwenye Benki ya *TIB*.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwanza, Waziri mwenye dhamana hii, ninaimani Waziri wa Fedha na Benki ya *TIB*, kwanza kabisa watuletee masharti hayo hapa Bungeni, tuyaelewe. Jambo la pili, ikiwezekana watufanyie semina ndogo sisi Wabunge tuelewe vizuri kabisa *process* kuanzia namba moja mpaka pale ambapo wakulima wanawenza kufaidika na mikopo hii ili tutakapokwenda Majimboni, tujue kabisa namna ya kuwaeleza, kama ni kuunda vikundi, wasajiliwe, watambulike rasmi, basi wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi naamini na nilishawaahidi wananchi wa Jimbo la Solwa kwamba nitakuwa karibu na wakulima pamoja na wafugaji kuanzia hatua za mwanzo mpaka mwisho baina ya wakulima, wafugaji na Benki, nitakuwa katikati yao ili kufanikisha suala hili. Naamini Benki yenyewe na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataweza kupeleka uelewa huu kwa wakulima wetu ili waweze kukopesheka. Naomba Serikali ijue kwamba tatizo kubwa ni sifa kwa wakulima kukopesheka basi!

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wakulima, kazi hii ya kuwakopesha wakulima jamani twendeni haraka. Naomba kama Serikali imeamua kuweka Benki ya Wakulima basi ifanye haraka na naishauri kabisa kwa kuwa asilimia kubwa ya Pamba inatoka Shinyanga, wakulima ni wengi, naishauri Serikali *Branch* ya Benki ya Wakulima iwekwe katika Mkoa wa Shinyanga, naishauri hivyo.

Mheshimiwa Spika, umwagiliaji, Shinyanga sasa hivi kutokana na hii *climate change*, tumekumbwa na tatizo kubwa sana la njaa na hasa Jimbo la Solwa na nilishaeleza hata kwenye Kamati yetu ya Chama, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaelewa vizuri sana. Tathmini iliyolekwa mwezi Desemba yaani ni miezi miwili tu mpaka sasa hivi hali inabadilika vibaya sana. Kwanza kabisa, niiombe Serikali ichukue umuhimu wake na ifanye juhudhi sana. Mwaka 2005 tulivyokumbwa na tatizo la njaa, Kitengo cha Maafa walipeleka watu watano kufanya *assessment* katika Jimbo la Solwa pamoja na Mkoa mzima wa Shinyanga, tulipata chakula kizuri na iliondoa tatizo kubwa mno katika Jimbo la Solwa na Mkoa mzima wa Shinyanga. Naomba Serikali ifanye haraka mno, hali siyo nzuri, hali ni mbaya mno katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umwagiliaji, kuna shilingi milioni 900 ambayo Serikali ilituahidi mwaka jana. Tukiingia kwenye suala zima la proram ya umwagiliaji ndiyo tegemeo la wananchi wa Jimbo la Solwa pamoja na Mkoa wa Shinyanga kwamba tukiweza kuingia kwenye programu ya umwagiliaji, ndiyo kitakachotuokoa pale ambapo tunahitaji mvua, hamna mvua, kilimo cha umwagiliaji kitawezu kutuokoa. Tuliahidiwa shilingi milioni 900, lakini mpaka sasa hatujapata, naomba Serikali ilifuatilie suala hilo ili hela tuliyohidiwa kwa programu ya umwagiliaji katika Kata ya Samue ifike na tuondokane na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, viwanda, mkulima au mfugaji au mwananchi yeote Tanzania ananufaika vipi na rasilimali yake? Leo Shinyanga tuna Pamba asilimia 60, hatuna kiwanda cha nguo. Leo, Shinyanga tuna mifugo zaidi ya milioni 4 au 5 (ng'ombe), hakuna kiwanda cha nyama. Sasa kumfanya mkulima aweze kunufaika na kuwa na maisha bora ni Serikali kutengeneza mazingira na kuwatafuta wawekezaji waje katika Mkoa wa Shinyanga. Naiomba Serikali ifanye hivyo. Tukiwa na viwanda viwili, vitatu vya nguo Shinyanga, tukiwa na kiwanda kimoja cha nyama Shinyanga, wakulima pamoja na wafugaji wataweza kuwa na soko la uhakika kabisa kwa maana ya kilimo pamoja na mifugo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, elimu, kushuka kwa elimu, *Form Four* wala hakuhitaji masuala marefu sana. Tunahitaji nyumba za Walimu, ni vitu vya kawada kabisa, tunahitaji maabara na tunahitaji *incentive* kwa ajili ya Walimu. Hivi Walimu unavyowaleta vijijini wanapokimbia, wanakimbia kwa sababu gani? Kwa sababu ya mazingira yale, lakini ukimwongezea mshahara, mimi nadhani atabaki. Tufikirie kuwaongeza mshahara Walimu ambao wanakuja vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. EUGEN E. MWAPOSA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama Bungeni, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu ndiye aliyenisimamia sana na kunipigania wakati natafuta kura kwa ajili ya nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru sana wapigakura wa Jimbo la Ukonga pamoja na wananchi wote, kwa jinsi walivyonihamini ili niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Niwahakikishie tu kwamba nitawawakilisha kwa uaminifu mkubwa na sitawaangusha kamwe.

Mheshimiwa Spika, vilevile niishukuru sana familia yangu kwa sababu ilini-*support* sana wakati ninatafuta kura kwa ajili ya nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye kuchagia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo aliileta hotuba hii. Ni hotuba ambayo imeja mapana na marefu, lakini ni hotuba ambayo imewapa Watanzania matumaini makubwa na hasa kama itapata utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu, napenda kuchangia katika kipengele kile ambacho Rais alikiita majukumu ya msingi. Mimi nitachangia kati ya vile vipengele vitatu, nitachangia kipengele cha pili ambacho nia yake ilikuwa ni kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ili kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa nchi na watu wake. Katika kuchangia kipengele hiki, napenda sana kujikita katika kipengele cha kuleta mapinduzi ya viwanda, pia nitazungumzia sana kipengele cha kuwawezesha wananchi kiuchumi halafu nitaongelea kidogo suala la elimu, nitamalizia na suala la bei ya bidhaa.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kipengele changu cha kwanza, nataka tu kumpongeza Rais kwamba hili suala la kufikiria kuleta maendeleo au mapinduzi katika viwanda, ni suala la msingi sana. Hili jambo litatusaidia kwa kiwango kikubwa kwa sababu katika nchi yetu na hususan katika Jimbo langu la Ukonga wako vijana wengi sana ambao hawana kazi, hawana ajira. Kama tutafanikiwa kuanzisha viwanda, basi viwanda hivi vitasaidia sana vijana wetu kupata kazi na kuweza kutumia nguvu kazi ya vijana wanaotoka vyuoni ambayo sasa hivi Serikali hatujui inakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, licha tu ya kutumia nguvu kazi katika viwanda hivi, viwanda hivi vitatusaidia sana kuza mazao ambayo yanazalishwa hapa nchini. Tunayo mazao mengi ambayo tunayazalisha lakini hayana masoko. Mengine hata kama yana masoko, lakini yanachukuliwa kwa mfano, matunda yanavuka tu mpaka kwenye nchi ya jirani hapa, halafu yanarudi katika *form* ya *juice*, halafu tunauziwa kwa bei ya juu wakati ambapo tungeweza tukazalisha hivyo vitu, tukavitengeneza hapa nchini kwa kutumia viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia licha ya kupata masoko kwa ajili ya bidhaa zetu, viwanda vitatusaidia vilevile kuweza kujipatia fedha za kigeni ambazo zitatuwezesha pia kununua vitu vingine ambavyo hatuzalishi hapa nchini. Kwa hiyo, ninaomba sana utekelezaji wa hili jambo ufanyike ili liweze kuleta manufaa kama nilivyoainisha hapo mwanzo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye kipengele kingine cha kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika kipengele hiki, Mheshimiwa Rais ameongelea mambo ya *TASAF*, ameongelea mambo ya *MKURABITA* pamoja na mambo ya kuwawezesha wananchi kwa kutumia vikundi vidogo vidogo kama *VICOBA* pamoja na *SACCOs*.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye suala la ule Mfuko Maalum kwa jina la Mabilioni ya JK. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Mfuko ule ulipata fedha na fedha zile zilikuja katika njia mbili. Njia ya kwanza, zilikwenda kwenye zile Benki ambazo zilikuwa zinawakopesha wananchi moja kwa moja lakini fungu lingine lilikwenda kwenye Benki ambazo zilikuwa zinashusha zile fedha kwa wananchi kwa kutumia vikundi kama *SACCOs* pamoja na *VICOBA*. Katika kundi la kwanza, fedha zile zilikwenda kwa makundi ambayo kusema ukweli hawakuwa walengwa halisi wa kupata fedha zile. Hazikuweza kuwafikia wananchi wa hali ya chini kwa sababu ya mtiririko mzima wa kuzipata zile fedha ulivyokuwa. Niseme kwamba pia, kwa utafiti mdogo ambao nilifanya, fedha zile ambazo zilizokopeshwa na Benki kwenda kwa wananchi moja kwa moja pia hazikuweza kurudishwa kwa ajili ya kukopeshwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini tukiangalia katika kundi la pili ambalo lilikopeshwa *SACCOs*, lile kundi fedha nyingi ziliweza kurudi. Lakini tatizo moja ambalo nililiona ni kwamba Serikali iliagiza kwamba wananchi wapate zile fedha kwa riba ya asilimia 10. Lakini bahati mbaya sana zile fedha walikuwa wanakopeshwa *VICOBA* kwa asilimia 10 pamoja na *SACCOS*, halafu *SACCOS* inaweka hapo asilimia sita au saba, halafu inawafikishia wananchi kwa asilimia 17 au 16. Asilimia 17 ni kubwa sana kwa mwananchi au mfanyakibashara mdogo. Naomba kama neema hii itakuwepo tena, basi Serikali iangalie ni namna gani ambavyo inaweza ikashirikiana na Benki ili wakopeshwe kwa asilimia ndogo ili ile asilimia 10 iweze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala la Benki ya Wanawake. Nipongeze sana Serikali kwa jinsi ambavyo ilitia msukumo katika hili. Ile Benki ni kweli imeonekana

kuwa ni mkombozi mkubwa wa mwanamke lakini pia niwashukuru sana kwa sababu wale wanachukua dhamana ambazo Benki nyingine hazichukui. Wanachukua leseni za makazi, leseni za magari na kadhalika lakini lipo tatizo pia la riba ambayo ni kubwa. Nilikuwa naomba kwa sababu Serikali pia ina-*invest* pale, basi iweze kuongea na Benki ile ili wananchi waweze kupata fedha kwa riba ndogo zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite sasa kwenye suala la elimu kwa sababu suala la elimu limekwishazungumziwa sana na wenzangu waliopita. Naomba nizungumzie suala la shule za msingi hasa shule ambazo ziko katika Jimbo la Ukonga, ni shule za wakazi amba uwezo wao ni mdogo. Naomba sana, pamoja na changamoto nyingine zote, lakini Serikali iangalie ni namna gani wale watoto wa watu maskini waweze kupata angalau mlo mmoja wa shulenili ili waweze kufuatilia vizuri masomo yao na waweze kuwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba nijikite tena kwenye suala la bei za vyakula. Bei ya vyakula inapanda usiku na mchana. Imekuwa ni kitendawili kwa sababu unaamka unakwenda kununua sukari, kesho ukienda tena unakuta sukari imepanda kwa kiwango kikubwa. Sukari sasa hivi ni shilingi 2000/=, mafuta lita moja ni shilingi 2500/=, ukija kwenye maharage ni shilingi 1800/=. Nipongeze Serikali kwa sababu imeweza sana kudhibiti bei ya mafuta, imeweza sana pia kudhibiti nauli za daladala kwa kutumia *EWURA* pamoja na *SUMATRA*. Niwaombe sana waangalie ni jinsi gani wanaweza kuweka Tume ya Bei kwa ajili ya kulinda mlaji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Rais ambayo aliitoa wakati akifungua Bunge lako Tukufu tarehe 18 Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliye niwezesha kuwepo mionganoni mwa Wabunge wenzangu walio katika Bunge lako Tukufu. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru sana wananchi na wapiga kura wote wa Jimbo la Ileje kwa imani yao kubwa kwangu, kwa kunipa kura nyingi na baadaye nimeweza kuingia na kuungana nanyi katika Bunge hili Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe pia kwa kupata nafasi hiyo ambayo umeweka historia katika nchi yetu, nakupongeza sana. Niwapongeze pia Wabunge wenzangu wote wa Chama cha Mapinduzi na kwa kweli pia watani zangu wa upande wa pili, Wabunge wa Upinzani, hongereni kwa kupata nafasi ya kufika katika jengo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya muda, naomba sasa nichangie hotuba ya Rais, nitazungumzia mambo machache, mengi yameongelewa na wenzangu lakini walau nizungumze machache hasa kwenye eneo la elimu, afya, mazingira, amani na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari sana, wenzangu wengi wamezungumzia juu ya elimu, sasa hivi nchi yetu tunajiandaa kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kweli tumeshaingia, tumeamua, tunatakiwa sasa kujua, je, tumejipanga sawasawa kushindana na wenzetu kwenye eneo la elimu? Hatutaweza kufanya chochote, tutakuwa watu wa kushangaashangaa, wenzetu wataendelea kuchota ajira, sisi hatutafanikiwa tusipokuwa na mkakati mkubwa na maalum kwa ajili ya kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri na maamuzi mazuri ya Chama cha Mapinduzi, kuamua kila Kata katika nchi yetu iwe na Shule ya Sekondari, hilo ni jambo jema. Wale tunaokumbuka enzi za miaka ya sabini, miaka ya themanini na kwa kweli miaka ya tisini, viji vingine vilikosa kabisa vijana wa kwenda sekondari, viji vingine vilitoa mtoto mmoja, lakini sasa vijana wetu wengi wanakwenda sekondari.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ambazo ni lazima tukabiliane nazo, Walimu wengi wanafundisha katika mazingira magumu mno. Ninao mfano wa Jimbo langu la Ileje, jiografia yake ni ya milima, barabara ni vigumu kupidika, Mbunge ye yeyote aliyepo hapa afikirie kwamba anaishi Dar es Salaam au Dodoma na mtoto wake anapangiwa katika Jimbo ambalo miundombinu haipo, kwa maana ya barabara, mitandao, hospitali za uhakika, halafu anafika Makao Makuu ya Wilaya anaambiwa aende, haendi. Ninavyo viji vingine mbalimbali katika Jimbo langu ambavyo kwa kweli mtoto ye yeyote anayetoka mbali hasa wale wanaotoka mjini, wakimaliza Vyuo vya Ualimu wakipangija katika Kata zile, wengi wanakimbia kwa sababu wakifika kwanza wanaanza kutembea kwa miguu, barabara hazipitiki, anatembea kilometra hamsini au kilomita arobaini kutoka Makao Makuu ya Wilaya, akifika kule anakuta nyumba hamna, akifika kule anakuta maji hamna, katika hali hiyo wengi wanakimbia.

Mheshimwia Spika, naomba nitoe ushauri katika eneo hilo, pengine kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu inayokuja, nishauri na ninaamini kila Mbunge aliyepo hapa angependa kusikia hivyo kwamba Walimu waliopo katika maeneo magumu kwa utendaji wa kazi, wapewe malipo ya ziada ya mazingira magumu ya kazi. Halmashauri zetu, Wakurugenzi, Maafisa Elimu na Utawala wa Wilaya kwa ujumla, unaweza kulifanya hilo kwa kuainisha Kata fulani na Walimu wanaoishi maeno haya wapewe pesa ya ziada, posho ya hali ngumu ya mazingira mpaka hapo hali itakapotengemaa.

Mheshimiwa Spika, kwenye afya, siwezi kuzungumzia mifano nje ya Wilaya yangu na Jimbo langu la Ileje, tunayo Hospitali moja ambayo imeendelea kutumikia Watanzania walioko katika Wilaya ya Ileje, wapigakura ambao wamechangia kuunda Serikali hii tuliyopo, kura zao zipo, lakini hospitali hiyo ilikuwa ya misheni baadaye Serikali imeingia ubia nayo na kuwa *DDH*. Nasikitika kwamba toka mwaka 1976 mpaka leo hospitali hiyo haijawahi kupewa gari na Serikali ili lisaidie wagonjwa badala yake tumeendelea kutumia gari za mmiliki wa hospitali ambaye ni misheni ambapo sasa hivi kwa kiwango kikubwa, kwa asilimia zaidi ya themanini amepunguza misaada yake. Naomba Serikali katika bajeti ijayo pamoja na maeneo mengine iainishe, iangalie uwezekano wa kuwapatia vitendea kazi watumishi wanaoishi katika hospitali hii.

Mheshimiwa Spika, lakini pia watumishi wanaofanya kazi katika mazingira yale, Madaktari wakifika kuripoti wanaondoka, *Clinical Officer* wanaondoka, *Assistant Medical Officers* wanaondoka, Manesi wanaondoka, je, Serikali inachukua hatua gani? Mawazo na ushauri wangu ni tuone namna ya kumaliza shida hii, wahudumu hawa wa afya wapewe motisha kwa kuishi maeneo haya.

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili, nilikuwa nimevutiwa na mchango wako, nimesahau kwamba ni kengele ya pili.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Naomba nianze kwa kukupongeza wewe Mama yetu kuwa Spika wa kwanza mwanamke. Nichukue fursa hii kuwashukuru wapenda maendeleo wa Kagera na hususani wapigakura wa Wilaya ya Muleba Kaskazini, kwa kuniamini na kunipa jukumu hili zito lakini ninalolipenda sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna vitabu viwili navyovipenda sana baada ya kupewa jukumu hili, kitabu cha kwanza ni Ilani ya CCM, kitabu cha pili ni Hotuba ya Rais. Vitabu hivi ndivyo vinavyoniongoza katika kutenda kazi na tayari nimeshaanza kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nипитие kwenye mambo ambayo Rais aliyaainisha ili niweze kuchangia, tuelimishane, tuelekezane na wenzangu. Naomba Watendaji wa Serikali, tujenge utamaduni wa kupeana muda tunapozungumzia mambo haya. Mfano tunasema jambo fulani ni tatizo, tungeomba wahusika mtueleze je, hilo ni tatizo au tujipangie hilo tatizo totalitatua lini, haya mambo ya kusema tu, inakatisha tamaa na inamaliza nguvu.

Mheshimiwa Spika, Rais aliainisha kipaumbele namba tano, faida ya kijiografia, watalamu wa mikakati watakuambia sisi tunayo-*location advantage*, faida ya pale tulipo ni faida ya kiushindani, *the competitive advantage*, lakini faida ya mahali ulipo au *competitive advantage* inaweza ikaondoka. Naomba tupewe muda, haya mambo tunayoyazungumzia, yatakekelezwa lini? Mimi nimeanza kupiga kelele siku nyingi kweli, naandika kwenye magazeti, nikajipenyeza mpaka kwenye ofisi kubwa jamani hii fursa ya mahali tulipo mbona hatuitumii?

Mheshimwia Spika, mafuta ya *petrol* kwenda DRC Congo yameanza kupitia Beira baada ya mimi kujitahidi kushawishi yapite Dar es Salaam kushindikana. DRC-Congo, Lumbumbashi uchumi wao unakua kwa asilimia 27, kama mafuta yote yangepita hapa, kama tungepata shilingi mia tano kwa kila lita inayopita hapa tungepata pesa nyingi, wapi! Nimekuwa nikisema nikiwa nje, nimefika hapa nasema, naomba utaratibu wa kupeana muda au *time framework* uwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia suala la bandari, nimelifuatilia, nisingependa kulisemea sana kuna matatizo pale, rafiki zetu wa *TRA* wana matatizo, lakini ukizungumza nao kirafiki mmoja mmoja na wao matatizo wanayatupa upande mwingine, wale watu huwezi kuwanyonga, ukija kuwanyonga wanarudisha mpira kwingine. Kuna matatizo pale, naomba Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha muangalie pale, wananchi hawawezi kulia na sisi tukalia, kama kuna matatizo bandarini, sisi tuna mamlaka, tuielekeze Serikali yetu na tuweze kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, *competitive advantage* ya sehemu ya kijiografia haiishii bandarini tu, kuna fununu kwamba DRC-Congo wangependa wawe sehemu ya Afrika Mashariki, kuna fununu kwamba Sudan Kusini wangependa wawe sehemu ya Afrika Mashariki, hilo likifanyika, Kagera inakuwa katikati ya Afrika Mashariki. Kagera kuwa katikati ya Afrika Mashariki kubwa, *subcontinent* haitoshi, ni namna ya kutumia hiyo faida ya kiushindani. Naomba mamlaka zianze kuturuhusu sasa tufanye mazoezi ya kulima sana ndizi tuenze kupeleka Darfur na Sudan. Nasikia Sudan chochote unachopeleka kinanunuliwa, sasa Waganda wanunua kwetu wanakwenda kuuza kwa faida kubwa sisi tunashabikia kuangalia. Wakati umefika na ningeomba mnipe fursa mimi ni mhamasishaji, nihamasishe kupeleka ndizi Sudan, nipeleke mchele wa Shinyanga, nipeleke mihongo ya Sengerema, *competitive advantage* haina maana kama hutukuitumia, hilo nilianche nadhani limefika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la Kilimo Kwanza, namshukuru Rais alipokuja kwetu alisema mabonde ya Burigi yatalimwa mpunga, watu wa kwetu wanapenda mpunga kweli, naomba mabonde ya Burigi yanapoanza kulimwa tuyaone.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza sisi kinaendana na shughuli za uvuvi, vijana wa kwetu wanasaafiri, wanakwenda Uganda, nchi ya Uganda inapata faida kubwa kutokana na ufugaji wa samaki kwa njia ya mabwawa, Malyasia imechukua jitihada za kusoma ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa, nchi za Malyasia zinapata faida kubwa, naomba Wizara ya Uvuvi iongeze nguvu, iufanye Mkoa wa Kagera na hususani Wilaya ya Muleba mfano wa kufuga samaki kwa mabwawa, *economics* zake zinakubalika. Mimi nitapiga baragumu na vijana wameshaanza kuchimba mabwawa tuone tutafika wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Kilimo Kwanza, vilevile nichukue fursa hii, kushukuru Wizara ya Kilimo, tuna matatizo kweli ya ugonjwa wa migombा, lakini leo hii imefanyika semina kubwa baada ya kuzungumza na wahusika, watu wa kilimo wako kule wanafanya utafiti kuweza katuondolea tatizo la ugonjwa huu. Naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uvuvi, kuna tatizo lingine la viwango vya nyavu. Nyavu zinazotumika upande wa Tanzania zina macho madogo kuliko nyavu zinazotumika Uganda ilhali viwango ni vilevile, samaki hawana mipaka, wana-*migrate* tu. Sasa matatizo yake ni kwamba wavuvi wa upande wa kwetu hasa Visiwa vyangu tisa wanasumbuliwa kweli na Wakaguzi. Tarehe saba walipita watu wanawafuata Wavuvi, wanawaambia mnatumia nyavu zisizotakiwa, wanakusanya pesa, naomba hilo lifuatiliwe ili tuwe na *standard* moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii, kuwapa pole wanaharakati wenzangu wanaopenda shule, tumehangaika kweli kujenga Sekondari za Kata, lakini niwaambie tumeshindwa pambano hatujashindwa vita. Nachowaomba Watanzania wenzangu, elimu au ujenzi wa shule na zenyewe tuziweke kwenye vipaumbele. Sisi kama jamii pamoja na Serikali, ni wangapi mionganoni mwetu wana kadi za kuchangia shule, lingenisha na kadi za harusi na vipaimara tulizonazo? Tupige harambee, tukusanye rasilimali, tujenge shule, ninaimani ya Serikali hayo yatatukuta mbele.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kumshukuru Waziri wa Maliasili na rafiki yangu hapa Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa Kilufi. Mheshimiwa Kilufi ameweza kutatua mgogoro wa Mbarali kwa Maliasili kukaa na wananchi. Naomba mfano huo utumike kwenye mgogoro wa ardhi kati ya *NARCO* na wananchi wa Jimbo langu ambapo nchi ya baba yangu nchi ya Tanzania, inatumiwa na watu wa Mataifa ya jirani kama sehemu ya kuchunga. Hakuna kashfa kubwa kwa Mhaya kama shamba la baba yako, unakuta mtu anachunga ng'ombe. Shamba la baba wa baba yako wanapanda viazi. Mnisaide nimalize tatizo la Lutoro kwa mimi kama alivyo Mheshimiwa Kilufi hapa rafiki yangu, nitakuwa *mediator* kati ya *NARCO* na wakulima. Wakulima wananipenda sana na siri moja, wananchi wakipata matatizo hawaedi Polisi wala kwa Mtendaji wanakwenda ofisi za Chama cha Mapinduzi bila kujali itikadi zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sana hotuba ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wa Chama change. (*Makofii*)

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupewa nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia katika Bunge lako Tukufu ambalo kwa kweli ni mara yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wananchi wa Mbarali kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na mimi naahidi kabisa kwamba nitawatumikia kwa uaminifu na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba hotuba ya Rais ni dira ya kuelekea kwenye kutatua matatizo ya Watanzania. Nampongeza sana Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo kimsingi inaonekana kabisa kwamba kama itasimamiwa, matatizo ambayo yanawakabili Watanzania yataisha lakini yapo matatizo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba mipango tunayo mizuri sana, Rais ameonesha mipango ambayo ikisimamiwa, nchi hii haitakuwa katika matatizo

ambayo tunayajadili sasa hivi. Tuna matatizo kwenye utendaji, ni wazuri sana kwenye kupanga lakini kwenye usimamizi, kwa kweli kama tungekuwa tunapewa alama tungepata sifuri, hakuna usimamizi. Mipango tunaweza sana kupanga na Rais ametoa mwelekeo kabisa kwamba kama mipango hiyo itasimamiwa, ndio maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana lakini maisha hayo yanakuwa ni ndoto kwa sababu ya kutokujibika. Uwajibikaji nchi hii uko kwa kiwango cha chini sana.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na *gape* kubwa kati ya Watendaji na Waheshimiwa Wabunge. Vyombo hivi viwili kama Serikali na Waheshimiwa Wabunge, wataungana pamoja katika kusimamia vipaumbele ambavyo Mheshimiwa Rais ameviainisha, nina hakika kabisa kwamba Watanzania watapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitahadharishe, hawa Watanzania wa leo siyo wale wa siku zile za nyuma, wana uelewa wa kutosha kabisa. Watanzania wa leo jambo likifanyika wanaelewa kwamba hapa tumetendewa isivyo. Hatutaweza kufanikiwa kabisa kama hatutasimama imara kusimamia kikamilifu mipango ambayo tunaipanga wenyewe.

Ndugu zangu mimi nimeshuhudia mwenyewe kwa macho yangu sisi tumekuwa na mipango ambayo tunadhani kwamba itawasaki, lakini iko mipango mingine tunaipanga bila kuangalia vizuri kama ni kweli itawasaki wananchi wetu. Kwa mfano, ipo Sera nzuri ya Uwekezaji hata mimi naipenda ni Sera nzuri, lakini Sera hii haikuzingatia sana wale wanaozunguka eneo lile la mwekezaji watanufaika namna gani. Imekuwa ikipangwa tu kwa kuona kwamba tunataka uwekezaji kwa mfano, tumewekeza kwenye mashamba makubwa ya kilimo ambayo Serikali ilikuwa inayamiliki. Wakati ule Serikali ilipokuwa inayamiliki wale wananchi walikuwa wamepewa fursa fulani ya kunufaika na mradi ule lakini sasa baada ya kupelekwa kwa wawekezaji, tumepeleka kule bila kuangalia maslahi ya wananchi wanaozunguka shamba lile watanufaika namna gani. Matokeo yake, yule amekuja amepewa shamba, hakupewa *conditions* zozote, anafunga maeneo yale ambayo watu walikuwa wanasaidiwa kupata maji, anazuia kabisa maana yake ni kwamba maeneo yao yale hayatalimika.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kama unaweza kufika maeneo hayo, ukaona kilio cha wananchi wa Mbarali, kwa mfano ukienda shamba la Kapunga lililokuwa la *NAFCO*, Kijiji cha Mwashikamile, ni mionganoni mwa vijiji vilivyoathirika sana pamoja na Kijiji cha Kapunga. Wale wananchi walikuwa na maendeleo makubwa sana, lakini sasa hivi makazi yao ni magofu sababu kubwa ni kwamba kilimo chao hakipo, maeneo yale waliyokuwa wanapewa maji, Serikali ilikuwa inawasaki kama wanufaika wanaolizunguka shamba, sasa wawekezaji wale wamezuia na hakuna pa kuwaauliza kwa sababu katika mikataba yetu hatukuangalia hilo. Nadhani sasa tubadilike, uwekezaji uzingatie na maslahi ya wananchi watakuwa wanayazunguka maeneo ya uwezekezaji. Kama hilo hatutaliangalia, hawa wananchi wa maeneo hayo tutawafanya kuwa maskini badala ya kuwa na maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie sekta ya mifugo. Wafugaji katika nchi hii, wamekuwa wakiwa. Wafugaji wa maeneo yote, hakuna utaratibu mzuri ambao

umekuwa ukiwalinda na kuona kwamba ile ni sehemu ya ajira ya Watanzania. Nataka niwahakikishie ndugu zangu wafugaji, walibarikiwa na Mwenyezi Mungu toka enzi hizo, wale wanaosoma vitabu Vitakatifu wanajua. Walikuwa ndio wa kwanza kwenda kuona mahali alipozaliwa Yesu Kristo. Mkubali kwamba sekta hii kama hatutaisimamia vizuri, tutapata laana. Wafugaji wa nchi hii wanahangaishwa, utafikiri tuna ng'ombe wanaozidi nchi za jirani kumbe kuna majirani ambao wana maeneo madogo kuliko sisi lakini wafugaji wao wamestarehe lakini siyo sawa na nchi hii wanapata tabu mno wafugaji ndugu zangu. Nashukuru kwamba mimi nimepangwa Kamati hiyo hiyo, nadhani nitasimama imara kabisa kuhakikisha kwamba wafugaji nao wanaleshimiwa kwa sababu wana baraka za Mwenyezi Mungu na sisi tutabarikiwa tukiwasimamia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo tuna maradhi ambayo tusipoyaangalia hawa Watanzania watafika mahali hawatatuamini tena. Siku za nyuma tulikuwa tunasema hivi, ‘aliye juu mnoge chini’, siku hizi methali hiyo haifai tena ‘aliye juu mfuate huko huko’. Kwa sababu gani? Hawa Watanzania wana maradhi mengi ambayo sisi tumeshindwa kuyasimamia, watafika mahali hawatusikiliza tena. Kwa mfano, rushwa imekithiri, tumewasaidiaje Watanzania hawa kuondokana na maradhi haya ya rushwa? Tumeona kabisa hakuna haki zinazotolewa vizuri kwenye Mabaraza ya Kata, huko kwenye Mahakama kote kumeharibika, ni rushwa tu. Naamini kabisa kwamba Baraza Jipyia la Mawaziri lililoundwa, tafadhalini muwe ni marefallii wazuri, mtusaidie kusimamia hao Watendaji kama hamtafanya hivyo basi itafika siku hawa Watanzania hawatatuelewa. (*Makofi*)

Mheshimwia Spika, naomba kabisa kila Waziri kwenye Wizara yake asimamie kwa karibu kuona kwamba watendaji wa Serikali wanafanya kazi kikamilifu badala ya kutengeneza watu ambaeo ni nusu miungu. Wako watu huko ni mabwana wakubwa. Tunayo mifano mizuri, michango hii ya Sekondari, wananchi wamejitoa vizuri kabisa kuchangia, lakini inafika mahali inakuwa ni kero kwao. Michango ya sekondari ina muda maalum, lakini unakuta muda huo mzuri wa kuchangia wanawaacha, lakini muda ambaeo hawana fedha kwa sababu hawa ajira yao ni kilimo, wamemaliza fedha zote ndio wanakamatwa sasa kuchangisha mchango wa Sekondari. Hii yote sasa unataka kuwadhalilisha kwa sababu wamemaliza hela, unataka uwakamate walipe kutoka wapi? Kwa hiyo, yako mambo mengi ambayo tatizo kubwa ni usimamizi. Kama tutafaalu vizuri kusimamia mipango yetu, nina uhakika nchi hii itakuwa na amani.

Mheshimwia Spika, yako maradhi mengi siku hizi yamejitokeza hasa magonjwa ya moyo, ni mengi sana kiasi kwamba yanatishia uhai wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Magonjwa ya moyo ni kama ya rushwa hivyo hivyo. (*Makofi*)

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Rais mnamo mwezi wa kumi na moja.

Mheshimwia Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha leo kusimama hapa nikiwa na afya tele kabisa. Lakini pia nitakuwa ni mnyimi wa fadhila kama sitawashukuru viongozi wote wa Chama cha Wananchi *CUF*, katika Wilaya yangu ya Rufiji na Chama cha Wananchi *CUF* ngazi ya Taifa, kwa kuniona mimi na kunipa dhamana hii kubwa ya kuja kuwawakilisha Watanzania katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie machache sana katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. Moja kwa moja naomba nichangie kipengele cha afya. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Rais, ameleezea Sera ya mwaka 2007 ambayo ilibeba mambo makuu manne. Jambo la kwanza, naomba ninukuu, ni kuongeza, kusogeza huduma ya afya karibu na wanapoishi watu. Hili bado ni tatizo. Bado wananchi wetu wanatembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma afya. Naomba Serikali iongeze nguvu zaidi katika hili ili wananchi wetu wasipate tabu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata katika sehemu ambazo Zahanati hizi zimejengwa bado uhaba wa Wauguzi ni mkubwa sana. Kwa mfano, katika maeneo ya Rufiji, katika eneo la Delta, utakuta Zahanati ina Mhudumu/Muuguzi mmoja tu wa afya lakini Mhudumu huyo anapokwenda kuchukua mshahara au anapokuwa likizo, anafunga kufuli katika Zahanati ile. Sasa je, mwana mama ambaye anataka kwenda kujifungua kwa wakati huo anasaidiwa vipi mtu kama huyo? Kwa kweli inasikitisha sana. (*Makofi*)

Mheshimwia Spika, naomba Serikali ituangalie sisi akina mama kwa jicho la huruma sana kwa sababu mimi naamini kwamba bila ya mama hata sisi Wabunge tusingekuwepo humu ndani. Mama ni *number one* na hana mshindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huduma bado ni mbaya sana hasa kwa upande wa mama wajawazito na watoto walio chini ya miaka mitano. Mama wajawazito na watoto wetu bado wanakufa sana kwa maradhi ambayo yanaweza kutibika. Lakini bado hali inakuwa ni ile ile ya kila siku kwamba huduma zinaboreshw, mama wajawazito watapata matibabu mazuri lakini wanakufa kwa maradhi ambayo yanaweza yakasimamiwa na wakatibiwa vizuri zaidi.

Mheshimwia Spika, lakini pia naamini hata hili tatizo la ufaulu wa watoto wetu, linachangiwa na hiki kipengele cha afya. Kwa mfano, tunaambiwa katika baadhi ya tafiti kwamba kwa kila watoto 100 ambao wako chini ya umri wa miaka mitano basi watoto 44 hawapati lishe bora. Sasa hawa watoto ubongo wao utajengwa vipi ili wawe wazuri zaidi katika kupokea masomo yao hapo wanapokuwa? Mimi naona hapa kuna tatizo, inabidi Serikali iangalie zaidi katika kipengele hiki.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ilitamka kwamba Wazee wote ambao wako juu ya miaka 60 watapata matibabu bure lakini hili bado ni gumzo kubwa. Wazee wetu bado

wananyanyasika, huduma zenyewe ukienda chini kwa kweli hazieleweki. Naomba Serikali inapotoa tamko hasa katika mambo yanayohusu jamii hasa ya kimsingi basi iwe inafanya ufuatiliaji wa kina kabisa hasa katika ngazi za chini katika Zahanati zetu, katika Vituo vya Afya kwa kweli hali ni ngumu, wazee bado wanalamika. Naomba wazee hawa waangaliwe sana kwa ukaribu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kuchangia katika sehemu ndogo ya maji. Naamini kwamba tatizo la maji kama Mheshimiwa Rais alivyosema katika hotuba yake kwamba tatizo la maji bado kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania, naona na naamini kwamba tatizo la maji katika nchi yetu ndiyo hasa inapelekea katika matatizo ya kipindupindu. Kila siku tunasikia kipindupindu Dar es Salaam, Mikooani lakini yote hii ni kwa sababu watu bado wanaendelea kunywa maji ambayo siyo safi na salama. Naomba katika huduma zote za msingi hasa maji, elimu, afya, Serikali iweke kipaumbele, iongeze nguvu zaidi ili wananchi wengi waweze kujikwamua katika matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru, sina mengi ya kuongea zaidi ya hapo, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati akizindua Bunge hili. Nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Bukoba Vijijini walionichagua kwa kura nyingi sana nikawa Mbunge na mwakilishi wao katika Bunge hili la Tanzania. Niwahakikishie kwamba nitakuwa mwaminifu kwao, nitatimiza wajibu wangu kwao na kwa nchi hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Bunge hili tarehe 14 mwezi wa 11, niseme kwamba ilikuwa ni nzuri sana na iliyosheheni mambo yote yanayohusu ustawi wa nchi hii. Alianzia suala la umoja na amani na mshikamano. Niwaombe wahusika, wasimamizi wa amani, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi au tuseme Utawala Bora kwa maana ya Usalama wa Taifa na Idara nyingine, waongeze nguvu sana kwenye jambo hili la amani na usalama. Kwenye kampeni zilizopita, kulijitokeza jambo moja ambalo nafikiri ni jambo la hatari sana kwenye suala la amani, suala udini. Jambo hili lilikuwa baya sana na lilishamiri. Kuna baadhi ya wagombea wa Chama fulani walitumia jambo la udini kama ndio sera yao. Nafikiri hawakuwa na sera nyingine ya kusema kwa bahati mbaya wakatumia udini kama ndio siasa yao ya kugombea nafasi za Ubunge na nafasi nyingine. Lilikuwa jambo baya sana na tusipolisimamia vizuri na kuliondoa, tunahatarisha amani yetu na umoja tulionao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Rais, kama nilivyosema, ameongelea mambo mengi sana karibu mambo yote, jambo moja ni kuhusu kilimo. Kilimo bado ni uti wa mgongo wa nchi yetu. Tumepiga hatua kwenye mambo mengine, madini na mambo mbalimbali lakini kilimo bado ni njia mojawapo kubwa ya uchumi wa nchi yetu. Nashukuru Serikali kwa mipango mingi iliyanayo katika kuboresha kilimo. Kuna Programu ya Kilimo Kwanza na miradi mingi ya kilimo lakini nisisitize kwamba

tuongeze nguvu, wakulima wazidi kusaidiwa. Tuna mipango mingi kama nilivyosema, kuna vocha za kilimo, pembejeo za mbolea, tuzidi kuwaongeza nguvu na kuwahamasisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tusipuuze suala la kilimo cha mashamba makubwa (*estate*), tuwahimize na kuwakaribisha wawekezaji katika eneo hili. Tukipiga hatua kwenye hili, tutafanya vitu vingi. Kwanza, tunaboresha ajira, akija mkulima mkubwa akafungua shamba la ekari 2000, 3000 la mahindi au la maharage au zao lolote, ataajiri Watanzania wengi na pia tutakuwa na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Spika, asubuhi tulisikia Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema kwamba takwimu zilizopo kuna uwezekano tukapata baa la njaa. Tukiwa na wakulima wa mashamba makubwa, tukatumia matreksa, mitambo na mbolea na pembejeo nyingine, tutakuwa na uhakika wa chakula, tutakuwa na ziada, tutauza nje na tutakuwa tumepiga hatua kubwa katika eneo la usalama wa chakula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia mambo mengi na mimi niyachangie, suala la uvuvi. Uvuvi ni njia mojawapo ya kujiletea maendeleo, kama alivyoongelea Rais kwamba tuboreshe uvuvi, tuongeze bidii kwenye uvuvi. Kule kwenye Jimbo langu, kuna vijiji vingi viko Ziwanji, Ziwa Victoria. Kazi kubwa ya wananchi hawa ilikuwa uvuvi kabla ya kuzuiwa kuvua. Sasa hivi hawaruhusiwi kuvua kwa maelezo kwamba wanaharibu mazingira, wanaharibu mazalio ya samaki kwa sababu wana nyavu ambazo haziruhusiwi na vifaa ambavyo ni duni. Sasa mimi nasema kuwazuia haitoshi, Serikali iongeze juhudhi iwasaidie. Kama alikuwa mvuvi mmoja mmoja, waelimishwe, waunganishwe wapate msaada. Tunaruhusu wavuvi wakubwa, wana mitambo mikubwa na maboti makubwa na nyavu nzuri wanavua wanapeleka samaki viwandani, zinakwenda nchi za nje. Tutumie kipato hiki kuwasaidia wakulima wadogo wadogo waweze kuvua, ndio rasilimali yao na wazidi kuboresha michango yao katika uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu, kama tunavyojua, kama walivyoongea wenzangu wengi hapa, elimu ndio msingi wa maendeleo yetu. Serikali yetu imefanya jitihada kubwa sana, naipongeza kwamba imepiga hatua kubwa kwenye elimu, shule za msingi na za awali, vyuo, sekondari na kadhalika. Kila Kata sasa ina sekondari moja, tuongeze juhudhi kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika Walimu walioajiriwa juzi juzi hawa 10,000 tumepata 46 kati yao waliopo leo ni 28 wengine wamefika wakaondoka, wakakimbia. Mazingira ni magumu. Naomba Serikali iongeze bajeti kwenye sekta ya elimu na bajeti hii itumike zaidi kwenye sekondari na hasa kwenye nyumba za Walimu. Maana shule hizi ziko kwenye Kata, hata shule ilipo hata nyumba ya kupanga Mwalimu haipo. Sasa naomba bajeti iongezwe kwenye sekta ya elimu na kipaumbele iwe kwenye nyumba za Walimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa vile muda umeisha, niongelee suala la maji. Hotuba ya Rais imezungumzia suala la maji. Nashukuru Serikali imepiga hatua kubwa sana kwenye maji, miradi inaendelea. Asubuhi kulikuwa na Waziri wa Maji, nikamuuliza mbona kule

Bukoba tulikuwa na miradi kumi ya maji imebaki minne? Akanihakikishia kwamba hata ile mingine sita itakuja, nashukuru, naomba juhudhi hizi ziendelee.

Mheshimiwa Spika, suala la nishati ya umeme, nishati hii ni kubwa sana na ni muhimu kwa maendeleo ya nchi hii. Nishukuru pia kwamba pale Bukoba kuna mradi mkubwa wa kupeleka umeme eneo linaloitwa Ikimba Area. Hata kama sitafaidika na umeme huu lakini mwendo kasi wa ujenzi huu ni mdogo. Naomba kasi iongezeke kusudi angalau mwisho wa mwaka huu mradi huu uwe umekamilika lakini pia kuwe na mpango madhubuti kusaidia wananchi. Juu kwenye nyumba yake unakuta umepita waya wa umeme mwananchi hana umeme, ukimwambia akaweke mwenyewe gharama ile haiwezi. Kuwe na mpango mahsus wa kusaidia wananchi wawezekana kupata namna ambayo wanawenza kuingiza umeme kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii, ahsante. (*Makofî*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hatuwezi kumpa nafasi Mbunge mwingine kuchangia kwa sababu hautoshi. Orodha yetu bado ni ndefu sana. Mpaka sasa ambao bado hawajachangia wako 110. Siku ya Jumatatu na Jumanne, Mawaziri mbalimbali waliguswa na michango yetu watakuwa wanapewa nafasi ya kujaribu ku-*react* katikati maana Wabunge wengine ambao wapo nao pia watakosa nafasi, kama mtaangalia kule *notice board*, orodha itakuwa imebandikwa. Kwa hiyo, sisi tunajitahidi kwenda kufuatana na orodha mtakayoiona kwenye *notice board*. Naona kuna wenzangu wengi sana wanaandika *vi-note* hapa nipe nafasi, nasafiri kesho, nina mganjwa, ukiangalia ni watu 118 sasa ukimpa nafasi, kwa kweli hata kesho angekuwepo asingefikiwa. Kwa hiyo, ni namna tu ya kusema nipe nafasi mimi, siwezi, tunakwenda kwa *list* kama tulivyopanga kule. Kwa hiyo, msiniandikie hii habari ya dharura, msiniandikie kabisa.

(*Hapa kengele ililia*)

SPIKA: Sasa napigiwa kengele? (*Kicheko*)

Msiandike habari ya dharura kwa sababu haya majina tutakuwa tumebandika kule na mimi uzoefu ninao humu ndani watu wengine wanawenza kukuambia hivi, ukamuonea huruma kweli ana mganjwa, anakwenda kutibiwa, akishaongea unamwona yuko hapa hapa halafu anaona hata aibu. Kwa hiyo, jamani muangalie majina kwenye *notice board*, ukienda kuona kule usikate tama lakini tunayabandika na tutakwenda kwa mtiririko huo huo. Kwa hiyo, naomba sana hilo mlizingatie, msiniandikie barua ya kusema mna dharura maana wengi mtabakia. Lakini hii ni hotuba ya Rais, kiko kipindi cha bajeti ndio pale mtazungumza kweli kweli. Maana pale unatafuta hela, maana hapa unaunga mkono maeneo aliyosema Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, huko pia mtapata nafasi ya kuzungumza. Kama tulivyosema, mnawenza pia kuchangia kwa maandishi, kwenye *Hansard* yetu itaonekana kama ulichangia. Kama ukikuta uko mbali na mawazo yako unafikiri ni muhimu sana basi andika kwa maandishi.

Lakini pia Kanuni yetu mojawapo inasema usirudierudie kwa mfano hili suala la kufeli watoto karibu kila aliyesimama amesema, sasa kwani mmesema nini cha zaidi? Nenda kwa mambo ambayo wenzio hawajayazungumzia. Kwa hiyo, unajikuta umerudia sana, umepoteza kile kitu ambacho unafikiria kwenye Jimbo lako pengine kiko *very specific*, usipotuambia sisi hatutajua. Hii ya kufeli, tumeshajua nchi nzima, nenda kwenye *specific* katika maeneo yako, ikusaidie zaidi.

Lingine kuna vitu vingi hatukuwa tumesema na Kanuni wakati mwagine ni vigumu kusoma, nasikia mnasoma sana magazeti na vitabu wakati mjadala unaendelea, Kanuni inakataa. Huwezi ukakazana humu ndani unasoma gazeti au kitabu kisichohusiana na hapa, Kanuni zinakataza.

Asubuhi niliweka mfano mdogo tu wa Mheshimiwa Steven kukatisha kati ya Spika na mzungumzaji, hilo ni kosa yaani unaposimama kuna mzungumzaji nyuma yako na Spika mbele yako basi angalia. Kama utam-*block* Spika unaweza kuitwa kwa jina halafu unaambowi kaa chini. Kwa hiyo, muangalie mnapotoka kama kuna mzungumzaji karibu yako usitoke ama uangalie au tokea upande ule ambao hukatishi kati ya mzungumzaji na Spika, hiyo iko ndani ya Kanuni. Kwa hiyo, tutaendelea kukumbushana vitu vidogo vidogo kama hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Ijumaa tarehe 11 Februari, 2011 Saa
Tatu Asubuhi)*